# Nipashe

Jumamosi Februari 15, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580155

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



## Baba watoto 3 jela miaka 30 kubaka binti darasa 7

UKURASA 3




UKURASA 13

# Uzuiaji maiti hospitali sasa wapigwa 'stop'

• **Waziri** aeleza msimamo wa serikali..... *Endelea uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### PM AONYA MATUMIZI CORONA KUJITAFUTIA UMAARUFU KISIASA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewaasa wanasiasa nchini...

UKURASA WA 3

### 26 KUKAMATWA TUHUMA ZA UFISADI WA MABILIONI SACCOS

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, ameziagiza Taasisi ya...

## Bei samaki yapaa Dar

UKURASA 2



Umati wa wachuuzi wa samaki wakiwa kwenye mnada katika Soko la Samaki la Kimataifa Feri, jijini Dar es Salaam jana, ambapo kitoweo hicho kilionekana kuwa adimu na kusababisha bei yake kupaa. **PICHA: ROMANA MALLYA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play  Download on the App Store

## Laini za simu mil. 10 kuzimwa

UKURASA 2



**MICHEZO** SIMBA, LIPULI HESABU KUTAWALA SAMORA UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Uzuiaji maiti hospitali sasa wapigwa 'stop'

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amepiga marufuku hospitali nchini kuzuia maiti kutokana na gharama za matibabu na badala yake zibuni njia za kudai malipo hayo.

Katazo hilo alilitoa jana jijini Dar es Salaam, alipofanya ziara katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Tawi la Mloganzila, kuangalia kero na vikwazo wanavyopata wagonjwa wanaopatiwa matibabu.

Alisema anafahamu lipo tatizo la wananchi kushindwa kumudu gharama za matibabu na ikizingatiwa kuwa hospitali hiyo inatoa huduma kwanza kabla ya kudai malipo.

"Ni marufuku hospitali kuzuia maiti kwa sababu mgonjwa alishindwa kulipa deni. Watafute utaratibu mwingine wa deni kulipwa bila kuzuia maiti," aliagiza.

Ummy alitoa agizo hilo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wagojwa wanaodaiwa hospitalini hapo baada ya kupatiwa matibabu na hali zao kuimarika.

Alisema hilo ni tatizo katika hospitali nyingi nchini na kwamba serikali inafanyia kazi kuhusu namna ya kuwezesha wananchi wote kupata huduma za matibabu.

Waziri huyo alisema wameshatoa mapendekezo serikalini kuhusu bima ya matibabu kwa wote, lakini serikali imechelewa kutoa majibu kwa sababu wanafanya tathmini ya gharama ambayo kila Mtanzania atamudu na mfuko utatoa huduma.

"Suala la wananchi kushindwa kumudu gharama za matibabu siyo hapa tu, ni la nchi nzima, ni changamoto (tatizo) ambayo serikali inaifanyia kazi, nasi kama wizara tushatoa mapendekezo yetu, serikali imechelewa kutoa uamuzi kwa sababu lazima tufanye tathimini kuhusu gharama na matibabu," alisema.

Alisisitiza kuwa licha ya kuwapo kwa tatizo hilo, wananchi hawapaswi kunyimwa huduma za matibabu wala maiti kuzuiwa.

Mbali na tatizo hilo, Ummy alisema hospitali hiyo pia iko mbali na makazi ya wananchi, akiahidi kuwa suala hilo linafanyiwa kazi na Manispaa ya Ubungo ambayo inajenga kituo cha mabasi kwa lengo la kurahisisha usafiri.

Alisema wingi wa ndugu wa wagonjwa wanaokwenda hospitalini hapo kuona wagonjwa ni tatizo lingine kulingana na miundombinu ya jengo la hospitali hiyo, inayowalazimu kupanda lifti.

"Najua ipo changamoto ya ndugu kulalamika kukaa foleni muda mrefu kusubiri kuwaona wagonjwa wa hii inatokana na miundombinu ya jengo letu hili, lilijengwa kwa mfumo wa nchi za wenzetu ambao watu wawili au watatu huenda kuona wagonjwa.

"Lakini hapa kwetu mgonjwa mmoja wanaenda ndugu 10 hadi 20 kumtizama na hatuwezi kusema tuzuie kwa sababu ndiyo utamaduni wetu.

"Naomba angalieni mpeane zamu, ndugu wote hawawezi kupanda lifti kwa wakati mmoja, ndiyo sababu kuna changamoto hii," alibainisha.

Kuhusu huduma za matibabu zinazotolewa hospitalini hapo, Waziri Ummy alikanusha taarifa kuwa wanaotibu wagonjwa ni madaktari wanafunzi waliopo mafunzoni.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Lawrence Museru, alisema sababu ya kuwapo kwa kashfa ya kuwa hospitali hiyo haina madaktari na wagonjwa wanafariki dunia, ilitokana na mfumo wa awali ulioitambulisha hospitali hiyo kama kituo cha mafunzo kwa wanafunzi wa udaktari.

"Hiyo ni dhana ambayo ilijengeka kwa wananchi, lakini tangu imekuwa hospitali ya MNH, hakuna changamoto hiyo na kuna madaktari bingwa wanaotoa huduma," alisema.



Baadhi ya waombolezaji wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa Waziri wa zamani wa Viwanda na Biashara, Iddi Simba, baada ya kuwasili nyumbani kwake Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana, na baadaye kuzikwa katika makaburi ya Mwinyimkuu, eneo la Magomeni. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Laini za simu mil. 10 kuzimwa

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA), imetangaza kuwa itazifunga laini zingine za simu zaidi ya milioni 10 zenye wamiliki takriban milioni 3.5 kutokana na kutosajiliwa kwa mfumo wa alama za vidole.

Kwa mujibu wa taarifa yao iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA kwa vyombo vya habari, idadi ya laini ambazo hazijasajiliwa kwa mfumo huo ni 10,829,442.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa laini hizo zilisajiliwa kwa kutumia kitambulisho cha mpigakura na Mzanzibari Mkaazi.

"Uhakiki kwa kushirikiana na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) unaendelea na utaratibu wa kuzifunga unatekelezwa," TRCA ilieleza katika taarifa yake hiyo.

Mamlaka hiyo pia ilisema idadi ya laini zilizosajiliwa kwa alama za vidole hadi Jumatano ni 32,948,073, sawa na asilimia 75.3 ya zote.

"Taarifa ya usajili hadi Jumatano ya wiki hii, jumla ya laini zote za simu zilizounganishwa mitandaoni ni 43,777,515, na laini zilizozimwa ni 7,316,445.

"Tayari watumiaji wa laini 1,790,646 wamezirudisha kwa kusajili kwa alama za vidole, hivyo kufanya idadi ya laini zilizozimwa kubakia 5,525,799," ilifafanua.

Uzimaji wa laini za simu ambazo hazijasajiliwa ulikuwa ufanyike Desemba 31, mwaka jana, lakini Rais John Magufuli aliongeza siku 20 na mchakato huo ulikamilika Januari 20 na baada ya hapo TCRA imekuwa ikizizima kwa awamu laini ambazo hazijasajiliwa.

# Bei ya samaki yapaa

**Na Romana Mallya**

SAMAKI na dagaa katika Soko Kuu la Samaki la kimataifa Feri jijini Dar es Saam wamekuwa adimu na kusababisha bei zake kupanda mara dufu.

Bei ya ndoo kubwa ya dagaa wa aina mbalimbali wanaovuliwa Bahari ya Hindi kwa sasa ni kati ya Sh. 80,000 hadi 85,000 huku samaki walio wengi waliopo sokoni hapo wanatokea visiwa vya Mafia na Kilwa.

Nipashe ilifika jana kwenye soko hilo na kushuhudia hali ya upatikanaji wa samaki na dagaa imepungua, huku maofisa uvuvi na wavuvi wenyewe wakitaja sababu ni kipindi cha mbalamwezi.

Akizungumza na gazeti hili sokoni hapo, mmoja wa wauzaji wa dagaa, Adam Issa, ambaye ni mkazi wa Manzese alisema, bei ya dagaa sokoni hapo hadi siku hiyo kwa ndoo kubwa ni Sh. 85,000 wakati kwa kawaida huwa ni Sh. 25,000.

"Kwa kawaida ndoo kubwa ya dagaa huwa kati ya Sh. 25,000 hadi 30,000 lakini kwa sasa ndani ya wiki moja iliyopita imepanda na inauzwa kati ya Sh. 80,000 hadi 85,000. Ukinunua kwa fungu kwa sasa ni kati ya Sh. 2,000 hadi 5,000 wakati awali lilikuwa ni Sh. 1,000 hadi 2,000. Hii inatokana na upatikaji wake kuwa shida.

Issa alisema uhaba huo wa dagaa licha ya kuwaathiri walaji kwa kushindwa kumudu bei, wamekuwa wakikaa nazo sokoni na wakati mwingine kupata hasara.

"Awali, ukinunua ndoo kama hii saa 1:00 asubuhi saa mbili mbele imekwisha lakini kwa sasa unaweza kupita siku hujamaliza kuuza, hii ni hasara kwa sababu tunauza wakiwa wabichi," alisema.

Akielezea hali hiyo, Ofisa Uvuvi sokoni hapo, Mwajuma Moyo, alisema changamoto hiyo imedumu kwa muda wa wiki sasa kutokana na kuwa kipindi cha mbalamwezi au mwezi mkali.

"Kipindi cha mbalamwezi ni kwamba kuanzia giza linapoanza kuingia kunakuwa na mbalamwezi mpaka asubuhi, ikitokea hivyo wavuvi wenye vifaa vya uvuaji kuviegesha feri kwa

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

# Wanaotumia corona kujitafutia kiki ya kisiasa waonywa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewaasa wanasiasa nchini kutotumia mlipuko wa virusi vya corona uliotokea nchini China kujipatia umaarufu wa kisiasa.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, aliwataka Watanzania waendelee kuitegemea serikali katika kupata taarifa za mara kwa mara kuhusu masuala mbalimbali zikiwamo na za mlipuko wa virusi hivyo na kusisitiza "tusiupotoshe umma."

Aliyasema hayo jana baada ya kushiriki swala ya Ijumaa katika msikiti wa Gaddafi, jijini Dodoma na kusisitiza umuhimu wa wananchi kuliombea taifa ili kuliepusha na maafa mbalimbali.

Alisema katika mji wa Wuhan ambako virusi hivyo vilianzia, wapo Watanzania 497 na kwamba wote wapo salama na serikali inaendelea kuwasiliana nao kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na ubalozi.

"Taifa hili ni muhimu sana kwetu na ni msingi wa maisha yetu, hivyo watu wasiwe wanapotosha umma na kuwatia hofu Watanzania, vijana wetu wapo salama. Pia tumejipanga kukabiliana na majanga hayo ikiwa ni pamoja na nzige. Tumuombe sana Mwenyezi Mungu atuepushe"

Wakati huohuo, ugonjwa wa corona umezidi kuongeza hofu duniani baada ya watu 59,804 walikuwa wameambukizwa ugonjwa huo nchini China.

Taarifa ya Ubalozi wa China jijini Dar es Salaam ilisema wagonjwa hao ni wa China Bara na kwamba kati yao 5,911 walipona na kuruhusiwa kutoka hospitalini wakati 1,367 walikufa na 52,526 wanaendelea kupata matibabu.

Ilisema hadi Februari 12 kulikuwa na wagonjwa 13,435 walioshukiwa kuambukizwa

INAENDELEA UK. 8



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (mwenye kofia), akishiriki chakula na wavuvi wa kisiwa cha Siza, akiwa katika ziara yake ya siku tano ya kukaguzi wa miradi ya maendeleo ya afya, maji, elimu na maeneo yalioathiriwa na mvua katika Halmashauri ya Ukerewe, jana. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Baba watoto 3 jela miaka 30 kubaka binti darasa la 7

**Na Daniel Limbe,** CHATO

MAHAKAMA ya Wilaya ya Chato mkoani Geita, imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela, Kabagambe Mihayo, baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mwanafunzi wa darasa la saba.

Mshtakiwa huyo ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Buzirayombo wilayani Chato, alikamatwa na askari polisi Februali 10 na siku tatu baadaye, alifikishwa mahakamani na kusomewa mashtaka ya ubakaji.

Katika kesi hiyo namba 45 ya mwaka 2020, Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Semen Nzigo, alidai mahakamani kuwa mshtakiwa alikuwa akimbaka mwanafunzi huyo (jina tunalo) kwa nyakati tofauti huku akijua kufanya hivyo ni kinyume cha sheria za nchi.

Alidai kitendo cha kushiriki ngono na mtu aliye chini ya miaka 18 ni kosa la jinai kwa mujibu wa Kifungu cha 130(1) na (2)(e) pamoja na Kifungu namba 131(1) cha Sheria ya Makosa ya Jinai.

Mbele ya Mahakama hiyo, mshtakiwa baada ya kusomewa mashtaka ya ubakaji, alikiri kutenda kosa hilo huku akidai kuwa mtoto huyo ambaye ni mwanafunzi wa darasa la saba kwenye Shule ya Msingi Buzirayombo ni mpenzi wake wa muda mrefu.

Sambamba na hilo, alisema uhusiano wao ni kama mke na mume licha ya kutambua kuwa mpenzi wake huyo ni mwanafunzi wa shule ya msingi.

Baada ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Alphonce Kagimbo, kusikiliza maelezo ya pande zote mbili, alisema mahakama hiyo imejiridhisha pasipo shaka kuwa mshtakiwa analo kosa kisheria kwa mujibu wa sheria za nchi.

Kabla ya kutoa hukumu hiyo, mahakama hiyo ilitoa fursa kwa mshtakiwa kujitetea ili apunguziwe adhabu, ambapo alidai kuwa alifanya kitendo hicho kwa kupitiwa na shetani na kwamba ana mke na watoto watatu.

Hata hivyo, licha ya utetezi huo, mahakama hiyo ilimhukumu kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 30 ili liwe fundisho kwa watu wengine wenye kufanya ngono na watu walio na umri wa chini ya miaka 18.

# 26 kukamatwa tuhuma za ufisadi wa mabilioni Saccos

**Na Gideon Mwakanosya,** RUVUMA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, ameziagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na Jeshi la Polisi mkoani humo kuwakamata viongozi kadhaa wa ushirika walioasababishia vyama vyao hasara ya Shilingi bilioni 1.3

Mndeme ameagiza wenyeviti, mameneja na wahasibu wa vyama vya akiba na mikopo (saccos) 26 wanaotuhumiwa kwa ufisadi wa Shilingi bilioni 1.3 kukamatwa mara moja. Aliagiza kukamatwa watumishi hao jana alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa viongozi wa vyama na wanachama wake.

Mndeme alikuwa kwenye mkutano wa viongozi na wanachama wa vyama vya akiba na mikopo vya wilaya ya Songea na Namtumbo uliofanyika Songea.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya kupokea malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wanachama hao ambayo yalihusiana na wanachama wastaafu kutokupatiwa marejesho ya fedha zao walizokuwa wakiweka akiba.

Mkuu huyo wa mkoa alisema kuwa baada ya kupata malalamiko mengi,serikali inachukua hatua kwa kumtaka mrajisi msaidizi wa ushirika wa mkoa wa Ruvuma kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini ukweli wa malalamiko hayo kutokana na kuwapo viashiria vya ubadhirifu wa mamilioni ya fedha za wanachama.

Alifafanua kuwa vyama vya akiba na mikopo 26 kati ya 124 vya mkoa wa Ruvuma vilifanyiwa ubadhirifu na kilichoongoza kulalamikiwa ni Chama cha Akiba na Mikopo cha Walimu Songea Vijijini ambacho wanachama 77 wanadai milioni 73.1. Alisema kufuatia hali hiyo aliamuru kukamatwa kwa wenyeviti, mameneja, wahasibu pamoja na viongozi ambao muda wao ulipita. "Wakamatwe na kuhojiwa ili kufanikisha kupata ufumbuzi wa upotevu wa fedha hizo." Alisema Mkuu wa Mkoa.

Mapema akitoa taarifa ya mikopo na madeni ya vyama vya akiba na mikopo kwa msimu wa mwaka 2018 /2019 mrajisi msaidizi wa vyama vya ushirika wa mkoa wa Ruvuma, Bumi Masuba mbele ya Mkuu wa Mkoa alisema, Ruvuma una vyama vya ushirika 124 .

Alisema kati ya hivyo 38 vipo katika hatua ya kufutwa kufuatia agizo la serikali kuvifuta vyama ambavyo havifanyi kazi hivyo Ruvuma inabakiwa na vyama 86.

Alifafanua kuwa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo haviendeshwi kwa ufanisi kutokana na matatizo mbalimbali kama utunzaji wa kumbukumbu za hesabu, kutopatikana kwa viongozi waadilifu, kutotaka kukaguliwa pamoja na uwepo wa madeni lala yasiyolipika kwa kiasi kikubwa.

Yote hayo alisema yameathiri mzunguko wa fedha na kusababisha kuwapo kwa malalamiko kutoka kwa wanachama, wanaolalamikia kukosa huduma na mikopo kwa mahitaji mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Akichangia hoja kwenye mkutano huo,mmoja wa wanachama wa chama cha akiba na mikopo cha changanyikeni Saccos Mustafa Songambele, alisema kuwa sababu kubwa ya kuwapo kwa madeni katika Saccos hiyo ni kutokana na viongozi kukopesha idadi kubwa ya fedha bila ya kufuata utaratibu tena kuwapa fedha watu ambao si wanachama.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Pili Mande, alisema mara baada ya kumalizika kwa mkutano huo, amewakamata watuhumiwa 18 kwa ajili ya mahojiano zaidi.

# Mshauri elekezi asakwa kuvuna maji

**Na Frank Monyo**

BODI ya Maji Bonde la Wami/Ruvu, imetangaza zabuni ya kumpata mshauri elekezi atakayefanya utafiti jinsi ya kuvuna maji ya mvua ili kuyahifadhi katika chanzo cha maji cha Mzakwe Makutupora.

Chanzo hicho ni pekee cha maji kwa wakazi wa Dodoma, na lengo ni kuendana na ongezeko la watu katika jiji hilo.

Kauli hiyo ilitolewa na Ofisa wa Bodi ya Maji wa Bonde hilo, Simon Ngonyani, wakati akizungumza na Nipashe baada ya bodi hiyo kutembelea chanzo hicho kwa lengo la kujionea changamoto zilizopo na kuzipatia majibu kwa ajili ya kuhakikisha zinatatuliwa.

Ngonyani alisema shughuli za Serikali zote zimehamia Dodoma ambapo ni makao mkuu ya nchi, na wakazi wake wanategemea maji kutoka chini ya ardhi ambapo chanzo cha Mzakwe Makutupola ndio chanzo pekee cha maji kinachotegemewa huku matumizi ya maji yakiongezeka.

"Kwa sasa kuna zabuni ambayo tumetangaza ya kumpata mshauri elekezi afanye utafiti jinsi ya kuvuna maji ya mvua na sisi tuyatibu ili baadae tuyaelekeze katika bonde hili yaingie chini, yaani kama benki ya maji kwa ajili ya matumizi ya baadae na hii inakuwa tahadhari ili chanzo hichi kiwe na maji ya kutosha," alisema Ngonyani.

Aliongeza kuwa Bonde la Wami/Ruvu ina jukumu kubwa la kuhakikisha wanahifadhi chanzo cha Mzakwe ili kiweze kufikia uhitaji wa kutosheleza mahitaji ya wakazi wa Dodoma wakati Wizara ya Maji wakitafuta chanzo kingine cha maji.

Alisema changamoto kubwa katika uhifadhi wa chanzo hicho ni shughuli za kibinadamu kama ufugaji ambapo ulizalisha sumu ambayo inakwenda kwenye maji na hiyo ni hatari kwa watumiaji.

"Watu wajifunze tukiongelea Wami/Ruvu sio Dar es Salaam tu, tunasimamia vyanzo vya maji hadi Dodoma.. Sisi kama Wami/Ruvu tunahakikisha chanzo hichi kinalindwa na kutunzwa kwa ajili ya kutoa maji yenye ubora na salama kwa matumizi ya wakazi wa Dodoma," alisema Ngonyani.




Mkurugenzi wa Sheria na Mambo ya Jamii wa kampuni ya Total Tanzania, Masha Msuya (wapili kushoto), akimpatia zawadi ya maua mmoja wa wateja wa kampuni hiyo, Sara Ndile, wakati kampuni hiyo kwa kushirikiana na Coca Cola walipoungana na dunia katika kusherehekea Siku ya Wapendanao, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Meneja Mauzo wa Kanda wa Coca Cola, Ruqaiya Alibhai (kushoto) na Meneja wa Huduma za maduka na vyakula wa Total, Jane Mwita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kortini tuhuma kumtumia Waziri Mkuu kutakatisha

**Na Hellen Mwango**

WATU watatu wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, ikiwamo kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Sh. milioni 22.9 kwa kutumia jina la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Washtakiwa hao ni mkazi wa Kigamboni, Bahati Malila, mkazi wa Oysterbay, Regina Mambai na mkazi wa Mbezi Jogoo, Godfrey Mtonyi.

Mapema jana, watatu hao kwa pamoja walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi Godfrey Isaya.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mawakili wa Serikali Waandamizi, Wankyo Simon na Mkunde Mshanga.

Katika shtaka la kwanza washtakiwa hao kwa pamoja wanadaiwa kuongoza genge la uhalifu katika tarehe tofauti kati ya Januari 3 na 31 mwaka huu jijini Dar es Salaam kufanya uhalifu.

Katika shtaka la pili ilidaiwa kuwa Januari 14 mwaka huu, washtakiwa wote kwa pamoja kwa nia ya udanganyifu, walishirikiana kutengeneza cheti cha utambuzi wa msaada kwamba kimetolewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, huku wakijua si kweli.

Mshanga alidai kuwa katika shtaka la tatu, Januari 14 mwaka huu, washtakiwa hao walighushi cheti cha utambuzi wa msaada kikionyesha kuwa ni cheti halali kutoka kwa Waziri Mkuu, jambo ambalo si la kweli.

Upande huo wa Jamhuri ulidaiwa kuwa katika shtaka la nne, washtakiwa wote kwa pamoja walishirikiana kwa makusudi kutoa cheti cha uongo kwa

INAENDELEA UK. 8

# Vigogo Chadema Ifakara watimkia CCM

**Na Waandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara, wilayani Kilombero mkoani Morogoro kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mashaka Mbilinyi na madiwani wenzake wawili, wamejivua uanachama wa chama hicho na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mwenyekiti Mbilinyi ambaye alikuwa Diwani wa Kata ya Viwanja Sitini, alitangaza kutimkia CCM akiwa na wenzake juzi mbele ya Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, wakati wa ziara yake ya siku moja mjini Ifakara.

Baada ya kutangaza kujiondoa Chadema, Mbilinyi alikabidhiwa kadi mpya ya CCM na kutoa ahadi kwa Katibu mkuu huyo kuwa yeye na wenzie waliotoka Chadema wataishi katika kiapo walichoapa, hivyo kuomba ushirikiano kutoka kwa wanachama wote wa CCM.

Wengine waliojiondoa Chadema ni aliyekuwa Diwani wa Kata ya Mbasa, Chiza Shungu, Diwani wa Viti Maalum, Digna Nyangile na aliyekuwa mgombea udiwani Kata ya Kibaoni kupitia Chadema mwaka 2015, Clarence Mbyatu maarufu "Manyota".

Mbali na madiwani, wengine waliotimka ni wanachama wa kawaida akiwemo aliyekuwa Mwenyekiti kijiji cha Nyandeo, Baraka Masala na Kamanda wa ulinzi kupitia chama hicho, wilaya Kilombero, Anthony Mwampamba.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Mbilinyi , alidai wamerudi CCM wakiwa si wageni kwani siasa za wilaya ya Kilombero wanazijua na kuwa wanajiunga ili kuongeza nguvu, hivyo kuwaomba wana-CCM wawapokee ili kuendeleza wilaya hiyo kupata maendeleo.

"Katibu Mkuu wa CCM ,natoka Chadema na kuiacha halmashauri ya wilaya ya Mji Ifakara salama na nilimwambia Mkurugenzi wangu kuwa naenda kupumzika Norway, ndio huku CCM," alisema Mbilinyi.

Akiwapokea, Dk. Bashiru aliwapiga marufuku wanachama wa chama hicho kusema kuna CCM asili na CCM wa kuja kwani waasisi wa chama hicho walishafariki na waliobaki ni warithi wa chama, hivyo kuacha kuwatenga wanaorudi kundini.

Alisema wanachama hao wapya wanatakiwa kupokewa na kupewa haki zao zote na wanatakiwa kuwajibika kama wanachama wenzao, na kuwataka wanachama wengine warudi CCM kwani nyumbani kumenoga.

**KIGOGO ATIMULIWA**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Mkoa wa Shinyanga, kimemfukuza uanachama Katibu Mwenezi wa chama hicho Jimbo la Shinyanga Mjini, Charles Shingino, kikimtuhumu kukosa uaminifu kwa chama.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Mwenyekiti wa Chadema Mkoa wa Shinyanga, Emmanuel Ntobi, alisema uamuzi wa kumtimua uanachama umefikiwa na kikao cha Baraza la Uongozi la Chadema Mkoa wa Shinyanga, kilichoketi Februari 11 mwaka huu. Ntobi alidai kikao cha baraza hilo kimejiridhisha na tuhuma za usaliti na utovu wa nidhamu zinazomkabili, hivyo kuamua kumfukuza uanachama.

Katika taarifa yake hiyo, Ntobi alidai uamuzi huo pia umezingatia Katiba ya Chadema ya Mwaka 2016 Ibara ya 5.4(1-3), kinachoeleza namna ambavyo uanachama wa mwanachama wa chama hicho unavyoweza kufika ukomo.

Alisema Shingino kwa sasa hatakiwi kujihusisha na shughuli yoyote inayohusiana na chama na wadhifa aliokuwa nao wa Katibu Mwenezi wa jimbo hilo.

Nipashe ilimtafuta Shingino, ambaye alisema hakubaliani na uamuzi huo kwa kile alichodai haukuzingatia haki kutokana na kutompa fursa ya utetezi, hivyo yeye bado mwanachama halali na kiongozi ndani ya Chadema.

Alidai kama kuna tuhuma dhidi yake, ilitakiwa kumwita kumsomea na kumpatia fursa ya utetezi na si kukiuka katiba ya chama kwa kuamua kutoa uamuzi wenye maslahi yao.

**Imeandikwa na Ashton Balaigwa, MOROGORO, na Neema Sawaka, SHINYANGA**

# TANGAZO

# TATEPA PUBLIC LIMITED COMPANY

## RESULTS FOR THE THE YEAR ENDED 30 SEPTEMBER 2019

### STATEMENTS OF PROFIT OR LOSS ACCOUNTS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME

for the period ended 30 September 2019

| | GROUP | | COMPANY | |
|---|---|---|---|---|
| | 30 Sept 2019 Audited Tzs' 000' | 30-Sept-2018 Audited Tzs' 000' | 30 Sept 2019 Audited Tzs' 000' | 30-Sept-2018 Audited Tzs' 000' |
| **Revenue** | 23,570,168 | 27,656,544 | - | - |
| Cost of sales | (22,172,207) | (18,914,550) | - | - |
| **Gross profit** | **1,397,961** | **8,741,994** | **-** | **-** |
| Other operating income | 314,488 | 231,815 | 141,896 | 700,000 |
| Selling and marketing costs | (2,033,077) | (2,229,631) | | - |
| Administration expenses | (3,980,151) | (3,831,211) | (1,025,714) | (491,909) |
| Fair value loss on embedded derivative | (178,907) | 226,743 | (178,907) | 226,743 |
| Grant amortization | 20,279 | 20,279 | - | - |
| **Operating profit / (loss)** | **(4,459,407)** | **3,159,989** | **(1,062,725)** | **434,834** |
| Finance Costs - net | (1,286,719) | (1,390,992) | (187,155) | (331,439) |
| Exchange profit/(Loss) & Finance income | 105,735 | | 534,577 | 794,724 |
| Profit /(loss) before income tax | (5,640,391) | 1,768,997 | (715,303) | 898,118 |
| Income tax credits /(expenses) | (1,998,790) | (868,288) | - | (37,384) |
| **Profit for the year** | **(7,639,181)** | **900,708** | **(715,303)** | **860,734** |
| Profit / (loss) on disposal of subsidiary KTPC | 1,944,400 | | (5,501,827) | |
| Statement of Comprehensive income | | | | |
| Profit /(loss) for the year | (5,694,781) | 900,708 | (6,217,130) | 860,734 |
| Profit / (loss) for the year | (5,694,781) | 900,708 | (6,217,130) | 860,734 |
| **(Loss)/ profit attributable to:** | | | | |
| Owners of the parent | (2,917,979) | 579,398 | 0 | 0 |
| Non-controlling interests | (2,776,802) | 321,311 | 0 | 0 |
| | **(5,694,781)** | **900,709** | **(6,217,130)** | **860,734** |
| **Other Comprehensive Income:** | | | | |
| Item that will not be seclassified to profit or loss: | | | | |
| - Gain on revaluation of biological assets | - | | | |
| - Actuarial gain / (loss): net of tax | | | | |
| **Total comprehensive income/(loss) for the year** | **(5,694,781)** | **900,709** | **(6,217,130)** | **860,734** |
| **(Loss)/ profit attributable to:** | | | | |
| Owners of the parent | (2,917,979) | 579,398 | | |
| Non-controlling interests | (2,776,802) | 321,311 | | |
| | **(5,694,781)** | **900,709** | | |
| **Dividend:** | | | | |
| Proposed final dividend for the year | | | | |
| Earnings per share attributable to the equity holders of the Company during the year (expressed in Tsh per share) | | | | |
| Basic earnings per share | (156.40) | 31.05 | | |
| Diluted earnings per share | (32.75) | 4.22 | | |

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION

As at 30 September 2019

| | GROUP | | COMPANY | |
|---|---|---|---|---|
| | 30 Sept 2019 Audited Tzs' 000' | 30-Sept-2018 Audited Tzs' 000' | 30 Sept 2019 Audited Tzs' 000' | 30-Sept-2018 Audited Tzs' 000' |
| **CAPITAL EMPLOYED** | | | | |
| Share capital | 466,431 | 466,431 | 466,431 | 466,431 |
| Share premium | 4,048,462 | 4,048,462 | 4,048,462 | 4,048,462 |
| Other reserves | - | (849,984) | - | - |
| Properties revaluation reserve | 582,169 | 595,507 | | |
| Accumulated earnings /(losses) | (14,659,031) | (11,754,389) | (6,250,097) | (32,967) |
| **Equity attributable to owners of Co.** | (9,561,969) | (7,493,973) | (1,735,204) | 4,481,926 |
| Non-controlling interests | (1,713,323) | 929,399 | | |
| **TOTAL EQUITY** | (11,275,292) | (6,564,574) | (1,735,204) | 4,481,926 |
| **Non-current liabilities** | | | | |
| Borrowings | 11,346,457 | 13,924,988 | 8,647,597 | 8,737,864 |
| Deferred capital grant | 150,551 | 170,830 | | |
| Deferred income tax liabilities | 139,177 | 138,421 | | |
| Retirement benefit obligations | 826,678 | 768,726 | 6,583 | 4,222 |
| | 12,462,863 | 15,002,965 | 8,654,180 | 8,742,086 |
| | 1,187,571 | 8,438,391 | 6,918,976 | 13,224,012 |
| **REPRESENTED BY** | | | | |
| **Non-current assets** | | | | |
| Property, plant and equipment | 9,763,675 | 10,010,733 | | |
| Intangible asset | | 4,727 | | |
| Investment in subsidiaries | | | 5,783,271 | 11,845,034 |
| Loan receivable | 279,244 | 391,628 | | |
| Deferred income tax asset | | 1,995,224 | | |
| | **10,042,919** | **12,402,312** | **5,783,271** | **11,845,034** |
| **Current Assets** | | | | |
| Inventories | 4,427,019 | 5,875,913 | | |
| Trade and other receivables | 5,383,758 | 4,638,291 | 1,750,559 | 1,684,566 |
| Loan receivable | | - | - | - |
| Prepaid land rent | 20,481 | 7,066 | | - |
| Cash and cash equivalents | 51,644 | 157,598 | 29,989 | 13,306 |
| Tax recoverable | 466,606 | 401,701 | 374,353 | 372,276 |
| | **10,349,508** | **11,080,569** | **2,154,901** | **2,070,148** |
| **Current liabilities** | | | | |
| Embedded derivative | 302,618 | 123,711 | 302,619 | 123,711 |
| Borrowings | 14,409,204 | 10,170,605 | | |
| Trade and other payables | 4,493,034 | 4,750,174 | 716,577 | 567,458 |
| | 19,204,856 | 15,044,490 | 1,019,196 | 691,169 |
| **Net current liabilities** | (8,855,348) | (3,963,921) | 1,135,705 | 1,378,979 |
| | **1,187,571** | **8,438,391** | **6,918,976** | **13,224,012** |

### STATEMENT OF CASH FLOWS

for the period ended 30 September 2019

| | GROUP | | COMPANY | |
|---|---|---|---|---|
| | 30 Sept 2019 Audited Tzs' 000' | 30-Sept-2018 Audited Tzs' 000' | 30 Sept 2019 Audited Tzs' 000' | 30-Sept-2018 Audited Tzs' 000' |
| **Cash from Operating Activities** | | | | |
| Profit /(loss) before tax | (5,694,781) | 900,708 | (6,217,130) | 860,734 |
| Adjustments for : | | | | |
| Income tax expenses recognised in P & L | 1,998,790 | 868,288 | | 37,384 |
| Fair value loss on embedded derivatives | 178,907 | (226,742) | 178,907 | (226,742) |
| Depreciation | 648,902 | 655,418 | - | - |
| Amortisation of deferred capital grant | (20,279) | (20,279) | - | - |
| Amortisation of prepaid land rent | (13,415) | (322) | | |
| Employees Gratuity | (57,953) | (122,082) | | |
| Interest Expenses | 1,286,719 | 1,095,438 | 149,831 | 167,438 |
| Interest income | - | | (164,480) | (193,475) |
| Tax adjustment | - | | - | |
| Gain on disposal of property, plant & equipment | - | (8,729) | | |
| Unrealised exchange loss on terms loans | (105,735) | 295,554 | 37,324 | 164,002 |
| Other noncash (investment in KTPC W/O) | 813,116 | 116,534 | 6,061,763 | |
| Changes in working capital: | | | | |
| Loans from related parties | | | | 2,201,314 |
| Inventories | 1,448,894 | (1,109,417) | | |
| Receivables | (758,396) | (2,231,257) | (103,317) | (557,366) |
| Payables | (257,139) | (1,006,501) | 151,480 | (229,932) |
| **Cash generated from operating activities** | **(532,370)** | **(793,389)** | **94,378** | **2,223,356** |
| Interst paid | (1,069,812) | (1,095,438) | (149,831) | (167,438) |
| Income tax paid | (62,077) | (926,724) | (2,077) | (68,673) |
| Net cash generated/(utilised in) from Operating activities | (1,664,259) | (2,815,551) | (57,530) | 1,987,246 |
| **Cash flow from investing activities** | | | | |
| Purchase of property, plant and equipment | (504,136) | (358,187) | - | - |
| Investment in Subsidiaries/ disposal proceeds | 228,956 | | 228,956 | (3,192,870) |
| Repayment of loan advanced to Moravian | - | | | |
| Loans to third parties | 112,384 | 49,763 | | - |
| Proceeds from sale of property, plant & equipment | - | | | |
| Net cash (utilized in) /generated from investing activities | (162,796) | (308,424) | 228,956 | (3,192,870) |
| **Cash flow from Financing Activities** | | | | |
| Proceeds /(repayment) borrowings | 879,396 | (1,026,356) | (201,331) | 1,057,915 |
| Repayment of borrowings | | | - | - |
| Cash used for purchase of shares | | | | |
| Effects of exchange rates on loan | 83,792 | 144,333 | 46,588 | 135,597 |
| Proceeds from issue of shares | | 1,374,947 | | |
| Dividends paid | | | | |
| **Net cash flow from Financing Activities** | **963,188** | **492,924** | **(154,743)** | **1,193,512** |
| **Net movement in cash and cash equivalents** | **(863,867)** | **(2,631,051)** | **16,683** | **(12,112)** |
| **Cash and cash equivalents at start of period** | **(8,293,413)** | **(5,662,362)** | **13,305** | **25,417** |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | **(9,157,280)** | **(8,293,413)** | **29,988** | **13,305** |

### STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY

for the period ended 30 September 2019

| | Share capital | Share premium | Accum. Losses | Properties revaluation reserve | Othe reserves | Non-controlling interests | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Group** | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' |
| **For the period ended** | | | | | | | |
| **30 September 2019** | | | | | | | |
| At start of year | 466,431 | 4,048,462 | (11,754,389) | 608,845 | (863,322) | 929,398 | (6,564,574) |
| Comprehensive income | | | (2,917,979) | | | (2,776,802) | (5,694,781) |
| Profit /(loss) for the period | | | | | | | - |
| Other comprehensive income | | | | | | | - |
| Elimination reseres on KTPC sale | | | | | 849,984 | | 849,984 |
| Elimination noncontrolling interest KTPC | | | | | | 134,080 | 134,080 |
| Amortisation of excess depreciation revaluation | | | 13,338 | (13,338) | | | |
| **As at 30 September 2019** | **466,431** | **4,048,462** | **(14,659,030)** | **595,507** | **(13,338)** | **(1,713,324)** | **(11,275,291)** |
| **For the year ended** | | | | | | | |
| 30 September 2018 | | | | | | | |
| At start of year | 466,431 | 4,048,462 | (12,347,125) | 608,845 | (838,250) | (510,940) | (8,572,577) |
| Comprehensive income | | | | | | | |
| Profit /(Loss) for the year | - | - | 579,398 | | | 321,311 | 900,709 |
| Other comprehensive income | | | | | | | |
| Amortizations | | | 13,338 | | (13,338) | | - |
| Changegs in ownership of subsidiary | | | | | (11,734) | 1,419,028 | 1,407,294 |
| Final dividend | | | | | | (300,000) | (300,000) |
| **As at 30 Septemer 2018** | **466,431** | **4,048,462** | **(11,754,389)** | **608,845** | **(863,322)** | **929,398** | **(6,564,574)** |

| **Company** | Share capital | Share premium | Retained earnings | Total |
|---|---|---|---|---|
| | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' |
| **30 September 2019** | | | | |
| At start of year | 466,431 | 4,048,462 | (32,968) | 4,481,925 |
| Comprehensive income | | | (6,217,130) | (6,217,130) |
| Loss for the period | | | | - |
| Actuarial loss net of tax | | | - | - |
| **As at 30 September 2019** | **466,431** | **4,048,462** | **(6,250,098)** | **(1,735,205)** |
| **30 September 2018** | | | | |
| At start of year | 466,431 | 4,048,462 | (893,702) | 3,621,190 |
| Comprehensive income | - | - | | - |
| Profit / (loss) for the year | - | - | 860,734 | 860,734 |
| **As at 30 September 2018** | **466,431** | **4,048,462** | **(32,968)** | **4,481,924** |

**Note : The audited accounts were signed by the Auditors on 14 January 2020.**

**The Annual General Meeting of sharehlders will be held on 30 April 2020 at 11:00 hours at Protea Hotel, Courtyard, Sea View Ocean Road, Dar es Salaam. Notice will be mailed in due course.**

Vimalendu Kumar Tewari
Company Secretary
**Tatepa Limited**
P.O. Box 1344,
Dar es Salaam.
28 March 2020

215631802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TPLB imulike upya adhabu kwa waamuzi

**KWA** mara nyingine tena Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) katika kikao chake cha Februari 10, mwaka huo ilipitia mwenendo na matukio mbalimbali ya ligi na kisha juzi kufanya uamuzi wa kuwafungia baadhi ya waamuzi.

Kamati hiyo, ilibaini katika mechi namba 190 wakati Yanga ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Lipuli FC mwamuzi wa kati, Abubakar Mturo na mwamuzi msaidizi namba mbili, Joseph Pombe walishindwa kumudu pambano hilo.

Kubwa katika mchezo huo, waamuzi hao walishindwa kutafsiri vyema mpira uliokuwa umeibua mvutano mkubwa kuwa ni goli au si goli baada ya kipa wa Yanga, Metacha Mnata kuukandalimiza mpira upande wa ndani wa mlingoti.

Mturo na Pombe kwa pamoja walishauriana na kuamuru ipigwe kona, uamuzi ambao ulishangaza wadau na mashabiki wengi wa soka ndani na hata nje ya nchi waliokuwa wakifuatilia kupitia luninga.

Hata hivyo, kwa kuzingatia Kanuni namba 39(1) ya Ligi Kuu Kuhusu Udhibiti wa Waamuzi, Kamati hiyo ya TPLB ikawafungia Mturo na Pombe kwa kipindi cha miezi mitatu kila mmoja.

Kifungo kwa waamuzi hao wawili kimekuja ikiwa ni siku chache tangu kamati hiyo ilipomfungia kwa kipindi cha miaka mitatu mwamuzi namba mbili, Kassim Shafisha wa mechi kati ya Simba na Namungo FC.

Safisha alikumbwa na adhabu hiyo kwa kushindwa kutafsiri vema sheria 17 za soka kwa upande wa kuotea (offside) baada ya kulikubali bao la kuotea la Meddie Kagere wa Simba.

Kwa ujumla, Nipashe tunaipongeza TPLB kwa hatua ambazo imeanza kuzichukua kwa waamuzi kwani walikuwa wanalipeleka soka letu sehemu isiyoyojulikana.

Tunaamini adhabu hizo zitawaamsha waamuzi na kurudi katika mstari na hatimaye timu kushinda kwa uwezo wake uwanjani na si kwa kutegemea mbeleko ama makosa ya waamuzi.

Lakini pia tunaiomba TPLB inapotoa adhabu hizi kuzingatia kanuni zaidi na kutoangalia sura, undugu ama urafiki, kwani namna inavyotoa adhabu hizo kunazua maswali mengi.

Hii ni kutokana na waamuzi wa mechi dhidi ya Yanga na Lipuli FC, Mturo na Pombe na yule wa mchezo kati ya Simba na Namungo FC, Shafisha, makosa yao yote ni kushindwa kutafsiri sheria, lakini adhabu zikionekana kutofautiana sana.


Kitendo cha TPLB kumfungia Shafisha kwa kipindi cha miaka mitatu huku Mturo na Pombe wakifungiwa kwa miezi mitatu kila mmoja kwetu sisi Nipashe tunaona adhabu hiyo ilitolewa kimhemko zaidi.

Tunatambua suala la kubaini mchezaji kaotea ama la ni kitendo ambacho kinatokea kwa haraka zaidi na ndiyo maana wenzetu nchi zilizoendelea kisoka wameamua kuweka teknolojia ya video kumsaidia mwamuzi, VAR.

Ikumbukwe pia kuna makosa ya kiubinadamu, hivyo Nipashe tulitarajia kuona adhabu ya Shafisha ikiwa ndogo zaidi kuliko hii ya Mturo na Pombe, ambao walichukua dakika kadhaa kujadiliana uwanjani kabla ya kufikia uamuzi wa kuamuru ipigwe kona, lakini mambo yamekuwa tofauti.

Tunasema hivyo kwa sababu hata watoto wanaocheza soka mchangani hadi leo wakiitazama video ya tukio hilo la mechi ya Yanga na Lipuli wanahoji ilikuaje waamuzi hao kuamuru itengwe kona, lakini kwa bao la Kagere linahitaji umakini kubaini aliotea na kama mshika kibendera alipepesa macho ama alizembea kwenda na kasi ya mpira, ni wazi asingeweza kubaini kama aliotea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tucheze mpira badala ya kupenda kulalamika

Na Adam Fungamwango

**MBALI** na kutoa adhabu mbalimbali kwa wachezaji, makocha na waamuzi, Kamati ya Usimamizi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania, imewatia hatiani wasemaji wa klabu kubwa mbili za Simba na Yanga.

Hao ni Haji Manara wa Simba na Antonio Nugaz wa Yanga.

Hawa wanapelekwa kwenye Kamati ya Nidhamu ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF).

Kwenye kikao chao kilichokaa hivi karibuni, Kamati hiyo inawatuhumu wasemaji hao kwa madai wamekuwa wakishutumu na kutoa matamshi yenye kukashifu na kudhalilisha viongozi Chapa ya Ligi na Taasisi kwa ujumla kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa vipindi tofauti.

Mkumbo wa kupelekwa huko kwa makosa kama hayo, pia yamewakumba makocha wawili, Luc Aymael wa Yanga na Thierry Hitimana wa Namungo.

Binafsi niipongeze Kamati hiyo kwa kuamua kuwapeleka makocha na wasemaji hayo kwenye Kamati nyingine ili kama wana makosa basi waadhibiwe ili iwe fundisho kwa wengine.

Haiwezekani viongozi nao wawe ni watu wa kulalamika lalamika kama vile mashabiki.

Mimi ninavyojua ni kuwa kama timu haikufanyiwa haki, viongozi wanajua nini cha kufanya. Ni kuandika barua rasmi ya kulalamikia kile unachoona kuwa hakikuwa sawa na kwa miaka mingi ndivyo ilivyokuwa ikifanywa.

Kwa miaka ya karibuni kumekuwa na baadhi ya viongozi wamekuwa wakiishutumu waziwazi TFF, waamuzi au Bodi ya Ligi tena bila ushahidi, halafu hawaandiki barua ya malalamiko, badala yake wao wanakuwa wanatumia zaidi vyombo vya habari kuwasilisha wanachokiona.

Nadhani nia yao ni kuwasilisha ujumbe kwa wanachama na mashabiki wao ambao nao wanakichukua kama kilivyo na kuanza kusambaza kwenye mitandao ya kijamii kiasi cha kuzidisha mlolongo wa mlalamiko na mihemko.

Kwa siku za karibuni kwenye Ligi Kuu kumekuwa na tabia ya makocha na viongozi kulalamika sana, mara timu fulani inabebwa, au tunaonewa, wengine wanakwenda mbali zaidi wanatuhumu kuwa ndani ya vyumba vya kubadilishia nguo kumepuliziwa dawa, au kuna harufu kali.

Malalamiko yote haya mimi nadhani kama kweli yapo ilibidi yawasilishwe kimaandishi, ili utafutwe ushahidi, au hata kama mlalamikaji akipeleka ushahidi usio na shaka ni sawa, kuliko kulalamika au kutuhumu watu kwa hisia tu.

Mfano kama tuhuma za kupulizia dawa kwenye vyumba vya kuvalia wachezaji ilikuwa ni suala jepesi tu.

Kocha yoyote au kiongozi anayetaka kuliongelea suala hilo, awe amefuatana na daktari yoyote ambaye ameingia kwenye chumba hicho na kugundua kuwa kuna harufu isiyo ya kawaida na atuambie ni harufu ya dawa gani, huwa inatumika kwa ugonjwa gani, na anadhani kupulizwa kwenye vyumba vya wachezaji lengo ni nini, ina athali gani kwa wachezaji na binadamu kwa ujumla.

Hapo ndipo uchunguzi unapoweza kufanyika ili kubaini jambo hilo. Ikumbukwe uchunguzi ni suala linalohitaji muda na pesa, hivyo haiwezekani tu mtu asiye na utaalamu aseme kuna harufu haielewiki, basi moja kwa moja uchunguzi ufanyike.

Kuhusu waamuzi nadhani tayari suala hili limeshaanza kushughulikiwa, kwani tayari baadhi wameshaanza kukutana na rungu.

Ifike wakati viongozi na makocha wawatayarishe wachezaji kucheza soka, badala ya kuonekana kulalamika kila kukicha kuja na staili mpya, hii inaleta sintofahamu na chuki kwa mashabiki, badala ya upendo na amani.

Haiwezekani TFF, Bodi ya Ligi, waamuzi wako sahihi timu yao inaposhinda tu, lakini ikifungwa basi inageuka kuwa haifai, haielewiki na inawahujumu.

Itafika wakati wakawaambukiza hata wachezaji ambao wakipoteza mechi badala ya kuangalia mapungufu yao, wao wataona ni kama wamehijumiwa tu.

Hakuna timu yoyote duniani ambayo haifungwi.

Hata Barcelona na Real Madrid zinafungwa, tena na timu za kawaida, sasa iweze Simba au Yanga zikifungwa inakuwa nongwa, kila mmoja anaonekana mbaya?

# MATANGAZO


WOMEN FUND TANZANIA
Empowering Local Women Heroes

THE REGISTERED TRUSTEE OF WOMEN FUND TANZANIA (WFT-TRUST)
FEBRUARY 2020

## WITO YA MAOMBI YA RUZUKU

**KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KUKUZA NA KUIMARISHA UPATIKANAJI WA HAKI ZA WANAWAKE, WASICHANA NA WATOTO KATIKA MUKTADHA WA UTEKELEZAJI WA MTAKUWWA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA**

**I. UTANGULIZI**

The registered Trustee of Women Fund Tanzania (WFT-Trust) ni mfuko unaotoa ruzuku kwa maswala ya haki za wanawake uliosajiliwa mnamo 2008 kama shirika lisilo la kiserikali, mnamo Septemba 2019 ilisajiliwa upya kama Wadhamini waliosajiliwa wa Mfuko wa Wanawake Tanzania. Mfuko unazingatia kusaidia utekelezaji wa miradi ambayo inalenga kukuza upatikanaji wa haki za wanawake, wasichana na watoto na kwa kuchagiza mabadiliko chanya katika jamii kuhusu haki za wanawake ,wasichana na watoto kwa kuchangia ujenzi wa TAPO la wanawake kimapinduzi Tanzania na harakati za kuleta usawa wa kijinsia kwa kuimarisha harakati za wasichana na wanawake nchini kwa lengo la kukuza uwezo juu ya maswala na haki za wanawake, wasichana na watoto Tanzania.

Katika wito huu ,WFT-Trust itatoa ruzuku kwa taasisi, mashirika ya kijamii na kiraia au vikundi vitakavyokidhi vigezo na masharti ambavyo vinatekeleza shughuli mbalimbali za kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto chini ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto ( MTAKUWWA) katika Halmashauri ya wilaya ya Shinyanga.

Mashirika ya kijamii/ vikundi yenye vigezo yanakaribishwa kulete maandiko yao ya kuomba ruzuku kwa ajili ya utekelezaji wa afua zilizopo ndani ya MTAKUWWA na zinazotekelezwa ndani ya halmashauri ya wilaya ya Shinyanga kupitia michakato mbalimbali ya utekelezaji huo.Lengo kuu ya ufadhili huu ni kusaidia kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na Watoto kwa njia shirikisha na jumuishi kama zilivyoainishwa ndani ya MTAKUWWA.

Maswala mengine yanayoweza kuombewa ruzuku ni pamoja na michakato na mikakati ya kuboresha utekelezaji wa mpango wa MTAKUWWA ndani ya halmashauri husika. Mikakati hiyo inaweza kuwa na lengo la kuongeza umiliki na uwezo wawanajamii kushiriki na kushika hatamu za utekelezaji na kujengea uwezo wa watendaji wa Serikali za Mitaa na wengine (kama vile Asasi za kijamii, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, jamii na wadau wengine) katika muundo wa MTAKUWWA ili kuongeza ufanisi na kukuza mifumo shirikishi ili kuhakikisha ushiriki wa jamii katika utekelezaji wa MTAKUWWA.

**II. WFT-TRUST INATARAJIA RUZUKU ZITAKAZOTOLEWA ZIENDE KUTEKELEZA MIKAKATI IFUATAYO.**

- Kuchagiza utekelezaji wa masuala ya jamii yanayohusiana na MTAKUWWA pamoja na kuhakikisha kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya tatizo linaloshughulikiwa, mikakati ya utekelezaji pamoja na matokeo yanayopimika kutokana nautekelezaji wa mradi husika.
- Kuonesha uendelevu wa shughuli zilizofadhiliwa,ubunifu pamoja na jinsi ya kuonesha ni jinsi gani kuna uwezekano wa shughuli hizo kutumika kama mfano kwa maeneo mengine kwa kiwangu cha juu zaidi.
- Kuonesha mchango wake katika jitihada za ujenzi wa TAPO la pamoja baina ya watetezi wa haki za wanawake na watoto na pia katika kupigania kutokomeza aina zote za uklatili dhidi ya wanawake na watoto kwa pamoja na haswa kwa kuimarisha muingiliano baina ya mashirika na asasi hizo za utetezi.katika (harakati/ vuguvugu la pamoja) kwa lengo la kutengeneza / kuimarisha mitandao na majukwaa ya kuleta nguvu ya pamoja
- Kujenga ari ya umiliki na uwezo wa kuimarisha umiliki wa mchakato wa MTAKUWWA na miundo yake ya utekelezaji ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga
- Kukuza mikakati na jitihada zenye kuimarisha ujenzi wa TAPO la wanawake na Watoto.

**III. VIGEZO MUHIMU KWA WAOMBAJI WA RUZUKU**

- Mashirika ya kijamii / Vikundi vya kijamii vinavyotambulika kisheria na wanaotekeleza shughuli zake ndani ya halmashauri ya wilaya ya Shinyanga.
- Mashirika ya kijamii/ vikundi vya kijamii ambavyo vimekuwa wakitekeleza shughuli za MTAKUWWA katika halmashauri ya wilaya ya Shinyanga.
- Mashirika ya kijamii/ vikundi vya kijamii yenye mtazamo kama wa WFT - Trust katika kuondoa taratibu za kibaguzi na kuleta usawa wa kijinsia ili kuondoa udhalilishaji na ukatili kwa wanawake na Watoto, na ambao shughuli zao zinalandana na maudhui ya shirika la WFT-Trust.
- Taasisi nyingine zinazotambulika kisheria zenye uhalali na fursa za kutekeleza na / au kusimamia utekelezaji wa MTAKUWWA ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

**IV. MADIRISHA YA UFADHILI**

**DIRISHA DOGO LA UFADHILI**

- Kiwango cha ruzuku inayotolewa (TSH 10,000,000 – TSH 15,000,000)
- Muda wa kutekeleza mradi/shughuli (miezi 0 - 3)
- Sifa – Ruzuku katika dirisha hili zinaweza kuombwa na Mashirika / Taasisi zinazotekeleza na kusimamia mikakati ya muda mfupi ya utekelezaji wa MTAKUWWA.

**DIRISHA LA KATI LA UFADHILI**

- Kiwango chauzuku inayotolewa ni kati ya ( TSH 16,000,000- TSH 50,000,000)
- Muda wa kutekeleza mradi kuanzia miezi 6 hadi mwaka mmoja
- Sifa - Ruzuku katika dirisha hili zinaweza kuombwa na Mashirika / Taasisi zinazotekeleza na kusimamia mikakati ya muda wa kati katika utekelezaji wa MTAKUWWA

**JINSI YA KUOMBA RUZUKU**

Waombaji wa ruzuku wafuate hatua zifuatazo:

1. Kuwasilisha Andiko la Mradi (lisilozidi kurasa 5-7) likielezea mradi pendekezwa utakaotelezwa
2. Andiko la mradi litumwe na viambatanisho vifuatavyo:
   - Nakala ya cheti cha usajili cha shirika/kikundi
   - Nakala ya katiba ya shirika/ kikundi
   - Taarifa ya karibuni ya akaunti ya benki ya shirika/ kikundi
3. Maombi yote yatumwe kwa kutumia fomu ya muongozo wa maombi ya ruzuku inayopatikana katika tovuti ya WFT-Trust: www.wft.or.tz . Fomu pia zinapatikana katika ofisi za WFT-Trust zilizopo Jengo jipya la NSSF MAFAO House barabara ya mwanza, Ghorofa ya kwanza ( muda wa kazi)

   Maombi yatumwe kwa barua barua pepe: grants@wft.or.tz kichwa cha habari kisomeke "NPA VAWC SHINYANGA "

   **Ama kwa sanduku la barua**
   **Mkurugenzi Mtendaji, WFT-Trust,**
   **S. L. P 79235, Dar es Salaam**

   Kwa maelezo Zaidi unaweza kuwasiliana na WFT-Trust kwa nambari : +255 753 912130.

4. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **29 Februari 2020,** saa kumi na moja jioni

* Waombaji wote watajulishwa kuhusu kupokelewa kwa maombi yao na kuhusu hatua inayofuata katika mchakato wa kupata ruzuku kabla ya tarehe **20 Machi 2020.**

215632102

WOMEN FUND TANZANIA
Empowering Local Women Heroes

THE REGISTERED TRUSTEE OF WOMEN FUND TANZANIA (WFT-TRUST)

**TANGAZO LA MAOMBI YA RUZUKU ZA MIRADI KATIKA KUKUZA UELEWA WA HAKI ZA WANAWAKE, WASICHANA NA WATOTO TANZANIA**

The registered Trustee of Women Fund Tanzania (WFT-Trust) ni mfuko unaotoa ruzuku kwa maswala ya haki za wanawake uliosajiliwa mnamo 2008 kama shirika lisilo la kiserikali, mnamo Septemba 2019 ilisajiliwa upya kama Wadhamini waliosajiliwa wa Mfuko wa Wanawake Tanzania. Mfuko unazingatia kusaidia utekelezaji wa miradi ambayo inalenga kukuza upatikanaji wa haki za wanawake, Wasichana na Watoto na kwa kuchagiza mabadiliko chanya katika jamii kuhusu haki za wanawake ,wasichana na watoto na pia kuchangia ujenzi wa TAPO la wanawake kimapinduzi Tanzania na harakati za kuleta usawa wa kijinsia kwa kuimarisha harakati za wasichana na wanawake nchini, kwa lengo la kukuza uwezo juu ya maswala na haki za wanawake, wasichana na watoto Tanzania.

WFT-Trust inakaribisha maombi kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali, vikundi vilivyosajiliwa na haswa yaliyo katika ngazi ya jamii yanalolenga kukuza haki za wanawake, wasichana na watoto, kuomba fedha ili kufanya kazi kwenye maeneo husika.

Yafuatayo chini ya madirisha yake matatu ya ufadhili:

- Uimarishaji wa tapo/ujenzi wa nguvu za pamoja katika kuwezesha harakati za kuandaa, utetezi na sera/ushiriki wa kisheria katika ngazi tofauti.
- Uongozi na haki za uchaguzi na uongozi kwa wanawake, wasichana, pamoja na vijana na vikundi vingine vilivyo pembezoni katika ngazi za mitaa na kitaifa
- Haki za uwezeshaji uchumi kwa wanawake na wasichana ikiwa ni pamoja na kukuza haki zao na ushiriki wa wanawake na wasichana katika tasnia mbalimbali (Madini, Mafuta, na Gesi) kupitia umoja, Jukwaa la VICOBA, harakati za wakulima/wasichana.
- Haki ya mazingira na usawa wa jinsia na hatua za kuimarisha sauti na ushiriki wa wanawake, wasichana na watoto katika kushughulikia (sera) maswala ya mabadiliko ya hali ya hewa, haki za ardhi, nishati, maji na nyingine zinazohusiana.
- Upingaji wa ukatili wa jinsia dhidi ya wanawake, wasichana na watoto ikiwemo miradi yenye lengo la upingaji wa maswala ya ngono katika ngazi mbalimbali
- Kukuza uelewa wa haki ya elimu kwa wasichana, watoto hasa wale wanaoishi katika mazingira magumu (yakiwemo mazingira ya Uhamiaji)
- Kukuza utafiti na utunzaji wa kumbukumbu(ke-storia) za wanawake na wasichana ili kutokeza mchango wao katika sekta mbalimbali za jamii
- Kutokeza agenda za haki za wanawake, wasichana, watoto na jamii kwenye siku za maadhimisho maalumu ikiwa ni pamoja na siku za kumbukumbu za kimataifa/kitaifa/kikanda ndani ya nchi kama Wiki ya 8 Machi, Juni 16 Siku ya Watoto wa Kiafrika, Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike Oktoba/Novemba na Siku 16 za Uanaharakati wa Kukutaa Ukatili wa Jinsia nchini, na shughuli mbalimbali za kuadhimisha miaka 25 baada ya Mkutano wa Beijing.

Tunatoa Ruzuku kwa Kupitia Madirisha Yafuatayo:

**1.DIRISHA DOGO LA UFADHILI (TSH 10,000,000 – TSH 15,000,000)**

Dirisha hili ni kwa ajili ya asasi na mashirika ya kijamii ya kutetea haki za wanawake, wasichana na watoto, na vikundi vya wanaharakati vilivyosajiliwa walio katika maeneo ya vijijini na mijini. Dirisha hili linafunguliwa pia kwa vikundi vya jamii yanayoanza, na yenye nia ya kujenga uwezo wao wa kiundeshaji na wa kukuza uhamasishaji unaopelekea kukuza haki za wanawake, wasichana na watoto katika jamii zao.

Waombaji wanaostahili kuomba ruzuku chini ya dirisha hili wanahitaji kuzingatia yafuatayo:

- Muda wa utekelezaji/mradi wa kutekelezwa kati ya miezi 0 hadi 3
- Shughuli za mradi zenye makusudio ya kuibua/kutoa sauti kuhusu maswala ya wanawake, wasichana na watoto, pamoja na wale waliotengwa na walio katika mazingira magumu katika jamii
- Waombaji wa mara ya kwanza kutoka katika kikundi cha jamii.

**2. DIRISHA LA KATI LA UFADHILI (TSH 16,000,000 - 50,000,000)**

Waombaji wanaostahili kuomba ruzuku chini ya dirisha hili wanahitaji kuzingatia yafuatayo:

- Pendekezo la mradi chini ya dirisha hili linapaswa kuzingatia hatua za kusaidia wanawake, wasichana kwa kupitia mashirika na vikundi vyao kukuza haki za wanawake, wasichana na watoto kwa njia ya kujenga/kuimarisha uwezo halisi wa dhana na shirika, utaalamu, mitandao na ushiriki wa maarifa na harakati za wanawake na wasichana.
- Muda wa utekelezaji wa mradi unaopata ruzuku kwa kupitia dirisha hili unapaswa kuwa kati ya miezi 6 na mwaka 1
- Mradi utakaopata ruzuku kwa kupitia dirisha hili uonyeshe kwa uchambuzi wa jinsi lengo/malengo yatakavyo polekea kuwezesha walengwa , hasa wale waliotengwa au makundi maalumu la kutoa sauti kwa wanawake waliotengwa kama ilivyoainishwa kwenye wito wa ombi.
- Dirisha hili liko wazi kwa mashirika ya wanawake, wasichana na watoto katika ngazi za taifa na za jamii ambazo zinahitaji ruzuku za kuimarisha mashirika au kujenga mbinu za kimkakati za kuendeleza harakati za walengwa wao, ikiwemo kujenga nguvu za pamoja.
- Waombaji wa ruzuku chini ya dirisha hili lazima wawe wamesajiliwa kisheria kama vile, mashirika au vikundi vya Wanawake, vikundi vya Wanaharakati n.k.
- Watendaji wa shirika wawe na uzoefu wa kutekeleza mradi huo kwa mafanikio, ikiwemo kuwa na uelewa wa kimsingi katika ajenda wanayofanyia kazi, kuweka rekodi nzuri katika usimamizi wa kifedha na njia za kimfumo
- Yawe ni mashirika/taasisi au vikundi yanayooendeshwa na kuongozwa na wanawake na wasichana kwa asilimia kubwa

**3. DIRISHA LA UFADHILI LA KIMKAKATI (TSH 51,000,000 - 250,000,000)**

Chini ya dirisha hili, tunatafuta kuwekeza na kushirikiana na Asasi, Mitandao na majukwaa katika ngazi ya taifa na jamii, yanayotetea haki za wanawake, wasichana na watoto na ambayo yana uwezo wa ujenzi wa harakati-jumuishi zinazofikia wadau /makundi mengi katika sekta nyingi wakiwa na lengo ya kukuza mwingiliano kati ya agenda ya wanawake, wasichana na watoto katika sekta nyingine ili kuimarisha mikakati ya ujenzi wa harakati za wanawake katika sekta zote na hivyo kukuza nguvu za pamoja/tapo katika maeneo mbalimbali.

Katika muundo huu, tunakubali mapendekezo ya miradi ambayo yanalenga kuanzishwa au kuongeza kasi ya hatua ambazo zinakuza vitendo vya pamoja vya utetezi, majukwaa jumuishi, Mitandao ya kukuza ujuzi wa uandishi, mitandao na kujifunza katika sekta mbali mbali za wanawake, wasichana na watoto nchini.

**VIGEZO VIKUU ViNAVYOANGALIWA KATIKA UTOAJI WA RUZUKU**

Waombaji wanapaswa kujitahidi kuzingatia vigezo vifuatavyo wakati wa kuandaa andiko la mradi

**1. KUOANA KWA MALENGO YA MRADI NA MAHITAJI MAKUU YA KIJINSIA KATIKA JAMII**

- Andiko ambalo linaonyesha jinsi malengo yatakavyokidhi matamanio ya wadau katika kuchangia juhudi za kuleta usawa wa kijinsia na ukombozi wa fikra katika maeneo yaliyoainishwa kutekelezwa na mradi

**2. UWEZO WA MTANDAO, SHIRIKA/KIKUNDI & UFAHAMU WA TATIZO LA MSINGI LA KUTATULIWA NA MRADI**

- Andiko la Mradi lenye kuhakikisha kwamba kuna uchambuzi wa kina kuhusu uwiano kati ya tatizo la kutatuliwa na mikakati iliyowekwa na matokeo tarajiwa yanayopimika.
- Andiko la Mradi linalo onyeshe uwezo madhubuti wa Mtandao, Taasisi, Shirika, au Kikundi husika kwenye kutekeleza mradi pendekezwa.
- Andiko la mradi linalo akisi ushiriki mpana wa wadau katika kuibua, kutekeleza na hasa ikuhusisha wale walioathirika kwa kiasi kikubwa na tatizo linalotakiwa kutatuliwa.
- Andiko la mradi linalo akisi juhudi kuelekea ujenzi wa ushirikiano na nguvu za pamoja kati ya mashirika ya haki za wanawake katika ngazi mbali mbali kwa lengo la kuunda/kuimarisha utendaji wa Mitandao na Majukwaa kwa ajili ya ukuzaji wa haki za wanawake na wasichana ili kuwaongezea uwezo wao katika Nyanja mbali mbali.
- Andiko la mradi linalo onyesha uwezo na muendelezo wa kuibua na kutunza mafanikio (na mafunzo) ambayo yanaweza kuigwa na kutumika katika mradi mingine katika ngazi mbalimbali.
- Andiko la mradi linalo onyesha ubunifu wa mikakati ya kiutekelezaji na matokeo yake.

**WAOMBAJI WA RUZUKU WAFUATE HATUA ZIFUATAZO:**

I. Kuwasilisha Andiko Fupi la Mradi (lisilozidi kurasa 5-7) likielezea mradi pendekezwa utakaotelezwa
II. Andiko la mradi liwe na viambatanisho vifuatavyo
- Nakala ya Cheti cha Usajili
- Nakala ya Katiba ya Shirika/Kikundi
III. Tumia Fomu ya Muongozo wa Maombi ya Ruzuku inayopatikana katika tovuti ya WFT: www.wft.or.tz. Fomu hiyo pia inapatikana katika ofisi za WFT kipindi chote cha muda wa kazi.

Mwisho wa Kupokea Maombi ni tarehe **29 Februari 2020**

- Email, grants@wft.or.tz
- S.L.P 79235, Dar es salaam
- Ofisi za WFT Nyumba namba 659 mtaa wa Mikoroshini (Msasani) Dar es Salaam.
- Simu 0753 912 130

* TAFADHALI FAHAMU KUWA WATAKAO JULISHWA KUHUSU MAOMBI YA RUZUKU NI WALE TU AMBAO MAANDIKO YAO YA MRADI YATAPITISHWA. KAMA HUJAJULISHWA KUHUSU KUPITISHWA KWA ANDIKO LAKO IFIKAPO TAREHE 20 MACHI 2020, BASI ANDIKO HILO HALIKUCHAGULIWA NA UTAENDELEA KUSHIRIKIANA NA WOMEN FUND TANZANIA -TRUST KWA NJIA NYINGINE MBALIMBALI

215632102

# THBUB, Ireland kuelimisha umma haki za binadamu

Na Mbaraka Kambona

IRELAND imeonesha nia ya kushirikiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) katika kutoa elimu ya kukuza uelewa wa wananchi kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini.

Hayo yalibainishwa na Balozi wa nchi hiyo nchini, Paul Sherlock Sherlock, alionesha utayari huo wa kushirikiana na THBUB wakati wa mazungumzo yake na ujumbe wa tume, ulioongozwa na Mwenyekiti wake, Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu, ulipomtembelea katika ofisi zake jijini Dar es Salaam, juzi.

Akijibu ombi la Mwenyekiti wa tume ambaye alimuomba kuangalia uwezekano wa kushirikiana katika kuelimisha wananchi wa Tanzania kuhusu haki ya ardhi, Balozi alisema kuwa hilo ni jambo zuri na wataangalia uwezekano huo.

Kwa mujibu wa Jaji Mwaimu, maeneo mengi nchini kuna migogoro ya ardhi, huku akitaja baadhi ya maeneo kama ya Kilosa na Kilombero kama mfano wa maeneo yenye migogoro, na kusema kuwa wanawake ndio wahanga wakubwa linapokuja suala la umiliki wa ardhi.

"Nafikiri hilo litakuwa jambo zuri, tutakaa tuone namna bora tunaweza kushirikiana katika kazi hiyo ambayo ipo katika mamlaka yenu, tutajadiliana na kuona wapi tunaweza kushirikiana," alisema Balozi Sherlock

Kamishna wa Tume, Nyanda Shuli, alisema kuwa kwa sasa THBUB inapokea malalamiko mengi yanayohusu mafao, watu kuachishwa kazi bila kuzingatia taratibu, upatikanaji wa haki kwa wakati na malalamiko kuhusu migogoro ya ardhi.

Nyanda alisema kufuatia hali hiyo, THBUB inajipanga kujikita katika kuandaa mbinu zitakazosaidia kutoa majawabu ya matatizo hayo.

" Katika utatuzi wa migogoro tume tunahimiza kukaa katika mazungumzo ili kupata ufumbuzi, sisi tunaamini katika kuleta watu pamoja na kuzungumza kuhusu matatizo yao na kuyapatia ufumbuzi," alisema Shuli.

Kaimu katibu Mtendaji wa THBUB, Hajjat Fatuma Muya, alieleza kuwa tume imekuwa ikifanya kwa karibu na taasisi mbalimbali za ndani na za kimataifa likiwamo Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

Aidha, Muya alisema tume imeingia mkataba wa ushirikiano na AZAKI 21 nchini kwa lengo la kuunganisha nguvu ili kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa, zinakuzwa na kuheshimiwa.

Aliendelea kueleza kuwa kupitia ushirikiano huo, hivi karibuni THBUB kwa kushirikiana na taasisi ya Haki Maendelea walitoa mafunzo ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa Madiwani 27 wa Halmashauri ya Mkoa wa Lindi.

Ziara ya THBUB katika ubalozi wa Ireland ililenga katika kujenga mahusiano na kutafuta ushirikiano wa kikazi kwa muelekeo wa kuhakikisha kuwa haki za binadamu na misingi ya utawala bora inatunzwa na kuheshimiwa nchini.




Viongozi wa Shule ya Msingi Pwani, Tegeta, jijini Dar es Salaam na viongozi wa mashirika ya Time To Help, Embless Relief na Pionners Academy ya Marekani, wakisoma vitabu kwenye maktaba ya shule hiyo, iliyokarabatiwa na mashirika hayo, shuleni hapo, juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wanaotumia corona kujitafutia kiki ya kisiasa waonywa

INATOKA UK. 3

waliokuwa wakisubiri kupata majibu ya vipimo wanaotoka maeneo ya China Bara.

Aidha, ilisema huko visiwani Hong Kong, Macao na Taiwan, watu 50 walithibitishwa kupata ugonjwa huo wakati 10 waliripotiwa Macao na Taiwan walikuwa 18, hapo Februari 12.

Iliongeza kuwa wiki hii Februari 12, Kamati ya Kudumu ya Ofisi ya Siasa ya Kamati Kuu ya CPC ilikutana kwa mara ya tatu kujadili hali ya kuzuia na kudhibiti homa ya corona -COVID-19. Ikiongozwa na Katibu Mkuu wa Kamati Kuu ya CPC na Rais Xi Jinping.

Ilisema mkutano huo ulitaka kutatua fumbo la kudhibiti janga kwa kuinua viwango vya kulaza wagonjwa hospitali na viwango vya tiba na kupunguza maambukizi na viwango vya vifo.

Taarifa ilisema aidha, ilitoa wito wa juhudi za kuboresha matibabu kwa wagonjwa, hasa walio katika hali mbaya, kwa kutumia rasilimali bora zaidi za kitabibu na kiteknolojia, kufanya mapitio ya wakati mwafaka ya suluhiho la utambuzi na matibabu na kuongeza maendeleo ya dawa na chanjo.

Rais Xi Jinping, aliagiza wafanyakazi wa matibabu zaidi ya 2,600 kusaidia vita dhidi ya mlipuko wa COVID-19 huko Wuhan na ujumbe wa matibabu wa PLA unashughulikia hospitali mbili katika mji huo na utafanya kazi chini ya Hospitali ya Huoshenshan, ambayo ni ya kwanza ya muda iliyoanzishwa mapema Februari wakati wa janga hilo.

Ilisema kufikia Februari 13, Jeshi la Ukombozi la Watu wa China -PLA limepeleka vikundi vitatu vya wafanyakazi zaidi ya 4,000 wa matibabu Wuhan tangu kuzuka kwa janga hilo.

## Bei ya samaki yapaa

INATOKA UK. 2

sababu ni vigumu kupata samaki au dagaa kwa wingi unaotakiwa.

Alisema vyombo vinavyokwenda kuvua ni vichache na hutumia aina nyingine ya mitego kama mishipi.

"Hali hii imeathiri pia wafanyabiashara hususani wanawake ambao kwa wingi hufika sokoni hapa kila siku kununua dagaa na samaki ili kwenda kuwauza mtaani, kutokana na changamoto hii bei imekuwa juu zaidi na kufanya washindwe kuimudu," alisema.

Alisema inapokuwa hali ya hewa ya kawaida, uvunaji wa dagaa kwa siku sokoni hapo huwa ni tani 48 hadi tani 50, lakini kwa sasa ni kidogo sana.

Kwa upande wa samaki, alisema wengi kwa sasa wanatoka Kilwa na Mafia ambao huletwa wakiwa wamehifadhiwa kwenye mabarafu.

"Ingawa na wao ni wachache kwa sababu hata huko hali ya upepo ni kama huku, upatikanaji ni tatizo bado hadi sasa bado hatuna samaki wa kutosha na bei zake nazo zipo juu," alisema.

Moyo alisema kwa mfano kwa sasa samaki aina ya changu anauzwa kati ya Sh. 12,000 hadi 13,000 wakati awali bei ilikuwa ni Sh. 8,500 hadi 9,000.

Pia alisema kwa upande wa samaki aina ya tasi kwa sasa anauzwa kati ya Sh. 8,000 hadi 9,000 wakati awali alikuwa ni Sh. 6,000.

## Kortini tuhuma kumtumia Waziri Mkuu kutakatisha

INATOKA UK. 4

Guanhui Su Biaolin Tang kilichoonyesha kuwa ni cheti halali kutoka kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, huku wakijua si kweli.

Wankyo alidai kuwa katika shtaka la tano, washtakiwa wanakabiliwa na shtaka la kuwasilisha nyaraka za uongo ambapo mnamo Januari 14 mwaka huu, waliwasilisha cheti cha utambuzi wa msaada kilichoonesha kuwa ni halali kutoka kwa Waziri Mkuu huku wakijua kuwa si kweli.

Katika shtaka la sita, washtakiwa hao wanadaiwa kujipatia fedha zaidi ya Sh. milioni 22.9 kutoka kwa Guanhui Su Tang kwa njia ya udanganyifu wakijidai kuwa ni msaada wanaopeleka kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Shtaka la saba linalowakabili washtakiwa hao ni utakatishaji pesa ambapo inadaiwa kuwa mnamo Januari 14 mwaka huu, washtakiwa walijipatia zaidi ya Sh. milioni 22.9 kwa njia ya udanganyifu huku wakijua ni zao la makosa tangulizi.

Washtakiwa hao hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi mpaka upelelezi utakapokamilika na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) atakapotoa kibali.

Hakimu Isaya alisema kesi hiyo itatajwa Februari 28 mwaka huu na washtakiwa warudishwe mahabusu.



Naibu Waziri Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndungulile akiongea na wananchi wa Kijiji cha Momela, wilayani Arumeru, mkoani Arusha, jana wakati alipotembelea Kituo cha Afya cha Afrika Naamini Alama, kilichokuwa kimefugwa kutokana na mgogoro uliokuwepo kati yake na Halmashauri ya Meru. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Asakwa tuhuma kubaka mtoto miaka 10

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

UONGOZI wa Kijiji cha Mwikanzi Kata ya Mamire, mkoani Manyara, unamsaka mwimbaji wa kwaya na mpiga kinanda wa kanisa moja eneo la Kansi Mtaa wa Mamire, Elibariki Naeli, kwa tuhuma za kumbaka mtoto wa miaka 10, ambaye ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Sora.

Akizungumza jana na Nipashe katika Kijiji cha Mwikanzi, Mwenyekiti wa kitongoji, Jeremiah Bura, alisema tukio hilo lilitokea Februari 4, mwaka huu majira ya jioni kijijini hapo.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo alianza msako kumtafuta mtuhunuwa, lakini hawajafanikiwa kumpata.

"Tukio lilipotokea na kupata taarifa nilikusanya vijana na kuanza kumtafuta mtuhumiwa bila mafanikio, lakini tunaendelea na msako," alisema.

Mama mzazi wa mtoto huyo (jina tunalo), alisema siku ya tukio mwanawe alikuwa anatoka kwa bibi yake alikomtuma kupeleka mboga na akiwa njiani kurudi nyumbani, alikutana na mtuhumiwa akamkamata kwa nguvu na kumuingiza kichakani kisha kumfanyia unyama huo.

Alisema kijana aliyefanya unyama huo ni jirani yao na alimtisha mtoto huyo asipige kelele na kumtishia kuwa kama atapiga kelele atamuua.

"Alipotimiza haja yake alimtelekeza kichakani mwanangu na kumpa sharti la kutokupiga kelele, ndipo mtoto alijikokota na kurudi nyumbani," alisema.

Alisema baada ya kufika nyumbani alimweleza unyama aliofanyiwa na ilibidi amkimbize Zahanati ya Mwikanzi, na kuwa alipomfikisha daktari alimpima na kuthibitisha kuwa alibakwa na alikuwa na maumivu makali.

Akisimulia kwa masikitiko mtoto huyo alisema alikutana na kijana huyo akiwa na dada mmoja ila alipomuona ghafla alimuaga dada huyo na kumkimbilia.

"Alipofika alinishika mkono na kunilazimisha kwa nguvu na kunibeba begani, nilimuuliza nimekukosea nini akaniambia atanichinja ninyamaze, kisha akaniziba mdomo nisitoe sauti," alisema huku akilia..

Rehema Handa, ni jirani ambaye alibaini unyama huo, baada ya kumuona mtoto amelowa damu, huku akitembea kwa shida, ambapo alishirikiana na mama yake kutoa taarifa kwa mwenyekiti wa kitongoji.

Daktari aliyemfanyia uchunguzi mtoto huyo, ambaye hakuwa tayari kutajwa jina lake gazetini, alisema walimpokea mtoto huyo na kumfanyia vipimo na kubaini mtoto huyo wa darasa la tatu kufanyiwa unyama huo.

# Kamati ya ujenzi yaikuna Takukuru

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) wilayani Simanjiro mkoani Manyara, imeipongeza kamati ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani iliyosimamia ujenzi wa madarasa sita na ofisi mbili za shule mbili za sekondari kwa kuzingatia viwango bora.

Ofisa wa Takukuru wa Wilaya ya Simanjiro, Godfrey Roman, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wenyeviti wa mitaa wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani.

Roman alisema timu ya Takukuru wilayani Simanjiro ipo Mji Mdogo wa Mirerani kuchunguza ujenzi wa madarasa ya shule mbili za sekondari ila wakaridhishwa na ujenzi wa vyumba vya madarasa na ofisi ulivyofanyika.

"Niwapongeze wajumbe wa kamati kwa usimamizi mzuri wa madarasa matatu na ofisi ya shule za sekondari Mirerani B.W. Mkapa na Tanzanite kwani kwenye ujenzi tumebaini hakuna tatizo lolote," alisema Roman.

Hata hivyo, alisema kazi iliyobaki hivi sasa ni kuchunguza namna mchakato wa ukusanyaji fedha na matumizi yalivyofanyika na upatikanaji wa zabuni ya ujenzi wa madarasa hayo na ofisi hizo. "Tutachunguza vitabu vyote vya makusanyo ya fedha hizo zote na tunaomba ushirikiano wenu kwani sisi tupo hapa Mirerani hadi Ijumaa

ijayo tukichunguza hilo," alisema Roman.

Aliwatoa hofu wajumbe wa mamlaka hiyo kuwa kazi yao ni kuzuia na kupambana na rushwa na siyo kukamata watu pekee ila wanafikia hatua hiyo ya kukamata endapo kukiwa na tatizo la rushwa.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Adam Kobelo, alishukuru ushirikiano alioupata kwenye kamati ya ujenzi wa madarasa na ofisi za

Kobelo alisema hadi mwishoni mwa Januari Sh. milioni 22.3 zilikuwa zimetumika kwenye ujenzi huo katika shule ya sekondari Tanzanite na Sh. milioni 36.8 kwa shule ya sekondari Mirerani B.W. Mkapa.

Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji huo, Evence Mbogo, alisema nyaraka zote za ukusanyaji wa fedha za ujenzi huo wa shule za sekondari zipo na zinaweza kukaguliwa kwa wakati wowote ule.

# Wakuu wa shule wapigwa 'stop' michango

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, amewaagiza wakuu a shule za jiji hilo kutochangisha mchango wa aina yoyote kinyume cha taratibu na atakayekiuka hilo, atachukuliwa hatua kali.

Akizungumza jana kwa niaba ya Mkurugenzi wa jiji hilo, Ofisa Elimu wa Sekondari Jiji la Arusha,Valentine Makuka, wakati akikanusha taarifa iliyosambazwa na baadhi ya wananchi kuwa Shule ya Sekondari Lemara inachangisha wazazi michango, wakati serikali imekataza, Makuka alisema taarifa hizo siyo sahihi.

Alisema Halmashauri ya Jiji inazingatia na kufuata maagizo na nyaraka toka serikalini juu ya sera ya elimu bila malipo iliyotangazwa na serikali.

"Kutokana na maagizo haya Halmashauri yetu imekuwa ikiwakumbusha wakuu wa shule mara kwa mara kuzingatia maagizo haya, pia tunawakumbusha wananchi endapo watachangishwa watoe taarifa kwa Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya,"alisema.

Alisema hawawezi kuchangisha wazazi wakati serikali inatoa fedha za uendeshaji zikiwamo manunuzi ya viandikio na karatasi kila mwezi.

Aidha alisema endapo kuna mwananchi anakumbana na changamoto yoyote ya kuombwa chochote vema akatoa taarifa ngazi husika, ili hatua za haraka zichukuliwe kwa wahusika.

Pia alisema katika kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika shule zao, serikali imegawa vitabu vya kiada kwa shule za jiji tangu shule zifunguliwe na vifaa vya sayansi.

"Lakini serikali imeendelea kutuma fedha za uendeshaji Sh. milioni 134 kila mwezi katika shule zote za Jiji za msingi na sekondari ili kununua vifaa vya kufundishia,"alisema.

Makuka alisema kutokana na fedha hizo wanazopata, ufaulu kwenye shule za sekondari umekuwa ukipanda mwaka hadi mwaka, ambapo matokeo ya kidato cha pili ya mtihani uliofanyika mwaka 2019 Jiji ilishika nafasi ya kumi kati ya halmashauri 186. Kwa kidato cha nne walishika nafasi ya 43 kutoka nafasi ya 75 waliyoshika mwaka 2018.







Mratibu wa mradi wa Paza Sauti, Tokomeza Ukatili kutoka Shirika la kiraia la Tusonge, Consolatha Kinabo (kulia), akizungumza na wananchi wa Kata ya Arusha Chini, Moshi Vijijini, juzi, kuhusu ukatili unavyoweza kuathiri ustawi wa jamii hasa maeneo ya vijijini. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Walipwa fidi kupisha mradi umeme jua

**Na Godfrey Mushi,** SAME

WANANCHI wa vijiji vya Kisima na Kandoto katika Wilaya ya Same, wameanza kulipwa fidia ya mali na mazao ili kupisha ujenzi wa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa jua.

Taarifa iliyopatikana jana na kuthibitishwa na Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) mkoani Kilimanjaro, Mhandisi Mahawa Makaka, ineleza kuwa wananchi hao wanalazimika kuondoka sasa katika eneo lenye ukubwa wa ekari 100 ambalo tayari limesanifiwa kupisha ujenzi huo.

Serikali imeanza kulipa fidia hiyo, ikiwa imepita miaka minne tangu ilipofanyika tathimini na uthaminishaji wa mali.

“Tumetenga kiasi cha Sh. bilioni 3.5 kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi hawa wa Kisima na Kandoto. Katika awamu ya kwanza tutalipa Sh. bilioni 1.99 kwa wananchi 203,” alisema Mhandisi Mkaka.

Baadhi ya wananchi wa vijiji hivyo, wakizungumza baada ya maofisa wa Tanesco kufika katika mkazi yao waliishukuru Wizara ya Nishati kwa kuharakisha malipo hayo ya fidia na kuonyesha dhamira ya kuanzisha mradi wa umeme jua utakaozalisha megawati 150 ambazo zitaingizwa katika gridi ya taifa.

Fidia hiyo inalipwa kwa wakati mwafaka, kipindi ambacho serikali imenuia kuzalisha umeme wa kutosha kwa kutumia gesi asilia ili kukabiliana na upungufu unaojitokeza nchini.

Kwa mujibu wa Mhandisi Mkaka, mitambo mipya na ya kisasa itafungwa wakati wowote kuanzia sasa katika Wilaya ya Same.

Tanesco inafikia hatua hiyo, baada ya uzalishaji wa nishati ya umeme ukiwa unabadilika kadri teknolojia zinavyobuniwa na kukua, pamoja na kwamba Tanzania kwa miaka yote imekuwa ikitegemeza zaidi teknolojia kongwe ya umeme wa maji.

Mitambo ya umeme wa maji kwa kawaida huzalisha asilimia 35 ya mahitaji yote ya umeme Tanzania, huku gesi asilia na mafuta hujazia asilimia zinazobaki.

# Wadau washauriwa tuzo ya elimu kwa wasichana

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

KIONGOZI mmoja wa serikali katika Wilaya ya Moshi, ameshauri serikali na wadau wa elimu nchini kufikiria kuja na utaratibu wa kuwapa tuzo wasichana wa Tanzania watakaomaliza chuo kikuu na kukutwa hawajaharibiwa usichana wao.

Ofisa Tarafa ya Moshi Magharibi, Senzia Lushino, alisema ni vyema wasichana watakaomaliza elimu ya juu na kubainika hawajaondolewa bikira au kufanyia vitendo vya ukatili wa kijinsia kama ukeketaji wakapewa tuzo au nafasi za utumishi wa umma.

Alisema iko haja ya kuiga utaratibu huo unaotumiwa na nchi rafiki ya China, ambako wasichana wanaomaliza Chuo Kikuu wakipimwa na kukutwa bado ni bikra wanapewa kipaumbele kwa kuajiriwa katika nafasi kubwa za kazi serikalini.

Alisema utaratibu huo utasaidia kuwapa chachu wasichana wengi nchini kuepuka kujihusisha na mapenzi katika umri mdogo na hasa wakati wa masomo yao. “Kule China wenzetu wamepiga hatua kubwa katika kuzuia mapenzi katika umri mdogo, sasa kama sisi tunataka kudhibiti vitendo hivi hasa kwa wanafunzi wa kike kupata ujauzito wakiwa shule na katika umri mdogo kuna kila sababu ya kuja na utaratibu huo,”alisema Lushino

Wakati Ofisa huyo anataka kutumika utaratibu wa China, kuna taarifa za kitafiti zinaeleza kuwa wasichana wanaoanza kushiriki ngono katika umri mdogo wapo katika hatari kubwa ya kupata saratani ya shingo ya kizazi kuliko wenye umri mkubwa.

Utafiti wa kitaalamu unasisitiza kwamba hiyo ni kwa sababu kirusi cha HPV (Human Pappiloma Virus) ambacho husababisha ugonjwa huo huchukua miaka 20 kuanza kuonyesha athari kinapoingia kwenye mwili wa mwanamke.

# Tarura yakiri changamoto Moshi, Vunjo

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, imekiri kuwa bado kuna uhitaji wa matengenezo makubwa ya barabara za majimbo ya Moshi Vijijini na Vunjo ambayo yanaunda halmashauri hiyo, ikilinganishwa na kiasi cha fedha kinachopatikana.

Kwa mujibu wa Kaimu Meneja wa Tarura, Wilaya ya Moshi, Loishiye Mollel, halmashauri hiyo imetengewa Sh. bilioni 1.3 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zake.

Alisema Wilaya ya Moshi, ina mtandao wa barabara wa zaidi ya kilomita 700 na kwamba hivi sasa baadhi ya barabara zinazotarajiwa kutengenezwa kwa kiwango cha changarawe ni barabara ya Wami/Gomberi inayotarajiwa kutengenezwa kilomita nne na barabara ya Sangiti-Nganyeni inayofanyiwa matengenezo ya kawaida kwa umbali wa kilomita tatu.

“Tunategemea kuwa changamoto zote zilizotajwa na wananchi na kupigiwa kelele Madiwani zitafanyiwa kazi kwa maeneo yote yaliyotengewa bajeti ndani ya mwaka huu wa fedha,” alisema.

Maeneo mengine ambayo bado kuna changamoto na hayamo kwenye bajeti, tutaendelea kushauriana ili kuhakikisha shughuli za kimaendeleo zinaendelea wakati tukiendelea kutafuta fedha nyingine kwa ajili ya matengenezo yake,”alisema Mollel

Barabara nyingine inayojengwa kwa kiwango cha lami ni ya Getifonga/ Mabogini/ Kahe/ Chekereni ambayo ni utekelezaji wa ahadi ya Rais John Magufuli ya mwaka 2015. Barabara hiyo tayari imetengewa kiasi cha Sh.bilioni 22.

Kwa mujibu wa Tarura, sehemu ya utekelezwaji wa ahadi hiyo ya Rais Magufuli, ilipangwa kuanza katika bajeti ya mpya ya mwaka wa fedha ulioanza Julai mosi mwaka huu.

Aidha, alisema kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Tarura itatumia zaidi ya Sh. bilioni 1.1 katika ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 674.52 ikiwemo ahadi ya Rais John Magufuli ya ujenzi wa barabara yenye urefu kilomita 20. Kabla ya kutolewa taarifa hiyo inayoleta faraja zaidi kwa wananchi wa maeneo hayo, Diwani wa Kata ya Mabogini, Emanuel Mnzava, ilieleza kuwa katika sekta ya ujenzi ndani ya kata yake, ahadi ya Rais (Magufuli) ya kuijenga barabara hiyo bado haijatekelezwa.

Katika taarifa yake, Mnzava alitoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, zaidi akiiomba ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na Tarura kusaidia kufuatilia ahadi hiyo.





## Huduma dharura sasa zaimarishwa Benjamin Mkapa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH), imeanzisha Kitengo cha matibabu ya magonjwa ya dharura na majeruhi kanda ya kati ambapo hadi sasa kimeshahudumia zaidi ya wagonjwa 3,000.

Akizungumza jana katika uzinduzi wa kitengo hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, alisema kwa kanda hiyo kitengo hicho pekee kipo kwenye hospitali hiyo na kimeshahudumia zaidi ya wagonjwa 3,000.

Dk. Chandika alimuomba Naibu Balozi wa Israeli Eyal David kuendelea kutoa msaada wa mafunzo mbalimbali kwa watumishi wa hospitali hiyo ili kuwajengea uwezo zaidi kwenye maeneo mengine ya kibingwa.

Alitaja huduma zinatarajiwa kuanzishwa kuwa ni huduma za matibabu ya moyo, matibabu ya saratani na upandikizaji wa viungo.

Akizindua kitengo hicho, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk.Binilith Mahenge, alisema kitengo hicho ni mkombozi kwa wanachi wa Kanda ya kati hasa kutokana na ujio wa Serikali Dodoma ambao umechagiza ongezeko na muingiliano wa watu jambo linaloweza kuongeza matukio ya ajali na magonjwa ya dharura.

"Kitengo hiki ni mkombozi kwa wananchi wa kanda hii hasa ukizingatia kuwa ujio wa Serikali hapa Dodoma umechagiza ongezeko na muingiliano wa watu jambo linaloweza kuongeza matukio ya ajali na magonjwa ya dharura jijini na maeneo yanayozunguka jiji la Dodoma," alisema.

Alibainisha Hospitali hiyo pamoja na huduma zingine za afya ilianzishwa ili kutoa huduma za kibingwa, hivyo Serikali inategemea kuona kitengo hicho kikitoa huduma za kibingwa kwa magonjwa ya dharura na majeruhi.

Aidha, Dk. Mahenge alisema, Serikali iliingia makubaliano na Shirika la misaada la Israel kwa ajili ya kuboresha huduma za afya zinazotolewa BMH hususan wagonjwa wa dharula na majeruhi.

Alisema Shirika hilo limekubali kutoa msaada wa vifaa vya kutoa huduma za dharula na kwa majeruhi na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya wa Hospitali hiyo kuhusu utoaji wa huduma hizo.

Naye, Mkurugenzi wa Kinga wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, alimuomba Naibu balozi huyo pamoja na madaktari alioambatana nao kuendelea kuisaidia hospitali hiyo pale watakapohitaji msaada toka kwao.

# Huduma wezeshi kwa wakulima mbioni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imesema inaangalia namna ya kuwapo na huduma wezeshi kwa wakulima kutambua aina ya udongo na mbolea inayopaswa kutumika shambani.

Hayo yalibainishwa na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hussein Bashe, alipokuwa akizungumza katika Kongamano la Sita la Jukwaa la wadau wa sera za kilimo, mifugo na uvuvi, jijini hapa.

Alisema tatizo ambalo wizara hiyo inakabiliana nayo ni namna ya kufanya utaratibu huo kama huduma kwa mkulima ambayo ataweza kumudu.

"Kwa mfano, ukichukua sampuli moja ukaenda kwenye kituo cha utafiti unapaswa kulipa kiasi cha Sh.100,000 kwa mkulima mwenye hekari 5-10 anataka kuchukua sampuli zaidi ya moja atapaswa kutumia kiasi gani?" alihoji. Alisema suala hilo linajadiliwa ndani namna ya kufanya utaratibu huo kama huduma kwa sekta ya kilimo.

Akizungumzia kuhusu nzige, Bashe alisema Tanzania bado haijashambuliwa na nzige na hakuna eneo lolote lililoshambuliwa.

"Tumejipanga kwa vifaa na dawa, tunawaomba nyie kama wadau muanze kujadili namna ya kushirikiana kupambana na suala hili," alisema.

Aliwaomba kutumia washirika wenzao kwenye nchi zilizokumbwa na nzige ili kujua namna walivyofanikiwa kupambana nao.

"Hatua hii itasaidia serikali kupata taarifa ili kujipanga vyema na kujua namna ya kukabiliana nao ili wasilete madhara," alisema.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utafiti kuhusu zao la kahawa, Mkurugenzi wa Jukwaa la wadau wa kilimo wasio wa kiserikali(ANSAF), Audax Rukonge, alisema lazima kutangaza uwekezaji kwenye zao hilo ili kuleta ushindani na kuondoa kero zinazowakabili wakulima.

"Pia badala ya msimu wa kahawa kufunguliwa na kufungwa, iuze mwaka mzima ili wakulima waamue ni lini wauze kahawa zao,"alishauri.

Nao, baadhi ya wadau wakichangia kwenye kongamano hilo, walitaka kuwapo na mnyororo wa thamani kwenye zao la alizeti ili kuongeza uzalishaji nchini wa mafuta.



Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde (wa pili kulia), akifurahia jambo na kinamama wajasiriamali wanaojishughulisha na uuzaji wa mboga, kwenye Soko Kuu la Majengo, jijini Dodoma juzi, baada ya kuwatembelea na kuzungumza nao. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Halmashauri 20 zategwa fedha mipango miji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, amesema Halmashauri 20 zinasuasua katika utekelezaji wa mpango wa upangaji mji licha ya serikali kutoa fedha.

Kufuatia hali hiyo, Mabula amemuomba Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuzichukulia hatua halmashauri zilizotumia fedha hizo kinyume na masharti waliyopewa.

Mabula alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akizungumza kwenye uzinduzi wa Mpango Kabambe wa jiji la Dodoma.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha miji yote inapangwa vizuri na inakuwa salama kwa makazi ya watu lakini mpango umesuasua kwa halmashauri kutokana na kutokuwa waaminifu.

"Serikali ilitoa fedha zaidi ya Sh.Bilioni 6.2 ya kupanga kwenye halmashauri zetu ambao uliwezesha 24, mpango unasuasua kutokana na halmashauri nyingi kutokuwa waaminifu, tumepeleka fedha kwa Halmashauri 24 lakini ni nne tu ndio zimetekeleza," alisema.

Mabula alitaja Halmashauri zilizotekeleza kuwa ni Mbeya, Ilemela, Kahama na Bariadi huku zingine zikichukua fedha bila kufanya kazi hiyo.

"Miji mingine imechukua fedha na haijarejesha, katika hili tunaongeza kasi kwenye ufuatilia, nakuomba Waziri Mkuu, kuchukua hatua kwa halmashauri ambazo zimechukua fedha na kutumia fedha kwa kutozingatia masharti waliyopewa wanasababisha kusuasua kupanga miji yetu," alisema.

Mabula alisema kupitia mpango huo miradi mbalimbali imeanza kutekelezwa ikiwemo upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi ambapo viwanja 132,000 vimepimwa na zaidi ya laki mbili bado hajivapimwa katika jiji hilo. "Tuna Imani kasi itakuwa nzuri soko, stendi zimejengwa, tunaamini utekelezaji utaendelea kwa matakwa ya mpango ulivyo," alisema.

Aidha, alisema kudorora kwa uchumi katika miaka ya 1980 na kubadilika kwa dhana ya upangaji uandaaji wa mpango kabambe katika miji mbalimbali ilififia. "Dhana iliyopendekezwa ni upangaji wa miti kimazingira kwa kuangalia mazingira yake lakini pia kutayarisha mipango kabambe endelevu, kufifia kwa kasi kunatokana na kudorora kwa wataalam wetu katika uandaaji wa mipango kabambe,"alisema.


Alisema serikali haikukaa kimya, ilichukua hatua mbalimbali ya kufanya miji iwe mizuri ikiwa ni pamoja na kuwa na sera ya maendeleo ya makazi ya mwaka 2000, na kupitisha sera ya mipango miji

Awali, Katibu wa Kikosi Kazi cha Taifa cha kuratibu Mpango wa serikali kuhamia Dodoma, Meshack Bandawe, alisema ujenzi wa mji wa serikali kwa awamu ya kwanza umefanyika.

Alisema mpango kabambe umekamilika na mchoro wa awamu ya pili pia umekamilika huku akisema kiasi cha Sh.Bilioni 88 zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya kujenga barabara za lami zenye urefu wa kilometa 40 katika mji wa serikali.

"Nyumba 1,000 zinatarajiwa kujengwa na Shirika la Nyumba ambapo 200 zitajengwa katika mji wa serikali,"alisema.

Bandawe alisema majengo ambayo yalikuwa yakitumiwa Dar es salaam, baadhi yameshatolewa kwa taasisi za serikali na kuokoa Sh.Bilioni 9.9 ambazo zilikuwa zikitumika kulipa kodi ya pango.





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Azzan 'Zungu' (katikati), alipofika Ikulu mjini Zanzibar jana kujitambulisha akiwa na ujumbe wake. Kushoto ni Mkurugenzi wa Muungano, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# China: Watanzania wako salama dhidi ya corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BALOZI mdogo wa China jijini Zanzibar, Xie Xiaowu, amewahakikishia Watanzania kuwa jamaa zao waliopo China wako salama katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya ugonjwa wa mafua ya corona.

Xiaowu alisema hayo wakati alipofanya mazungumzo na Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, katika ofisi za Baraza la Wawakilishi wakati alipokwenda kumpa taarifa ya ugonjwa huo na hali ya usalama kwa Watanzania waliopo China.

Alisema licha ya kupungua kwa kasi ya kuenea kwa ugonjwa huo lakini idadi ya vifo imekuwa ikiongezeka na sasa imefikia watu 1,368.

Alieleza kuwa idadi hiyo ya watu walioambukizwa na ugonjwa huo imefikia 40,000 na juhudi zinaendelea kuchukuliwa na Wizara ya Afya kupambana na ugonjwa huo ambapo jumla ya wagonjwa 59,992 wanapatiwa tiba.

"Wizara ya Afya ya Jamhuri ya Watu wa China inaendelea kuchukua juhudi zote kukabiliana na ugonjwa huo na matumaini yetu kuwa tutafanikiwa kudhibiti maradhi hayo"alisema.

Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi alitoa shukrani za dhati kwa juhudi zinazochukuliwa na serikali hiyo katika kukabiliana na ugonjwa huo ambao umeleta hofu na wasiwasi mkubwa duniani kote.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatoa salamu za pole kwa watu wa China kutokana na maradhi hayo ambayo yamekuwa janga la taifa na dunia kwa ujumla.

Alisema serikali imepata faraja kubwa kuhusu kuwapo kwa taarifa kwamba zaidi ya Watanzania 4,000 waliopo China wapo salama na wameepushwa na tishio la ugonjwa huo.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaungana na ndugu zao wa China katika kipindi hiki kigumu cha ugonjwa wa corona. Matumaini yetu ni kwamba mafanikio yatapatikana na kwa pamoja tutokomeza ugonjwa huu,"alisema Balozi Iddi.

Alieleza kwamba ugonjwa huo umeleta athari kubwa zaidi kwa wajasiriamali ambao waliwekeza na kujikita katika kufanya biashara mbali mbali katika nchi hiyo zinazohusisha kusafiri nje na ndani ya nchi.

# Wawakilishi wahoji kuwapo 'utata' uamuzi kesi ubakaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameelezea udhaifu na kutoridhishwa na hukumu zinazotolewa mahakamani dhidi ya washitakiwa wa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ikiwemo ubakaji na kwamba baadhi yao wamekuwa wakipewa dhamana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Mwantatu Mbaraka Khamis, alisema licha ya juhudi kubwa kuchukuliwa na wizara na taasisi mbali mbali katika kudhibiti matukio ya udhalilishaji wa kijinsia, bado vitendo vya vimekuwa vikiendelea.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akiwasilisha ripoti ya kamati hiyo, ambapo alizitaja baadhi ya kasoro zilizojitokeza ikiwemo Mahakimu na Majaji kutoa dhamana kwa watu wanaotuhumiwa kufanya matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia. "Kamati ya ustawi wa jamii na wanawake bado haijaridhishwa na juhudi zinazochukuliwa katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ambapo bado tatizo lipo kwa upande wa vyombo vinavyosimamia sheria na hukumu,"alisema Mwanatatu.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walisikitishwa na matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na kuzitaka mahakama kuacha kutoa dhamana kwa watu wanaoshitakiwa kubaka.

"Tumesikitika na tukio la hivi karibuni huko Pemba kwa mtu kupewa dhamana kwa kosa la kubaka kwa madai kwamba ni mfanyakazi wa Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) na kwa sasa anashughulikia kazi ya uchumaji wa karafuu"alisema Ali Suleiman Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele.

Mwakilishi huyo alisikitishwa na sheria za kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi zimewekwa pembeni na hazitekelezwi kikamilifu.

Alisema," Tumetunga sheria ya ushahidi pamoja na kukataa kutoa dhamana kwa wabakaji lakini watuhumiwa wa aina hiyo hivi sasa wapo huru wakipewa dhamana.

"Mheshimiwa Spika tunaomba ufafanuzi kwa nini watu wanaotuhumiwa na ubakaji wanapewa dhamana na Mahakama zetu.....wazazi wanasikitishwa sana na watu wanaotuhumiwa na makosa ya ubakaji kupewa dhamana na kuonekana wakitembea mitaani"alisema.

Naye Mwakilishi wa viti maalumu vijana Dhulfa Mmaka, alisema katika kipindi cha miaka miwili matukio ya ubakaji yameripotiwa mengi huko Pemba lakini hakuna mtu aliyetiwa hatiani wala kufikishwa gerezani. "Sijasikia mtu akifungwa kwa makosa ya ubakaji licha ya matukio hayo kuripotiwa kila siku huku watoto wakipewa uja uzito na kuacha shule"alisema.

# Baraza lanusa ufisadi kilimo pilipili kichaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BAADHI ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wameitaka Mamlaka ya Kupambana na Rushwa (ZAECA) kufanya uchunguzi wa ufisadi kwenye mradi wa kilimo cha pilipili kichaa.

Walitaka hatua ichukuliwe kwani mradi huo umetengewa takribani Sh. milioni 500 lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika katika mchanganuo wa fedha hizo na matumizi yake.

Akizungumza katika Baraza la Wawakilishi, Mwakilishi wa jimbo la Uzini Mohamed Raza, alisema serikali malengo yake ni mazuri ya kupambana na tatizo la ajira kwa vijana na kuamua kutenga fedha milioni 500 kwa ajili ya kujiajiri na kazi za ujasiriamali.

Hata hivyo, alisema utekelezaji wa mradi huo umeingia katika utata mkubwa ambapo hadi sasa hakuna hata eka moja ya kilimo cha pilipili iliyovunwa katika mashamba yaliyotengwa ikiwamo Bambi na Pangatupu.

"Jamani Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mnamwangusha sana Rais Shein ambaye lengo lake la kuwawezesha vijana kujiajiri halijatamia.....mradi huu umetengewa fedha nyingi lakini huu ni mwezi wa sita hakuna kilichofanyika"alisema.

Mwakilishi wa jimbo la Bumbwini Mtumwa Peya, aliitaka wizara kabla ya kutekeleza mradi kufanya utafiti wa kina na kujua maeneo yepi ni muafaka kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha pilipili hoho.

Peya alisikitishwa na fedha zilizotengwa kwa vijana katika mradi wa pilipili hoho kuwa ni sawa na zilizopotea kwa sababu hakuna mafanikio ya kilimo hicho ambapo vijana hawakupata mashirikiano kutoka kwa wataalamu.

Alieleza kuwa katika eneo hilo mradi ambao unakubali ni wa kuotesha miwa ambao unatekelezwa na vikundi mbali mbali vya wajasiriamali huku ukipata mafanikio makubwa.

"Wananchi wangu wa Pangatupu kwa muda mrefu wamekuwa wakitekeleza mradi wa kuotesha miwa ambao umeleta mafanikio makubwa na sio huu mradi wa Pilipili hoho"alisema.

Kwa upande wake mwakilishi wa viti maalumu wanawake Vijana Salma Mohamed Mwinjuma aliitaka wizara kukaa pamoja na vijana kuweka mikakati ambayo itawawezesha kuimarisha kilimo hicho kwa mafanikio makubwa.

"Vijana wetu wapo tayari kushiriki kikamilifu katika kilimo cha pilipili hoho ambacho kimeonyesha mafanikio makubwa"alisema.

Awali akizungumza kuhusu sakata la mradi huo, Waziri wa Biashara na Viwanda Balozi Amina Salum Ali, alisema vijana walioteuliwa kushiriki katika mradi huo hawakuonesha mashirikiano wala utayari wa kutekeleza mradi huo.

"Vijana tuliowachaguwa kushiriki katika mradi wa pilipili hoho hawakuonyesha utayari na mashirikiano mazuri ya kufanya kazi hizo na ndiyo maana mradi umeyumba"alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI FEBRUARI 15, 2020



**BURNA BOY UMEMCHUMBIA STEFFLON?** Soma UK.20



PENZI JIPYA

# Dogo Janja, Linah shaka tupu

BASI SAWA

## Isha Mashauzi awatolea shombo wadangaji

STAA wa muziki wa Taarabu, Isha Mashauzi, ameamua kupasuka kwa kuwakemea wanawake wanaosaka pesa kwa kudanga, kuwa kitendo hicho kinawadhalilisha na kuwashushia heshima.

"Maisha yangu yote sijawahi kudanga, hata wigi hili nimevaa kwa hela yangu na hela ya mashabiki, huwa najisikia vibaya nikimkuta mtoto wa kike anauza mwili au anadanga, niwaambie tunajidhalilisha sana, hatuwawekei maisha mazuri watoto wetu" amesema Isha Mashauzi.

Aidha msanii huyo ameongeza kwamba ni lazima wajifunze kuthubutu na kuchukua mfano wake ambao amekuwa mwanamke wa kwanza kuimba Taarab, kumiliki bendi na kumiliki gari kwa pesa yake mwenyewe.



## Matumaini eti ni kweli Ebitoki anapenda kiki

MCHEKESHAJI mkongwe nchini, Matumaini, amesema licha ya kumkubali msanii mwenzake Ebitoke, anachukizwa na tabia yake ya kupenda skendo, kashfa na kiki mbaya.

Akizungumza na kipindi cha Planet Bongo, kinachorushwa na East Africa Radio, Matumaini amesema kama akiachana na vitendo hivyo atakuwa msanii bora hapa nchini.

"Mimi nimekaa Kaole miaka minne bila ya kuchaguliwa kufanya maigizo, siku ambayo naambiwa nikarekodi kipande cha kuigiza na Ray nilitoka kwa mguu kutoka Yombo hadi Kimara Suka, lakini nashangaa wasanii wa sasa nampenda sana Ebitoke kwenye suala la uchekeshaji na anaweza sana ila shida yake ana skendo chafu" amesema Matumaini.





# Lulu acha kutoa majibu ya kizushi

JE, umewahi kumuuliza staa yoyote wa hapa nchini na kukupa jibu la kizushi? Basi hivi karibuni shabiki mmoja wa mwigizaji wa filamu Elizabeth Michael Lulu, amejikuta akijibiwa jibu la kizushi kutokana na swali lake na mtego.

Shabiki huyo aitwaye Veinnah aliweka ujumbe shiriki katika picha ya msanii huyo na kisha kumuuliza kwa nini anafanana na watoto wa Hamisa Mobeto? Lulu Bila kuchelewa akamjibu kizushi eti pengine mimba anazomeba Hamisa zinampenda.

"Hivi Lulu mbona unafanana na watoto wa Hamisa Mobetto hivyo kuliko yeye mwenyewe, yani hapo Daylan mtupu, kuna zingine Fantasy kulikoni dada, kwakweli jiangalie tu kwenye kioo ni wako kabisa" ameuliza shabiki huyo.

Kisha Lulu kuiona comment hiyo amemjibu kwa kuandika "Itakuwa mimba zake zinanipendaga".

INSTA-TWITTER





**Mdogo** wangu huishi vituko jamani. Mimi nilichokiona cha kwanza una meno marefu kama jembe. Haya nangojea hiyo nyimbo sijui itakuwaje, maana hakuna anayekufikia mkali wa singeli Dulla Makabilla- **Shamsa Ford.**



**Piga** kelele mara moja. Piga kelele mara mbili. Piga kelele mara tatu weee... Mtoto wa mjini unakaa nyumba ya familia? Mtoto wa mjini lazima ujue thamani ya kodi weeee... **- Jike**



# Vee Msechu namfahamu aba Levo!

ANAMUZIKI nyota, Peter Msechu, amemfananisha
i yake Baba Levo na shetani kutokana na tabia
e ya kupenda wanamke wengi.
izungumza na EATV & EA Radio Digital, Peter
chu amesema Baba Levo hawezi kupata neema za
gu hadi achague mwanamke mmoja wa kuishi naye,
lia na kufunga naye ndoa.
aba Levo lazima aelewe maisha ni gharama sana
a kufunga ndoa hawezi kama pete ina thamani ya
oni 4 au 5, tabia yake ya kucheza kamari ataiotolea
i, na baraka lazima upewe na Mungu halafu yeye
netani ana wanawake wengi hawezi kutoboa kwa
bu hajui chaguo lake" amesema Peter Msechu
dha Peter Msechu ameendelea kusema "Kila mwan-
e anayekutana naye anazaa naye, mwambieni aend-
kuzaa atachagua kisha kumpata mwanamke mzuri
aye atamvumilia lakini sidhani kama atafanikiwa
endelee kujifunza kupitia sisi wakongwe."



>>> **Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## UNASEMAAA...

## PENZI JIPYA

# Dogo Janja, Linah shaka tupu


SIKU chache baada ya rapa Dogo Janja, kupiga goti na kumvisha pete mchumba wake Linah, mambo mapya yameibuka baada ya watu kuanza kupata hofu kuhusu uhai wa mapenzi ya watu hao.

Mtu ambaye ameonekana kuwa na mashaka ni Madee Seneda, ambaye ametoa ushauri mrembo huyo kuwa macho na wambea kwani ategemee kupata mengi kwa sababu yupo kwenye mahusiano na mtu maarufu.

Dogo Janja alimvalisha pete ya uchumba mpenzi wake huyo Januari 10, mwaka huu kwenye boti wakati wanarudi Dar es Salaam wakitokea visiwani Zanzibar.

"Mpenzi wa Dogo Janja ajue kabisa yupo kwenye mahusiano na mtu maarufu na yeye anaelekea kuwa maarufu muda sio mrefu, kwahiyo asisikilize maneno ya watu na ategemee mengi ambayo yatatikisa mahusiano yao ambayo ni mapya" amesema Madee.

Hata hivyo, Dogo Janja mwenyewe ameonekana kufurahia penzi hilo jipya na kusema amefurahia mapenzi "Msimu wa mapenzi umekuwa mzuri kwetu kwani nimeufurahia sana mimi na mpenzi wangu kule visiwani Zanzibar, nikiwa na familia yangu kama Linah, Recho na Madee".



## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Unaweza** kuajiri mtu kukuendeshea gari yako, ama kukufanyia kazi ya kukutengenezea pesa. Lakini huwezi kukodisha mtu kukubebea ugonjwa wako-**Maimatha Jesse.**



**Mnaochaguliwa** kwenye Kamati za Harusi, sekta ya kupakua chakula. Tafadhali msiwe mnatupakulia kichoyo. Kwani mnataka mrudi navyo majumbani mwenu? Utakuta pale kwenye nyama hasa kuku, anakuwekea tule tupapatio tuduchu. Acheni roho mbaya. Maharusi walitudai sana michango yao-**Roma Mkatoliki.**



**Nnachojaribu** kusema ni kwamba wiki ikiwa haina mechi za EPL huwa nanenepeana kama kitimoto. Ubaya ni nikisikia wiki hii ligi ipo,sijui diet inatokea wapi hata najikuta tu napungua uzito. Hii Man United itaniua mimi siku-**Mwana FA.**

Kuumbe!



## DUDU BAYA

# Chunga na ulimi, ya jandoni hayaanikwi hadharani

HATIMAYE Msanii wa muziki wa kizazi kipya, Godfrey Tumaini, maarufu kama Dududu Baya, ametolewa kifungoni baada ya serikali kuamua kumsamehe.

Dudu Baya alifungiwa na Baraza la Sanaa Tanzania (Basata) baada ya kukataa wito wa kwenda kuhojiwa kuhusu tuhuma alizozitoa katika mitandao ya kijamii kuhusu sanaa.

Baraza hilo limeeleza kuwa Dudubaya alitumia lugha zisizo na maadili.

Hata hivyo, Januari 23, 2020 Dudubaya alijisalimisha Basata na kuomba msamaha lakini baraza hilo halikutoa uamuzi wowote kwa kuwa mamlaka ya kufanya hivyo ipo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Jana Jumanne Februari 11, 2020 msanii huyo alikwenda katika ofisi za Waziri wa wizara hiyo, Dk Harrison Mwakyembe kuweka mambo sawa.

Katika tangazo la katibu mtendaji wa baraza hilo, Godfrey Mngereza amesema Dudubaya amesamehewa baada ya kusikilizwa na Dk Mwakyembe.

Kuondolewa kwa kifungo hicho itakuwa fundisho kwa Dudubaya na wasanii wengine ambao wanaonesha kiburi pale wanapoonekana kwenda kinyume na tasnia ya sanaa.

Hata kama seheria inasema kila mtu ana haki ya kutoa maoni, lakini ni lazima kufuata taratibu zake na si kutumia sanaa kama sehemu ya kusema kile kinachomjia kichwani.

Ni muhimu kujifunza kuwa kila nchi ina taratibu na tamaduni zake, tabia ya kuiga utamaduni wa nje hauna faida na badala yake unawafanya baadhi ya wasanii kuwa na migogoro kati yao na mamlaka husika, jambo ambalo halina tija katika maendeleo yao ya kisanii.

Jambo la kumpongeza Waziri Mwakyembe, ni kuona kwamba Dudubaya ni kijana ambaye anahitaji kuendeleza maisha yake kwa kutumia muziki, kumsamehe ni njia nzuri ya kumwambia ajifunze tena na kujirekebisha kasoro zake.

Wasanii wawe wanasoma nyakati, na kutii mamlaka inayoowaongoza ambayo imewataka kuzingatia sheria kanuni na taratibu, pale wanapofanya kazi zao.

Afande Sele amewahi kusema kwamba kuna baadhi ya wasanii wanafanya mambo ya kihuni kwa nia ya kufungiwa na serikali ili kupata kiki. Lakini kiki za aina hiyo hazikubaliki na badala yake inadhalilisha tasnia.

Kuna usemi kwamba mafundisho ya jandoni hayaanikwi hadharani, hii ina maana kuwa kila mtu mwenye ufahamu ni lazima kuchagua maneno ya kuongea kwani mengine yanaweza kukushusha na kuonekana hauna maana katika jamii.

Ikumbukwe wasanii wana nguvu kubwa, wanapaswa kuishi kwa kufuta maadili kwani watu wengi wanawafuatisha wakiwamo watoto.

# Ngoma 5 kali 'Valentine' 2020



MAUA SAMA

RAYVANNY

**Na Adam Fungamwango**

JANA ilikuwa ni siku ya wapendanao, maarufu kama 'Valentine Day'. Ni siku ambayo vijana wengi wanaipenda kutokana na sababu mbalimbali.

Ni siku ambayo wengi hutumia kukaa, kutembea au kuwapelekea zawadi wapenzi wao au wazazi wao.

Wabongo kama kawaida yao, na kwa sababu asilimia kubwa sikuukuu hii asilia yake ni wazungu, basi wameiga hivyo hivyo, kwani zawadi kubwa tulizoziona ni kadi na maua.

Mwezi wote huu wa Februari huitwa ni mwezi wa mapenzi au mapendeko. Kwenye muziki kuna wasanii wa bongo fleva hawajaiacha hivi hivi kwani wametoka na vitu kwa ajili ya kuwafurahisha mashabiki wao na mashabiki wa muziki huu kwa ujumla.

Zifuatazo ni ngoma mpya za bongo fleva zilizotoka mwezi huu wa Februari kwa ajili ya kuwarusha mashabiki mwezi wa wapendanao, pamoja na wasanii waliotoa ngoma hizo.

**MEJA KUNTA FT LAVALAVA-WANGA**

Inawezekana hata zile tuhuma kuwa jamaa huyu alijisingizia kuwa amefariki baada ya kupata ajali ili apate kiki zinawezekana kuwa na asilimia kubwa ya ukweli, kwani siku chache tu baada ya jambo lile kutokea, ametoa ngoma iitwayo 'Wanga'.

Wengi walidai jamaa alitengeneza kiki na wakahisi kuwa ana ngoma anakaribia kuitoa, na kweli Februari 7 akatoa ngoma hiyo, akimshirikisha Lavalava ambayo tayari imeshaanza kubamba na kuendelea kuteka mijadala kama ilivyokuwa mwanzo. Na kwa kiasi fulani amefanikiwa.

**WALTER CHILAMBO-MOTO**

Unamkumbuka huyu jamaa? Ndiye aliyekuwa mshindi wa shindano la uimbaji mwaka 2012.

Ni msanii ambaye wakati mwingine anaingia kwenye gemu, wakati mwingine haonekani. Wakati mwingine tunasakia ameingia kwenye gospel, mara amerudi tena. Sasa ametoa ngoma yake mpya Februari 7 mwaka huu, akiita 'Moto'.

Naye amekuwa mmoja wa wasanii ambao hawakuuacha mwezi huu wa mapendeko uupite hivi hivi.

**HARMONIZE-HUJANIKOMOA**

Ukiusikia na ukaambiwa kuwa huyu ni Harmonize unaweza kata kubisha. Au ukadhani mtangazaji amekosea. Wimbo huu unaitwa 'Hujanikomoa' ambao msanii huyu amebadilika kabisa na ameupiga katika mahadhi ya singeli.

Ni ngoma ambayo imeshaanza kuwa gumzo tangu ilipotoka rasmi Februari 8 mwaka huu na kuwafanya mashabiki wamtazame Harmonize katika upande mwingine wa muziki.

**RAYVANNY FT MESSIAS MARICOA-TEAMO**

Kwenye mwezi huu wa mapendeko, Rayvanny naye hayupo nyuma. Februari 10 naye akaachia ngoma yake kali aliyoipatia jina la 'Teamo' ambaye nayo imeshaanza kutetemesha si tu kwenye mitandao ya kijamii, bali kwenye vyombo vingine kama redio na televisheni.

**G NAKO FT MAUA SAMA-GUSANISHA**

'Gusanisha' ni ngoma ya mapenzi, iliyoimbwa na wasanii G Nako akimshirikisha mwanadada Maua Sama. Hii nayo imetoka Februari 9 na kwa jinsi ilivyoimbwa na mpangilio mzuri kwenyer video yake, imeshaanza kuwababamba mashabiki wa bongo fleva na kadri siku zinavyozidi kusonga mbele, ndivyo inavyodizi kushika chati.

IMETOKEA

# Mikosi ya meli hii, wee acha tu

MELI moja ya kifahali iliyobeba watalii ambayo ilikuwa imekwama baharini isijue pa kwenda, hatimaye imekubaliwa kutia nanga bandarini.

Kutokana na wasiwasi wa uwezekano wa kubeba abiria walioambukizwa virusi vya corona, meli hiyo imetia nanga nchini Cambodia baada ya kukataliwa katika bandari za nchi tano.

Meli hiyo kwa jina MS Westerdam, ilizuiwa kutia ngana katika bandari tano barani Asia. Meli nyingine ya kitalii ilitengwa nchini Japan ina zaidi ya maambukizi 200.

Lakini Westerdam yenye zaidi ya abiria 2000 pamoja na wafanyakazi haina maambukizi yoyote. Siku ya Jumanne , meli hiyo ilijaribu kutia nanga nchini Bangkok lakini ikanyimwa ruhusa.

Meli ya wanamaji wa Thai iliisindikiza hadi nje ya ghuba la Thailand ambapo ni kutoka hapo ilipoamua kuelekea Cambodia.

Siku ya Alhamisi, meli hiyo hatimaye iliwasili katika eneo la kutia nanga katika mji wa bandari ya Sihanoukville.

''Mapema leo asubuhi , kuona ardhi ilikuwa kitu muhimu sana'' , alisema abiria Angela Jones kutoka Marekani akizungumza na Reuters, ''Nilijiuliza Je, huu ni ukweli?''.

The Westerdam, inayoendeshwa na kampuni ya America Line kutoka Uholanzi , iliondoka mjini Hong Kong tarehe mosi Februari ikiwa na abiria 1455 na wafanyakazi 802.

Meli hiyo ilikuwa imetarajiwa kuzunguka kwa wiki mbili na katika siku hizo 14 kulikuwa na matatizo ya kuisha kwa mafuta mbali na chakula.

Mbali na Thailand , pia ilifukuzwa na Taiwan, Guam na Japan.

''Tumekuwa na bahati mbaya chungu nzima, tulidhani tunaenda nyumbani kabla ya kufukuzwa'', alisema Jones .

Nahodha wa meli hiyo Vincent Smit alisema kwamba meli hiyo itatia nanga nje Sihanoukville iliruhusu mamlaka kufanya ukaguzi wa kiafya ndani ya meli hiyo.

Abiria baadaye wataweza kuondoka katika meli hiyo na kurudi nchini mwao kutoka mji mkuu wa taifa hilo Phnom Penh. Ubalozi wa Marekani nchini Cambodia ulisema kwamba umetuma kikosi kitakachosaidia raia wake kupanga safari zao.

Uamuzi huo wa Cambodia kuwaruhusu abiria hao kutia nanga nchini humo ulipongezwa na mkuu wa shirika la afya duniani WHO.

'' Ulikuwa mfano wa umoja wa kimataifa ambao tumekuwa tukiitisha,'' alisema mkurugenzi mkuu wa WHO Jenerali Tedros Ghebreyesus.

Kumekuwa na ukaguzi wa kiafya wa mara kwa mara kwa abiria wote na hakujaonekana hata kisa kimoja.

Meli iliopo Japan iliotengwa katika bandari ya Yokohama , kufikia sasa ina visa 200 vilivyothibitishwa , na kuifanya meli hiyo ya Diamond Princess kuwa kubwa kwa maambukizi mengi zaidi nje ya China.

Sio abiria wote waliofanyiwa vipimo na idadi ya visa huenda ikaongezeka. Visa vingine 44 viliongezwa katika jumla hiyo siku ya Alhamisi.

Meli nyengine ya utalii ilitengwa kwa siku kadhaa karibu na pwani ya Hong Kong , kwa kuwa mgeni mmoja alikuwa amepatikana na virusi vya corona. Abiria wote sasa wameruhusiwa kutoka.





Najua Kuoa

# Mapenzi ni raha, wala si karaha

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU hii ni mahsusi kwa wapendanao, nimeamua kuichambua kutokana na jana kuwa siku maalum ya upendo maarufu kama Valentine Day.

Mapenzi ni ridhaa ya watu wawili, mwanamume na mwanamke wanapoamua kuanzisha uhusiano.

Si mwanamume au mwanamke anayelazimishwa kumpenda mwenzake. Kinachotakiwa hapo ni mwanamume tu, kumuonyesha mwenzake na kumshawishi kuwa anamhitaji. Kinachobaki hapo ni ridhaa ya mwanamke.

Na hata wanapoishi pamoja kwenye ndoa, bado ridhaa inakuwa pale pale na mmoja anapochoka kwa sababu zozote zile, ziwe za kweli au za kushawishiwa, ndoa huyumba, tafrani inazuka ndani na hatimaye inavunjika. Mapenzi siku zote hayalazimishwi, ndiyo maana hali inapokuwa ngumu sana, watu huamua kutengana.

Hili limeonekana kwenye filamu ya 'Najua Kuoa' Ni filamu ambayo inatoa funzo kwa wenye ndoa na ambao bado hajaingia kwenye taasisi hiyo. Imechezwa na Riyama Ally, hayati Mzee Majuto, Ally Nogi na wengineo.

Awali, maisha ya Riyama na mumewe Ally Nogi yalikuwa ya raha sana. Waliishi kwa amani na utulivu.

Kuna kijana mmoja anaitwa Hamza, aliyetoka mjini kuja kijijini kumsalimia mama yake.

Huyu ndiye aliyezua balaa. Riyama baada ya kumuona kijana huyo, akili ikamruka, akazuzuka.

Penzi likahama kwa mumewe na kuhamia kwa kijana huyo. Usiku akawa halali anamuota Hamza.

Riyama anamtumia kijana muuza genge ambako ndiko alikomuona, ili amuelezee Hamza alivyokufa juu yake. Kwanza Hamza anasita kuingia kwenye uhusiano huo, lakini kutokana na kushawishiwa pesa na mwanamke, aliingia mzima mzima.

Bila kujali nafasi ya mumewe. Bila kujali ni mke wa mtu, Riyama alijiingiza kwenye mapenzi na kijana huyo, ikawa si siri tena kwenye kijiji hicho.

Kibaya zaidi mumewe akapata habari. Ally Nogi licha ya kufahamu, lakini hakuchukua uamuzi wowote. Mke akawa anazidisha vitimbi ili aachwe, lakini mume akikaza uzi na kudai kuwa yeye anajua kuoa na si kuacha licha ya kuwafumania mara kadhaa.

Visa vyote anavyofanyiwa, lakini wapi, mzee kakomaa tu na mke wake. Riyama akaona ampikie mboga ya jongoo ili amkere apate talaka yake aishi na kibenteni chake kwa raha mustarehe.

Baada kukuta kumbe mboga yenyewe iliyoungwa vizuri ni jongoo, alikasirika akaamua kuandika talaka. Lakini kabla ya kumpa akaichoma moto. Riyama akaamua kwenda kwa mganga ili kumuua mumewe. Ally Nogi anafariki dunia na muda mfupi tu, Riyama anaolewa na Hamza.

Ndugu za marehemu hawakukubali. Nao wakaenda kwa mganga kulipiza kisasi. Hamza akapooza mwili huku Riyama akigeuka kuwa chizi. Ally Nogi tangu mwanzo alipoona visa hadi visa, angeamua kuachana naye haya yote yasingetokea. Alilazimisha kuendelea kuishi na mwanamke ambaye moyoni mwake hakuwa na ridhaa kwake tena. Siku zote mapenzi ni ridhaa ambayo ndani yake huwa na raha na si kutiana karaha, mtu kuishi roho juu kama kaua mtoto wa jirani.

WACHA TUONE

# Ubaguzi Bafta, Oscar utakoma?



NI swali ambalo limekuwa na kigugumizi kujibiwa na waandaaji wa tuzo maarufu za filamu kama wanatumia kigezo cha usawa katika kuchagua washindi.

Kuanzia tuzo za Bafta hadi za Oscar, jibu la swali hilo bado halijapatikana na kuzua malalamiko kwamba kuna upendeleo wa watu wa jamii moja ya wazungu kuwapata washindi.

Watu wengi wanaamini katika uteuzi wa wanaogombea tuzo hizo wanawake, watu weusi na kutoka Asia huwa wanatengwa licha ya kufanya kazi nzuri na zenye ubora.

Kutokana na uteuzi wao kuwa watu wachache na wakati mwingine hakuna kabisa, hata washindi wanakuwa wa kuhesabika.

Kwa ujumla tuzo zote zimeshutumiwa. Hii ni pamoja na tuzo ya Bafta ya Brits inayotolewa nchini Uingereza, na Oscar nchini Marekani.

Tuzo ya Bafta inashutumiwa kwa kukosa uwakilishi baada ya kukosa kuteuliwa watu wasiokuwa wazungu. Hapakuwa na wanawake walioteuliwa katika kitengo cha muelekezaji bora kwa mwaka wa saba mfululiozo.

Katika tuzo ya mwaka huu ya Bafta, washindi kadhaa wa tuzo hiyo walitoa tamko katika hotuba walizotoa kuhusu kutoajumuisha watu wa tabaka mbalimbali na katika uteuzi.

Wakati, Dua Lipa aliponyanyua tuzo yake ya mshindi bora mwanamke Uingereza mwaka 2018, alisema " Tuzo hii iende kuchangia wanawake zaidi katika majukwaa haya, wanawake zaidi watakaoshinda tuzo na wanawake watakaoidhibiti dunia."

Mwaka mmoja baadaye katika tuzo za Brit 2019, idadi ya wanawake walioteuliwa iliongezeka kutoka wanne hadi kumi na wawili.

Lakini hali ilibadilika tena katika orodha ya wateuliwa 2020. Orodha ya wateuliwa wa mwisho katika kitengo cha albamu bora ilikuwa na majina ya wanaume watupu, huku mwanamke mmoja pekee ni Mabel, akiteuliwa katika vitengo ambapo wanawake na wanaume wanaweza kuwania ushindi.

Inapokuja orodha ya wateuliwa ushindi wa tuzo ya Oscar hapa pia uwakilishi sawa ni tatizo.

Filamu kama 'Us', 'The Farewell' na 'Dolemite Is My Name' zote zimejumuisha waigizaji wa tabaka tofuati lakini hakuna muigizaji au filamu kati ya hizo ilioteuliwa. Watafiti kutoka chuo kikuu cha Southern California wametazama fikamu 100 kuu na kugundua filamu nyingi za mwaka 2019 ziliwajumuisha waigizaji wanawake na watu wanaotoka makabila ya wachache zaidi.

Wakosoaji walidhani muigizaji Lupita Nyong'o huenda angepata fursa kwa uigizaji wake kwenye filamu ya Us, lakini hakuteuliwa.

Mnamo 2019, kamati mpya inayotangaza tuzo hiyo ya Oscar iliidhinishwa na iliyokuwa na idadi zaidi ya wanawake na watu wanaotoka makabila ya wachache.

TTY katika vitengo vya uigizaji mwaka huu

Nyota mmoja mweusi aliyeteuliwa kushinda tuzo ya Oscar ni Muingereza Cynthia Erivo. Anasema ni hali ya 'tamu uchungu' kuwa mtu wa pekee wa rangi kuteuliwa.

Sio mara ya kwanza kunazuka mzozo kuhusu uwakilishi wa sawa katika tuzo. Mnamo 2015, kampeni ilioanzisha katika mitandao iliopewa jina #OscarsSoWhite iliidhinishwa, ilifuata ukosefu wa uwakilishi wa sawa katika tuzo ya 2015 ya Oscar.

Watu wengi wanashinikiza mageuzi yafanyike, na kwamba hatua zaidi zichukuliwe kuhusu tatizo hilo kwenye sekta hiyo, lakini swali ni je, sherehe za tuzo zinazowadia zitalizingatia hilo?

# Burna Boy umemchumbia Stefflon?

UTATA mwingine umeibuka kwa mashabiki wa muziki nchini Nigeria, wakitaka kufahamu kama ni kweli mwanadada Stefflon Don amechumbiwa na mwanamuziki nyota Burna Boy.

Picha iliyoleta utata ni ile inayoonesha Steflon Don akiwa amevalia nguo ndefu akiangalia pete ya uchumba kwenye kidole chake.

Inawezekana mastaa hao wameweka picha hiyo katika ukurasa wa Instagram kwa makusudi ili kuwatangazia watu kwamba ni wachumba baada ya kuwa katika uhusiano wa kimapenzi kwa muda mrefu.





## Black Chyna ni mjamzito?

MWANAMITINDO na mpambaji wa video za muziki, Blac Chyna, ameweka hadharani kipimo cha picha cha ultrasound ambacho kimeleta hisia kwamba ni mjamzito.

Mrembo huyo ambaye ni mama wwa watoto wawili, ametumia ukurasa wake wa Instagram na kuweka picha hiyo na kisha kuandika ujumbe 'Baraka za 2020.''

Baada ya kutupia, mashabiki wake walianza kujadili picha hiyo na idadi kubwa wakiamini Chyna ni mjamzito.

## Naira Marley umetolewa ushamba

NI habari mbaya kwa mashabiki wa mwanamuziki wa Nigeria, Naira Marley, baada ya kutangaza kwamba wajanja wameipora akaunti yake ya Twitter.

Rapa huyo ametangaza kupitia mitandao ya kijamii kwamba ukurasa wake huo unatumiwa na watu hao na kwamba wanaendesha kihalifu.

Kulingana na taarifa hiyo, ukurasa huo wa Twitter ulichukuliwa tangu jumatatu ya wiki hii na wezi hao wamebadilisha nywila ya kuingia.





## Tonto kweli umekuwa na busara

KULINGANA na maono ya mwigizaji wa Nollywood, Tonto Dikeh, ni kwamba uhusiano wowote wa kimapenzi ambao hautaridhiwa na wazazi ni vyema ukaepuka.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, ameandika kwamba kama mwanaume umemtafuta wewe mwenyewe ni vizuri ukakaa upande mwingine kwa kujiupusha na jambo baya kutoka kwa wazazi.

"Epuka uhusiano ambao unachukiwa na mama na kumfanya kuchanganyikiwa, Ukweli ni kwamba huwezi kutomuheshimu mama yako ambaye alikutunza na kukulinda kwa hali ya juu,"

## Buriani mkongwe Victor Olaiya

MKONGWE wa muziki nchini Ghana, Victor Olaiya, amefariki dunia.

Mwanamuziki huyo kutoka lebo ya muda mrefu ya Evergreen Music amefariki akiwa na umri wa miaka 89 na atakumbukwa kutokana na umahiri wake wa kutumia chombo cha mdomo wa bata.

Olaiya alianza kusikika kuanzia miaka ya 1950 amekuwa na mafanikio makubwa katika muziki na kujijengea jina.



**MAKALA**



**MIONZI YA SHERIA**

# Hatua muhimu za kuzingatia unaponunua nyumba, kiwanja

**Na John Juma**
**0716217615**

MARA nyingi nimeandika kuhusu ardhi hususan, viwanja na nyumba. Katika kufanya hivyo, mara kadhaa nimejaribu kuwatahadharisha watu namna mbalimbali ya kisheria ya kuepuka kuingia katika migogoro ya viwanja na nyumba hasa wakati wa kununua ( wanunuzi).

Nimewahi kueleza namna au vitu vya msingi,unatakiwa kuwa navyo katika mkataba wa ununuzi wa nyumba au kiwanja.

Nikaeleza umuhimu wa kila kimoja na nikasisitiza kuwa, atayekuwa amenunua ardhi na mkataba wake ukajaliwa kuwa na vitu hivyo, basi si tu atakuwa amefanya manunuzi bora, pia atakuwa amefanya ununuzi bora inaokubalika kisheria.

Ifike hatua, watu wakaelewa kwamba migogoro mingi ya ardhi, huanzia na

kutokuwa makini kwenye ununuzi.

Kutokupata ushauri wa kisheria ni pamoja na kutopitia hatua za msingi za kisheria, kabla ya kufanya ununuzi, kuandikiwa mikataba ya manunuzi isiyokidhi vigezo vya kisheria,

ikiwemo ile ya serikali za mitaa, ambayo hairuhusiwi kabisa kisheria. Hiyo, ni sababu chache kati ya nyingi zitakazokuingiza katika mgogoro.

Leo nitaeleza hatua moja ya msingi sana, ambayo hutakiwi kuifanya wakati wa kununua ardhi.

Umuhimu wa hatua hizo, kwanza kabisa inakuepusha na mgogoro, pale utakapokuwa umezipitia.

Pili, iwepo bahati mbaya utokee mgogoro, basi wewe uliyepitia hatua hizo utakuwa salama na kama ni kesi, basi upo katika mazingira mazuri ya kushinda. Nikuorodheshee:

Kwanza kuna kinachoitwa, kabla ya mkataba (pre- contractual stage). Hiyo, inayo mambo mengi ya kisheria ambayo kuyafuata kwako, kunaweza kukuweka mbali na hatari ya kununua ardhi yenye mgogoro au itayokuingiza katika mgogoro .

Hatua hiyo ndiyo nitakayoeleza kama msingi wa makala ya leo. Kabla ya kueleza hatua hiyo, ni vyema pia nikazitaja hatua nyinginezo japo kwa ufupi. Hatua ya pili, inaitwa ya mkataba (contractual stage). Hii ni hatua ya kupitia na kujiridhisha na mkataba wa ununuzi, ikiwa ni pamoja na kutia saini.

Hatua ya tatu, ina jina 'pre - completion stage", hatua ya 'nne huitwa hatua ya kumalizia (completion stage) na hatua ya tano na ya mwisho, huitwa hatua baada ya kumalizia (post completion stage).

**HATUA MUHIMU**

Kama nilivyoeleza hapo juu hatua nitakayojadili hapa huitwa hatua kabla ya mkataba au "pre contractual stage." Jambo kubwa ambalo linahusishwa katika hatua hii, ni kufanya utafiti wa kitaalam uitwao 'official search.'

Katika hatua hii, mlengwa anayetaka kununua ardhi kupitia ofisi ya mwanasheria, ataandika barua kenda kwa msajili wa ardhi kumuuliza taarifa kamili za nyumba au kiwanja anachotaka kununua.

Msajili wa ardhi atapekua katika kumbukumbu zake rasmi na kutoa majibu sawa na kile kilicho katika kumbukumbu zake.

Mambo muhimu ya kuuliza katika barua kwenda kwa Msajili wa Ardhi, ni jina rasmi la mmiliki linalosomeka katika nyaraka za serikali. Hiyo inasaidia kulinganisha jina la anayeuza na lile linasomeka katika kumbukumbu za serikali.

Kwa kujua jina tu, tayari utaepuka kununua ardhi kutoka kwa mtu ambaye si mmiliki halisi.

Pili, utahitaji kujua iwapo ardhi hiyo imewekwa kama dhamana popote katika taasisi za fedha. Kama imewekwa dhamana basi taarifa zitaonyesha.

Hiyo ni kwa sababu, taasisi za fedha hutuma taarifa kwa Msajili wa Ardhi, katika kila ardhi inayowekwa kwao kama dhamana.

Tatizo la kununua ardhi iliyowekwa dhamana bila kujua, inakuweka katika hatari ya kupata hasara ya kulipa deni, ili nyumba ubaki nayo.

Tatu, utaweza kujua iwapo ardhi hiyo ni ya wanandoa, hasa iwapo wanandoa hao wana mgogoro. Hiyo ni kwa sababu, sheria inampa haki mwanandoa kuweka zuio katika ardhi ya familia, iwapo mmoja wao ana wasiwasi mwenzake anaweza kuuza ardhi hiyo.

Kwahiyo, ikiwa taarifa hizo zimeshapelekwa katika mamlaka ya ardhi, basi utakapopitia hatua hii kabla ya kununua nyumba na utaonyeshwa taarifa hizo, hivyo kuwa salama dhidi ya kununua mali ya familia, ambayo huenda pande zote kitu ambacho ni kama kupoteza.

Nisisitize kuwa hatua hii ni muhimu sana kwakuwa hatua pekee ya kujiridhisha na uhalali wa ardhi unayotaka kununua. Nathubutu kusema usinunue kiwanja au nyumba bila kupitia hatua hii. Naomba kuwasilisha!



**KALAMU YA MWALIMU**

# Wiki ya Sheria, elimu yake iwafikie wanafunzi shuleni

**Na Reubeni Lumbagala**

KILA mwaka nchini, kunakuwepo Siku ya Sheria, ambayo shughuli mbalimbali zinafanyika, ikiwamo utoaji elimu kwa umma kuhusu masuala ya kisheria na kimahakama.

Siku ya Sheria kwa Mwaka 2020 inachagizwa na kaulimbinu isemayo "Uwekezaji na Biashara: Wajibu wa Mahakama na Wadau kuweka Mazingira wezeshi ya Uwekezaji."

Kabla ya kufikia kilele cha Siku ya Sheria, kunatanguliwa na Wiki ya Sheria, ambayo pamoja na mengine, kuna maonesho mbalimbali ya wadau wa sheria, kwa ajili ya kuwapa wananchi uelewa wa sheria zinazotumika mahakamani.

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Job Ndugai, alikuwa mgeni rasmi wa matembezi maalum ya Wiki ya Sheria, yalioanzia Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dodoma na kuishia viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma.

Katika hotuba yake, Spika Ndugai alisema: "Bunge litashirikiana na serikali kuhakikisha mahakama inapata rasilimali za kutosha, ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kutoa haki kwa wakati." Ni kauli hii inayonesha namna ambavyo mihimili inavyoshirikiana katika kuwaletea wananchi maendeleo ya kweli.

Jaji Mkuu wa Tanzania Prof. Ibrahim Juma, akizungumza na waandishi wa habari wiki iliyopita, alisema:"Katika Wiki ya Sheria kutakuwa na maonyesho ya utoaji elimu ya mahakama yatakayofanyika rasmi kuanzia Januari 31, 2020 hadi Februari 5, 2020 katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma na Mahakama mbalimbali nchini."

Wadau ambao wameshirikiana na mahakama katika maonesho hayo kutoa elimu ya sheria kwa wananchi ni pamoja na; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, majeshi ya Magereza na, Polisi, Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake (TAWJA), Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) na Tume ya Haki za Binadamu.

Wadau hawa wamefanya kazi kubwa ya kutoa elimu kwa wananchi ambao wamepata fursa ya kufika katika maonyesho hayo ili kujifunza masuala mbalimbali ya sheria na namna mahakama zinavyofanya kazi katika utoaji wa haki wa wananchi wake.

Sheria ni nyanja muhimu ambayo wananchi wanapaswa kuifahamu japo kwa sehemu hasa katika kutambua haki zao na kuzidai pale zinapokiukwa. Kwahiyo, ni muhimu elimu ya sheria iwafikie wananchi wake katika kujenga jamii inayojitambua ili kupunguza kitendo vya uonevu na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Katika mafanikio ya utoaji wa elimu juu ya masuala mbalimbali ya kimaendeleo kama suala la elimu ya sheria kwa umma, ni vyema elimu hiyo ikaanzia ngazi ya chini yaani kuwaelimisha watoto kujitambua, ili watakapokuwa wakubwa wawe ni watu wanaojitambua na wanaoweza kudai haki zao kwa ujasiri mkubwa katika mamlaka husika.

Kalamu ya Mwalimu inashauri, wanafunzi walioko katika shule za msingi na sekondari nchini wafikiwe na elimu ya sheria ili waweze kufahamu mambo ya msingi kuhusu sheria na haki za binadamu.

Wiki ya sheria imemalizika Februari 05 na kilele chake kimehitimishwa Februari 6, 2020. Pamoja na kumalizika kwake, wadau wamefanya kazi nzuri ya kuwaelimisha wananchi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Pengine, mhimili wa mahakama unaweza kuangalia uwezekano wa kuongeza siku kadhaa mbele ili elimu hiyo muhimu iwafikie wanafunzi walioko shuleni, ambao hawakuweza kufika katika viwanja vya maonesho kupata elimu hiyo muhimu.

Wanafunzi wanapaswa kuelimishwa vya kutosha kuhusu haki za watoto na haki za binadamu kwa ujumla. Watoto wakiandaliwa vyema katika kutambua haki zao, Taifa letu litafanikiwa sana katika juhudi za maendeleo.

Zipo changamoto za ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi, hivyo wanafunzi wakipewa elimu ya sheria itawajengea uwezo wa kujua namna wanavyoweza kuripoti matukio hayo kwa usalama na maendeleo yao.

Wanafunzi shuleni ni wadau wakubwa wa kufanikisha azma ya kufikia maendeleo ya viwanda na uchumi wa kati kupitia kupata elimu bora. Elimu ya sheria itawasaidia wanafunzi kufahamu namna mahakama na utungaji wa sheria bora unavyoweza kuwa chachu ya kufanikisha maendeleo ya biashara na uwekezaji kwa kutenda haki kwa wananchi na kutafsiri vyema sheria za biashara na uwekezaji.

Kwahiyo, wadau wa wiki ya sheria waangalie namna wanavyoweza kufanya ili kuwafikia wanafunzi mashuleni ili kuwapa elimu ya sheria kwani wengi wao hawakupata fursa ya kufika katika viwanja vya maonesho kupata elimu hiyo adhimu.

Mahakama ione umuhimu wa kuwafikia wanafunzi katika kuwaelimisha ili wajitambue na waweze kudai haki zao. Elimu ianze kutolewa kwa wanafunzi shuleni halafu elimu hiyo isambae kwa wananchi wengine. Tafakari.

■ **Reubeni Lumbagala ni walimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Anapatikana kwa simu namba: (+255) 765 409249.**

MAKALA

# Ukeketaji wanasiasa lawamani

## ■Wanadaiwa kuukumbatia, kuhofia kupoteza madaraka

**Na Sabato Kasika**

VITENDO vya ukeketaji bado ni tatizo linaloendelea kujitokeza kwenye baadhi ya mikoa hapa nchini, licha serikali kuweka sheria kali kusaidia kutokomeza ukatili huo.

Inaelezwa kuwa miongoni mwa watu wanaochangia kuendelea kuwapo kwa ukeketeaji katika maeneo mbalimbali nchini ni baadhi ya wanasiasa ambao wamekuwa wakiupigia debe kichinichini kwa maslahi yao binafsi.

Velerian Mgani, ambaye ni Meneja Mradi wa Shirika la Kutokomeza Ukeketaji na Mimba za Utotoni (ATFGM) kutoka Tarime mkoani Mara, ndiye aliyotoa tuhuma hiyo baada ya kufanya uchunguzi wa kina.

Hayo yamefichuka wakati wa kongamano la maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ukeketaji Duniani, lililofanyika Februari 6 mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Kongamano hilo liliandaliwa an Umoja wa Ulaya nchini (EU), likiratibiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA) na kushirikisha wadau mbalimbali wa kupinga ukatili huo.

Mgani aliwashukia wanasiasa na kusema wanachangia kukwamisha juhudi za kumaliza tatizo hilo katika jamii, kutokana na kile anachodai kuwa wanafanya hivyo kwa kuhofia kung'olewa madarakani.



Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Faidha Suleiman (kulia) na wadau wengine , wakifuatilia kongamano hilo.. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

**WANAFANYAJE?**

Meneja huyo anasema, kuna jamii bado zinakumbatia mila potofu na kwamba zinapopata wanaoziunga mkono, hasa wanasiasa zinaendelea kuwepo na kukwamisha juhudi za kumaliza tatizo hilo.

"Wanasiasa wana ushawishi mkubwa katika jamii na waposema jambo wanasikilizwa na ndivyo inavyotokea kule kwetu, kwani wapo baadhi yao katika mikutano wanatamka wazi kwamba mila za ukeketaji zipo tangu enzi na enzi hivyo wananchi waachwe waendelee nazo," anasema Mgani.

Anafafanua kuwa kwa mazingira hayo, baadhi ya koo zimeendelea kukeketa watoto wa kike kana kwamba ni jambo la kawaida na kumbe ni ukatili wa hali ya juu kwa wasichana na wanawake.

"Nimewahi kusikia mwanasiasa akisema, ukeketaji umekuwapo hata kabla ya Yesu Kristo, hivyo wananchi waachwe waendelee na utamaduni wao waliouzoea kwa miaka yote, na wanafanya hivyo ili kupata kura," anasema.

Anasema, umefika wakati wanasiasa wakemewe, wasitafute kuungwa mkono kwa kukumbatia ukatili badala yake watafute kura kwa njia nyingine, na siyo kuhimiza kuendelea kwa mila potofu kama hizo.

Anasema, baadhi ya jamii bado ziko nyuma, hazina uelewa kuhusu madhara ya ukeketaji, na kwamba hizo ndizo wanasiasa wanazitumia kuzishawishi ziwaunge mkono kwa vile na wao wanazitetea, ili ziendelee kuketa.

**NYUMBA SALAMA**

Inaelezwa kuwa elimu ya kupinga vitendo vya ukeketaji itolewe, lakini nyumba salama ni muhimu ziwe nyingi zaidi zinasaidia kuokoa watoto wa kike dhidi ya vitendo hivyo.

Akichangia mada katika kongamano hilo, Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Hope for Girls and Women Tanzania la Mugumu Serengeti mkoani Mara, Rhobi Samwelly, anasema nyumba hizo zimekuwa kimbilio la mabinti wengi.

"Ninasema hivyo nikiwa na mfano hai. Shirika letu limeokoa wasichana 1807 kwa kuwalea katika nyumba salama tunazomiliki ikiwamo ya Mugumu na Butiama, hivyo nyumba hizo zijengwa nyingi zaidi,: anasema Rhobi.

Anasema, serikali na wadau wa kupinga ukatili imejitahidi kutoa elimu, ili jamii iachane na vitendo hiyo, lakini bado vipo, hivyo nyumba salama zijengwe za kutosha kote nchini, ili zitumike kuokoa watoto wa kike.

" Siyo kwamba ninapinga elimu, bali ninachoshauri ni kujenga nyumba salama nyingi zaidi, kwani zimekuwa kimbilio la watoto wanaokwepa ukeketaji kutoka nyumbani kwao na kuwa salama zaidi," anasema.

Anasema, Desemba mwaka jana, nyumba salama ya Butiama ilipokea zaidi ya wasichana kutoka Tarime waliojisalimisha baada ya kukimbia vitendo vya ukeketaji ambavyo wangefanyiwa mwezi huo.

"Desemba huwa ni mwaka wa ukeketaji, ulipotimia tu na wao wakakimbia kuja kwetu, tuliwatunza na kisha tunafanya mawasiliano na wazazi wao kwa kushirikiana na serikali, hatimaye wakarudi kwao," anasema.

Rhobi anasema, kabla ya kuwarejesha, shirika hilo lilijenga uhusiano na wazazi wa mabinti hao kuwaambia madhara ya ukeketaji wakakubali, ukawekwa utaratibu maalum wa kuwapokea huku wakiwa wamehakikishiwa usalama na sasa wanaendelea na masomo.

**KUWATIA MOYO**

Mwakilishi Mkazi wa UNFPA Tanzania, Jacqueline Mahon, anasema, watoto wa kike wanaokimbia ukeketaji lazima wapongezwe na kutiwa moyo.

Anasema wanatakiwa kuwa mabalozi wa kusaidia kupinga vitendo vya ukeketaji katika jamii na kwa watoto wenzao mashuleni.

Anasema, UNFPA inaendelea kusaidia juhudi za serikali na taasisi za kijamii kuendeleza mapambano ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto hadi kufikia sifuri mwaka 2030.

"Kwa hiyo hawa watoto wa kike wanaokimbia ukeketaji, wanatakiwa kuwa mabalozi wa kusaidia kupinga vitendo vya ukeketaji katika jamii, hivyo ni muhimu watiwe kwa uamuzi wao huo," anasema Mahon.

Wakati mwakilishi huyo akisema hayo, Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto, kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, SSP Faidha Suleiman, anasema, ukeketaji ni kosa la jinai. Anasema jeshi linafanya kazi kwa karibu na mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali yanayopinga ukatili wa kijinsia na limekuwa likipata taarifa mbalimbali zinazohusu vitendo hivyo na kuvikabili mapema.

"Mwaka huu unagawanyika kwa mbili, hivyo tunajua kwamba kwa mkoa wa Mara kutakuwa na ukeketaji, nasi tumeshajipanga kukabiliana na tukio hilo kuhakikisha hakuna nayekeketwa," anasema Faidha.

Anasema, polisi ina mkono mrefu na ina watu wake ndani ya jamii, hivyo ana uhakika wazazi watakaothubutu kukeketa watoto wao, watakumbana na mkondo wa sheria, na kuwataka waache mara moja.



Mkurugenzi wa Hope for Girls and Women Tanzania, Rhobi Samwelly (kushoto), akifurahia jambo na mmoja wa washiriki wa kongamano hilo.



Valerian Mgani akihojiwa na waandishi wa habari.

MAKALA

# Hakimu anayeongoza magari

## ■Mtoto wake aligongwa na gari, aendesha kampeni ya usalama barabarani




NI jambo la kushangaza kumuona hakimu ambaye amepewa mamlaka ya kutafsiri sheria, anasimama katikati ya barabara akiongoza magari.

Lakini kwa Monica Dongban Mensem (pichani), kwake si jambo linalompa ukakasi, kwani anapomaliza kazi yake ya kuhukumu watu mahakamani huelekea barabarani na kufanya kazi hiyo ya ziada.

Monica ambaye ni raia wa Nigeria, huongoza magari barabarani katika mji mkuu wa Abuja, kazi hiyo ameifanya ndani ya miaka minane baada ya mtoto wake wa kiume kufa kwa kugongwa na gari barabarani.

Kulingana na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), mwanamke alikutwa akiwa amevalia fulana ya bluu, miguu ikiwa upande, akitokwa na jasho akitumia mikono yake kwa ukakamavu kwa kuongoza magari.

Muda huo magari yalikuwa yamesongamana huku madereva wakipiga honi, kutokana kushindwa kuvumilia kusubiri kwa muda mrefu.

"Wanaigeria wengi huwa hawana subra na inaonekana katika uendeshaji wao wa magari ," Hakimu Dongban-Mensem aliiambia BBC

Hajafahamu ni nani aliyehusika na kifo cha mwanae, lakini anataka kukabiliana na baadhi ya uendeshaji mbaya wa magari anaoushuhudia katika nchi hiyo.

Kabla ya kuingia barabarani, alianza kwenda kwenye vituo vya magari kuongea na madereva juu ya usalama barabarani nchini Nigeria.

Anasema kilichomshtua ni idadi kubwa ya madereva hawakua wamepata mafunzo yanayofaa juu ya sheria za barabarani.

Monica ambaye ana umri wa miaka 62, ameanzisha shirika lisilo la kiserikali lililopewa jina la marehemu mtoto wake, Kwapda'as Road Safety Demand , kwa lengo la kutoa elimu kwa madereva juu ya usalama barabarani.

Kutokana na kutoridhika na hilo, hakimu Dongban-Mensem alitaka kushiriki katika kudhibiti uendeshaji wa magari mwenyewe.

Baada ya wiki kadhaa za mafunzo ya tume ya usalama barabarani alipata ujuzi wa ofisa usalama barabarani wa kuongoza magari.

Ilipofika mwaka 2016, miaka mitano baada ya ajali , alijaribu kwenda eneo alipofia kijana wake katika mji wa kati mwa Nigeria wa Jos.

"Lengo langu lilikua ni kumpata mtu ambae angalau angeniambia au kunielezea jinsi mwanangu alivyokufa." Anasema Monica

Lakini alipofika, alipata uoga, huzuni na hasira kutokana na ghasia alizozione.

Makutano ya Miners, katika eneo la Tundun Wada mjini, ni moja ya maeneo yenye msongamano mkubwa wa magari , ikiunganisha wilaya kadhaa za kibiashara katika eneo tambarare la mji mkuu Abuja

Aligundua miundombinu ya



barabara ulikua duni, aliona jinsi zilivyoharibika na hakuna alama za kuwaongoza madereva na watembea kwa miguu.

**TUKIO LA KUTISHA**

Ilikua ni miundombinu hatari ambayo husababisha ajali nyingi na hiyo ni moja ya sababu zilizomuua mtoto wake wa kiume wakati huo alikuwa kijana wa miaka 32.

"Kwa maoni ya mtu wa kawaida, ninaweza kusema muundo wenyewe wa barabara ni hatari na tuligundua kuwa watu wengi wameuawa katika maeneo mengi ya barabara na hakuna utatuzi uliotolewa na serikali ," anasema.

Maofisa mjini Jos wanasema kuwa wanakarabati barabara na kuongeza kwamba wanatoa pole kwa waliowapoteza wapendwa wao katika ajali za barabarani. Lakini ofisa mmoja anasema kuwa wanaotembea kwa miguu na madereva wanapaswa kuwajibika kuhusu namna wanavyotumia barabara.

Watu katika eneo hilo walimwambia Monica kwamba walimuona mtoto wake akiwa amelala barabarani, lakini hawakuweza kumsaidia.

"Miguu yake miwili ilivunjika na majirani katika eneo hilo waliangalia wakati mwanangu akipata maumivu, kuvuja damu iliyotiririka toka upande mmoja wa barabara hadi mwingine ," Hakimu Dongban-Mensem alisema kwa hasira.

"Alikata roho katika dimbwi la damu yake lakini nina uhakika angenusurika na kifo kama angekimbizwa hospitalini ."

Kijana wake alikua amehitimu shahada ya sheria katika chuo kikuu cha Jos muda mchache na alikua amerejea mjini humo kwa ajili ya kuchukua cheti chake.

"Mwanangu alitaka kuwa mwendesha mashtaka bora duniani lakini alikufa kama kuku mtaani baada ya kugongwa na gari ." aliongeza kusema huku akilia.

Tangu Kwapda'as Dongban alipogongwa na gari, idadi ya watu ambao wameuawa katika barabara za Nigeria imesalia kuwa ni ile ile.

**JUHUDI ZA KUTAKA HAKI**

Kwa mujibu wa mamlaka ya shirikisho ya usalama wa barabarani nchini Nigeria, idadi ya vifo ilishuka kidogo mwaka 2013, lakini tangu wakati huo kati ya watu 5,000 na 6,000 wanakufa kila mwaka kutokana na ajali za barabarani.

Hii inamaanisha kuwa watu 13 hufa kila siku.

Nyingi kati ya ajali husababishwa na madereva wasio na leseni, ni tatizo la mara kwa mara, kwa mfano zaidi ya watu 60,000 mjini Lagos walikua wakiendesha gari bila leseni.

Zaidi ya hayo, hakuna taarifa za usajiri wa magari au kamera za kunasa utambulishi wa madereva wa magari yanayotoroka

Hii inaleta ugumu wa kufuatilia madereva wanaogonga watu na kukimbia, kama aliyemgonga mtoto wa hakimu Dongban-Mensem.

Kama maderava wanaogonga watu na kukimbia wakikamatwa wanaweza kushitakiwa kwa kuua na kukabiliwa na kifungo cha miaka 14 jela , iwapo watapatikana na hatia. Hakimu Dongban-Mensem anahisi hii haitoshi. Anasema wale wanaopatwa na hatia wanapaswa kufungwa kifungo cha maisha na familia za waliouawa wapewe fidia ya pesa.

Lakini hii bado huenda isitoshe kukabiliana na maumivu ya kumpoteza mpendwa wako.

"Nilishindwa kulala, nikiwa na matumaini kwamba kijana wangu atapita mlangoni na kunikumbatia. Anasema na kisha anaendelea "Pia niliacha sahani ya chakula mezani nikitumai atarejea nyumbani akiwa na njaa," alisema.

Hataki mama mwingine apitie haya na ameazimia kupeleka ujumbe wa usalama wa barabarani katika kila mtaa wa nchi ya Nigeria.

# JKT TUMAINI LISILOISHA

## ■Kumaliza rushwa, kukuza uzalendo kwa vijana

**Na Gaudensia Mngumi**



CHANGAMOTO kubwa inayotatiza Tanzania na hata dunia zama hizi ni kukosa watu, waadilifu na waaminifu.

Mawazo ya kuwa na tamaa ya kujitajirisha hata bila kufanyakazi, kuwa tajiri ambaye alilala maskini lakini kwa ulaghai na ujanja ameamka bilionea yanawalazimisha wengi kujiingiza kwenye rushwa, ufisadi na kupoteza uzalendo.

Hata hivyo kama taifa, Tanzania imechukua hatua mbalimbali kuwanusuru vijana ili kupunguza fikira za kujitumbukiza kwenye ufisadi, tamaa za rushwa na pia kuwafanya kuwa wazalendo Zaidi na wachapakazi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Manejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika (pichani), anaeleza mbinu zinazotumiwa kuhakikisha vijana wanafinyangwa katika utaratibu unaowawezesha kuwa waadilifu na wazalendo. Aidha anataja mafanikio, changamoto katika utekelezaji wa masuala ya utawala bora.

Akizungumza na mtandao wa wanahabari wa uandishi wa taarifa za utawala bora jijini Dodoma hivi karibuni Mkuchika , anatoa angalizo kuwa mataifa mengi duniani yaliyofanikiwa kupambana na rushwa juhudi zilifanyika kuwafundisha watoto na vijana wake ubaya wa rushwa kuanzia shule za msingi hadi vyuoni, kuichukia rushwa.

Anasema walifundishwa maadili, kusimamia haki na uzalendo katika ngazi za chini na kwamba mataifa kama nchi za Asia zimefanikiwa na kufika mbali kwenye mapambano dhidi ya rushwa.

Akijibu swali, Tanzania inawaandaaje vijana kwenye masuala ya kuwa raia wema , waadilifu, wanaoheshimu haki za binadamu na misingi ya utawala bora, wenye uzalendo na wachapakazi anasema:

"Kama taifa tumekuwa tukiwaandaa vijana kuwa wazalendo, wenye maadili, wafanyakazi na raia bora kupitia mpango wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), ulioasisiwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere baada ya Uhuru, ambao hata sasa umerejeshwa".

Analitaja kuwa ndilo eneo Mwalimu Nyerere aliloliachia taifa kwenye kuwaandaa vijana kuwa watu bora wanaoheshimu haki za binadamu, wazalendo, wanaotii mri na maagizo, wenye ujasiri, wachapakazi na viongozi waadilifu.

Mkuchika anasema jitihada za kuwafundisha vijana zinaendelea hata leo kwa kuweka wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita katika makambi ya JKT japo ni machache kuliko idadi ya wahitimu wanaomaliza shule leo lakini serikali imeendelea kupanua mafunzo hayo.

"Sserikali ya awamu ya tano imeongeza makambi mengi zaidi . Nia ni kuwafundisha na kuwaandaa vijana kuwa wazalendo, wachapa kazi na viongozi bora. Imeona JKT ni chombo kikubwa na muhimu kiimarishwe ili kupata vijana bora.".

Anakumbusha kuwa wakiwa JKT vijana wa hali tofauti wanafundishwa kukaa pamoja, kuheshimiana, kutii amri na maelekezo hata kama wanatoka familia za maskini na tajiri wote wanakaa, kula , kulala pamoja. Kuimba nyimbo za kimapinduzi na kuendeleza uzalendo na kutii majukumu wanayopewa.

**VITA YA RUSHWA**

Waziri akizungumzia mafunzo ya kukataa ufisadi na kuwa wazalendo anasema kwa Tanzania mitaala ya kufundisha shuleni na vyuoni ipo na kinachotakiwa ni kupanga na kuamua masomo gani ya kuingizwa kwenye mitaala hiyo.

"Wizara ya Elimu imeandaa na kutoa utaratibu wa mafunzo ya kupambana na rushwa. Mathalani kuna elimu ya uraia katika shule za msingi , Civics katika shule za sekondari na katika vyuo vikuu kuna kozi ya Development Studies (taaluma za maendeleo).

" Utaratibu wa masomo upo kinachotakiwa ni kuingiza kozi au kuamua ni mambo gani yakufundishwa kwa mfano maadili, uzalendo kuanzia elimu msingi hadi vyuo vya elimu ya juu na kwamba hata vitabu vya kufundishia vipo." Anasema.

Anaongeza kuwa ili kuwahamasisha vijana kuchukua na kuepuka rushwa shule nyingi zimeanzisha klabu za kupinga rushwa ambazo huzungumzia masuala ya ubaya, udhaifu na fedheha inayotokana na rushwa kwa kushirikisha wanafunzi na wadau ikiwamo Taasisi ya Kuzia na Kupambana Rushwa (Takukuru).

**MAFANIKIO UTAWALA BORA.**

Waziri anapoulizwa kuhusu mafanikio ya utawala bora anasema ni mengi na yameifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za mfano barani Afrika kwa kutumia rasilimali kwa ufanisi na kwa tija kwa manufaa ya wote.

Anasema inasimika kwa mfano kutoa huduma za kijamii kuna vituo vipya vya afya vya kutolea huduma vilivyokarabatiwa kuanzia 2017 hadi 2019 vimefikia 487 kutoka 352.

Wakati hospitali mpya zimejengwa na nyingine kukarabatiwa na zahanati zilizokarabatiwa na kujengwa ni zaidi ya 1,000.

Juhudi zimefanywa kujenga miundombinu ikiwamo reli ya kisasa (SGR), kununua ndege za kisasa na kufufua shirika hilo, kujenga mradi wa kufua umeme wa megawati 2,100 kwenye Mto Rufiji yote haya yanaleta sura mpya katika utawala bora na matumizi ya rasilimali za taifa.

**KUWEKA WATU NDANI**

Waziri Mkuchika anataja kudhibiti vitendo vya wakuu wa Wilaya na Mikoa kuweka watu na watendaji ndani kwa saa 24 kuwa sasa vimedhibitiwa na kwamba ni masuala yanayohusu utawala bora.

Anasema yamefanyika baada ya kuwapa mafunzo ya uongozi wakuu hao na kuwaelekeza kwenye taratibu za kiuongozi.

"Ni lazima mtu yeyote akipewa kazi apate mafunzo awe Waziri, Mkuu wa Mkoa, Wilaya, Wakurugenzi hata polisi nao wamepata mafunzo kuhusu majukumu yao. Ndiyo maana hali imetulia. Maji yametulia mtungini."

Hata polisi wanaokamatwa nao wamefunzwa kuwa kukamata na kuweka ndani si jambo la kufanyika bila kuzingatia sheria.

Wanaelezwa kuwa wanapokamata mwananchi waangalie kosa, wasikamate watu kinyume cha utaratibu na kuwaweka ndani bila kuzingatia sheria.

Anaeleza kuwa hali hiyo imeleta utulivu ndiyo maana taarifa za watendaji na wananchi kuwekwa ndani na viongozi hazisikiki mara kwa mara.

**CHANGAMOTO**

Waziri Mkuchika anapoulizwa ni nini changamoto kubwa katika kutekeleza utawala bora, anasema shida kubwa inayokwamisha utekelezaji wa masuala ya utawala bora ni (umma) watu wengi kutoelewa haki zao za msingi.

Hata hivyo anasema kazi inafanyika na kwamba kinachoendelea ni watu kueleweshwe haki zao kila wakati, kwa mfano hospitalini wafahamu kuwa kutibiwa ni haki yao siyo lazima kutoa rushwa.

Taifa linahitaji kutoa zaidi elimu kwa umma ili wananchi waelewe haki za msingi ili wazipate bila kusumbuka.

"Ndiyo maana tumeamua na kutekeleza kwa vitendo kuwa katika mikusanyiko yoyote tuwaite Takukuru watoe semina kuelimisha jamii kuhusu ubaya wa rushwa. Na wamekuwa wakifanya hivyo."

Watu walikuwa hawadai risiti lakini baada ya kupewa mafunzo na kuhamasishwa na serikali kuwa kwenye risiti kuna kodi za serikali wameanza kudai risiti na wamebadilika si kama zamani.

"Wananchi wanahitaji mafunzo kuhusu maadili, uzalendo, kutaa rushwa, dawa za kulevya . Yote haya yafanyike kuanzia shule za msingi hadi taasisi za elimu ya juu."

HABARI KIMATAIFA

## Uganda wasaidia raia waliokwama China

**KAMPALA,** Uganda

SERIKALI ya Uganda imesema kwamba inatuma dola 60,000 ili kuwasaidia wanafunzi wake waliokwama katika mji wa Wuhan nchini China ambao umetengwa kufuatia mlipuko wa virusi vya corona.

Mamlaka ilisema wasafiri 265 kutoka China na wenzao wa Uganda wametakiwa kujitenga kwa wiki mbili.

Licha ya kuongezeka kwa viwango vya wasafiri kutoka Afrika kwenda China, hakuna kisa kilichothibitishwa kuhusu ugonjwa huo barani kulingana na mwanahabari wa BBC Catherine Byaruhanga.

Raia wa Uganda wameanzisha kampeni ya kutaka kuondolewa mjini humo kufuatia baadhi ya wanafunzi kulalamika kukosa chakula na vifaa kama maski za usoni.

Mamlaka inakadiria kwamba kuna takriban raia 105 wa Uganda mjini humo ambao ndio chanzo cha mlipuko wa virusi vya corona.

Waziri wa afya nchini Uganda aliambia bunge, takriban dola elfu sitini zimetumwa ijapokuwa haijulikani kila mwanafunzi anapata pesa ngapi.

Fedha hizo zitatumwa kwa njia ya kielektroniki kwa simu zao.

Serikali inadai kwamba kuwarudisha nyumbani raia wake kutoka Wuhan kunaweza kusababisha maambukizi hayo kufika Uganda, na iliongeza kwamba miundombinu ya taifa hilo haiwezi kukabiliana na ugonjwa huo.

Mataifa mengi vipimo vya virusi hivyo vimewekwa katika uwanja wa ndege . Na abiria wanaowasili kutoka China wametakiwa kusalia nyumbani kwa wiki mbili kama tahadhari. **BBC**

# Maambukizi mapya ya Corona yapungua

**BEIJING,** China

MAAMBUKIZI mapya ya virusi vya corona yamepungua katika mataifa mengine, lakini nchini China kuna ongezeko la ugonjwa huo katika eneo la Hubei.

Kulingana na shirika la afya duniani, meli ya kitalii nchini Japan ina wagonjwa 44 wapya na kuifanya nchi hiyo kuwa na watu 218, walioambukizwa.

Takwimu mpya kutoka katika mkoa wa Hubei sasa imefikia vifo 116 na watu 4,823 wamepata maambukizi. Hilo ni ongezeko la chini ikilinganishwa na siku iliyopita wakati kulipokuwa na ongezeko ambapo takriban vifo 240 na wagonjwa wapya 15,000.

**Takwimu mpya kutoka katika mkoa wa Hubei sasa imefikia vifo 116 na watu 4,823 wamepata maambukizi.**

Hatahivyo, wagonjwa wengi wanatoka Hubei ambapo watu wengi walipatikana na virusi hivyo hatari kulingana na Mike Ryan, mkuu wa mpango wa afya wa dharura.

Hii haionyeshi mabadiliko makubwa kuhusu mtindo wa mlipuko huo.

Nje ya China kumekuwepo vifo viwili na wagonjwa 447 katika mataifa 24. Siku ya Alhamisi Japan ilitangaza kifo chake cha kwanza cha virusi vya corona ambaye alikuwa mwanamke mwenye umri wa miaka 80 ambaye alikuwa akiishi Kanagawa kusini magharibi mwa mji mkuu wa Tokyo.

"Mwanamke huyo alipatikana na virusi hivyo baada ya kifo chake na kwamba hakuwa na uhusiano wowote na mkoa wa Hubei nchini China ambao ndio chanzo cha mlipuko wa corona", vilisema vyombo vya habari vya Japan.

Siku ya alhamisi wizara ya maswala ya nchi za kigeni nchini Marekani ilisema kwamba ilikuwa ina wasiwasi kuhusiana na athari za mlipuko huo nchini Korea kaskazini, ambayo hadi sasa haijaripoti kisa chochote.

Marekani imesema kwamba itatoa usaidizi katika taifa hilo kulingana na wizara hiyo. **BBC**



Wanafunzi wa Shule ya Ayutthaya, nje kidogo ya mji wa Bangkok nchini Thailand, wakiunda umbo la moyo kwa mikono yao kama ishara ya kuiunga mkono China katika mapambano dhini ya virusi vya Corona. **PICHA: REUTERS**

# Bwana harusi apigwa, akimbilia chini ya basi kujiokoa

**KARACHI,** Pakistan

BWANA harusi ametimuliwa kufunga ndoa na umati wa watu uliokua na jazba baada ya mke wake wa kwanza kuwasili harusini na kutoboa siri kwamba mwanamume huyo alikuwa na wake zaidi ya mmoja.

Asif Rafiq Siddiqi, (30) ambaye alielezewa kama mwanamume mwenye ndevu na mwili wa miraba minne, alisukumwa na kuzabwa makofi na umati wa watu hadi shati yake ilichanika wakati wa ghasia hizo.

Ghasia hizo zilizuka baada ya mke wake wa kwanza kufika harusini hapo na kufichua siri kuwa mwanamume huyo alikua ana wake wawili.

Bwanaharusi alilazimika kujificha chini ya basi na baadae kuokolewa na watu wasiojulikana.

Kuoa mke zaidi ya mmoja inakubalika kisheria nchini Pakistan.

Hata hivyo licha ya kwamba mwanamume anaweza kuoa hadi wake wanne, ni lazima apate idhini ya wake zake wa kwanza kabla ya kuoa tena.

Ilibainika kuwa Bwana Siddiqi alishindwa kutimiza hilo, na Bibi harusi na familia yake hawakufahamu kabla ya mke wa kwanza kuingia ukumbini iliyokua ikifanyika katika mji wa mwambao wa Karachi ambako sherehe zilikua zimepamba moto.

" Kuna tatizo gani dada?" mmoja wa ndugu wa bibiharusi alisikika akiuliza katika video ya tukio hilo liliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

Mwanamke , Madiha Siddiqi, hakupoteza muda wa kuelezea kilichomleta ukumbini.

"Ni mume wangu, ni baba wa mtoto huyu. Aliniambia anakwenda Hyderabad kwa siku tatu," alisema mwanamke huyo ambaye alikua amemshikilia mtoto mdogo wa kiume aliyedai ni mtoto wao.

Baada ya hapo familia ilijaribu kumpeleka katika chumba cha pembeni, jambo ambalo lilimpatia fursa ya kuwataja watu ambao aldai walikua ni ndugu zake.

"Yule ni mamamkwe wangu na yule ni jethani ni wifi yangu ambaye alisema kuwa mama yake alikua ni mgonjwa kwa siku tatu na alikua amewekewa drip ," Bi Siddqi alisema na kwenda moja kwa moja hadi kwa Bibi harusi na kumweleza kuwa asifikiri yeye ni mke wa kwanza.

"Hukujua kuwa alikua ni mme wangu? Hata hakufikiria juu ya mtoto huyo ambaye hana hatia." Alisema kwa hasira mke huyo wa kwanza

Hata hivyo, mke wa Siddiqi alisema kuwa aliolewa na mwanamume huyo mwaka mmoja baada ya kukutana nae katika Chuo Kikuu cha Federal Urdu University, ambako Siddiqi anafanyia kazi.

Halafu akafichua kuwa alioa mke wa pili kwa siri, anayeitwa Zehra Ashraf, ambaye ni mwalimu katika Chuo Kikuu cha Wanawake cha Jinnah kilichopo mjini Karachi, mnamo mwaka 2018.

Mke huyo wa Siddiqi alijua kuhusu ndoa hiyo na aligundua kupitia ujumbe ambao aliupata kutoka kwa mke mpya wa mumewe.

Siddiqi awali alikana kuwa ana mke mpya, lakini baadae alikiri alikua amemuoa mke wa pili.

Mke wa pili ambaye alimfahamisha mke wa kwanza kuhusu harusi hiyo ya hivi karibuni.

Haijawa wazi ni nini kilichotokea baadae. Hata hivyo polisi walioitwa kwenye eneo hilo wameiambia BBC kwamba ndugu wa Bibi harusi walimvamia na kumpiga Asif, wakachana ngua zake na kumpiga kipigo cha kila aina.

Maofisa walimuokoa Bwana Saddiqi, na kumpeleka kwenye kituo cha polisi cha karibu.

Alipotokea tena walimvamia na kumlazimisha kukimbilia chini ya basi. Katika video ya tukio hilo, sauti zilisikika zikimtishia "atoke chini ya basi au walichome".

Kwa uoga , aliwajibu kwa sauti ya juu akisema "subirini dakika moja, dakika moja ", huku akitambaa kutoka chini ya basi. Alipotoka baadhi ya watu waliingilia na kumuokoa.

Rao Nazim, Mkuu wa kituo cha polisi cha Taimuriha aliambia BBC kuwa hakukua na malalamiko rasmi yaliyosajiriwa juu ya kisa hicho.

" Ni suala la kifamilia , na walalamikaji wanatakiwa kwenda kwenye mahakama ya familia kusuluhisha matatizo yao ," alisema. **BBC**

# HADITHI


WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# JUMBA JEKUNDU- 40

Mtunzi anapatikana (0716 350534)

Na Adam Fungamwango




"Kwani mwenyewe anasemaje? Umeshamwambia?" Lilikuwa ni jibu la Eliza.

Aliuliza swali badala ya kujibu kwa sababu yeye ni mtoto wa kike. Haiwezekani akakubali, halafu baadaye mwanamume akakataa, itakuwa ni aibu kubwa.

"Nimeshaongeza na Meze. Amekubali na yuko tayari kutoa barua ya uchumba na hatimaye kukuoa kabisa." Kadili alimtoa hofu.

"Shangazi je, najua hili?" Eliza bado alionekana kuwa na wasiwasi.

"Kumbuka mama yeye alikuwa anataka wewe uwe mke wangu, lakini imeshindikana, sidhani kama atakataa wewe tena kuolewa na mtu mwingine, tena umemchagua mwenyewe, anayemfahamu, lakini pia ni rafiki yangu mkubwa. Ina maana hujaenda mbali."

"Sawa kaka hapo nimekubali."

Kadili alinyanyuka na kumnyayua Eliza akamkubatia kwa nguvu.

"Asante mchumba wangu wa zamani kwa kukubali kuolewa."

Eliza alijikuta akiangua kicheko cha nguvu kwa maneno hayo.

"Eee bwana, mzigo siyo wangu tena, ni wa Meze."

"Ndiyo na mimi haukuwa wangu tena ila ni wa Edina." Eliza alijibu na kuendeleza vicheko.

Ghafla mama Kadili aliingia na kukuta wako kwenye hali hiyo. Ilimshangaza na kumshtusha.

Vijana wake wawili, mmoja kijana wake na mwingine mtoto wa kaka yake ambao alitaka waoane, lakini haikuwezekana kutokana na mazingira jinsi yalivyokuwa.

Cha ajabu leo anawakuta wamekumbatiana laivu, tena kwa vicheko na bashasha. Hakujua nini kimetokea.

"Wamependana ghafla?" Alijiuliza. Kiasi ilimfariji kwa sababu alitaka iwe hivyo.

Aligeuka na kurudi alikotoka kwa sababu hakutaka kuwavuruga watoto wake. Kadili na Eliza walimuona, lakini kabla ya kufanya chochote walimuona akirejea anakotoka na macho yake yakijifanya kama hajaona kitu.

Wakatazamana na kuangua tena kicheko cha nguvu zaidi kuliko cha mwanzo na mama akashtukia kuwa walimuona.

************************************

Mwili ulimsisimka. Alikuwa anaingia tena ndani ya jumba jekundu. Ilikuwa ni baada ya miaka kadhaa. Anakumbuka siku ile ya kwanza alipoingia. Alikuwa ametekwa. Aliingizwa kwenye jumba hilo akiwa chini ya ulinzi wa mabaunsa mawili wakorofi.

Akakumbuka jinsi alivyopita kwenye bustani nzuri za maua na kupelekwa kwenye chumba kimoja kidogo ambacho kilikuwa ni selo au mahabusu.

Akakumbuka jinsi alivyoteswa na mtu mwingine ambaye alionekana kuwa kazi yake ilikuwa ni hiyo tu na si nyingine.

Akakumbuka jinsi alivyopelekwa kwenye bustani ya makaburi ya watu waliozikwa hai kwenye jumbe hilo.

Akili ikarudi nyuma na kukumbuka jinsi mateso makali kwa muda wa siku tatu, kabla ya kutolewa na kupewa chakula, kabla ya kupelekwa kwenye kumbi iliyokuwa imejaa wafanyakazi wa Mama Pauline ambaye kwa sasa ni marehemu na kudhalilishwa vya kutosha.

Si kudhalilishwa tu, bali aliondoka hapo kwa mkwara wa nguvu, asimfuate tena binti Edina, pia kutotoa siri yoyote ya ndani. Anakumbuka aliingia nyonge na kutoka mnyonge zaidi.

Lakini leo anaingia akiwa si yule tena. Alikuwa anajiamini. Ametinga suti moja kali ya 'kufa mtu'. Pembeni alikuwa amemshika mkono Edina. Ni binti huyo ambaye alimletea matatizo yote hayo. Leo hii yupo mikononi mwake.

"Karibu tena ndani ya jumba jekundu." Ilikuwa ni sauti nyororo ya Edina iliyopenya kwenye masikio ya Kadili na kumshtua kutoka kwenye lindi la mawazo ya nyuma, mara ya kwanza alipoingia kwenye jumba hilo.

Maneno yale yalimfanya Kadili mbali na akili yake kurejea kwenye hali ya kawaida, lakini aliangua kicheko na kutikisa kichwa. Edina alijua ni kwa nini Kadili anacheka. Kadili naye alifahamu kwa nini Edina ameongea maneno yale.

"Kumbe na wewe na una utani eee, ushaanza kuniona babu yako unanitania ee." Kadili alimjibu kwa utani huku Edina naye akiungana na kicheko cha mpenzi wake.

Kadili aligeuka nyuma na kuwakaribisha wageni wapya. "Karibuni jamani, hili ndilo jumba jekundu. Hapa ndipo nyumbani kwa Edina."

Wageni hao hawakuwa wengine ni Meze na Eliza ambao walikuwa wanaingia ndani ya geti la jumba hilo kwa mara ya kwanza. Walishangaa kuona uzuri wa jumbe hilo la kifahari.

Ndani tayari shamra shamra zilianza. Ilikuwa ni ile siku ambayo Edina alimwalika mpenzi wake Kadili na wenzake, Meze na Eliza kwa ajili ya tafrija ndogo ya kusherehekea ushindi wa yote magumu waliyopitia.

Tayari kila kitu sasa kilikuwa mikononi wa Edina. Ndiye alikuwa mrithi na mmiliki wa mali zote za marehemu mama yake Mama Pauline.

**********************************

Ilikuwa ni katikati ya sherehe, Edina alipata nafasi ya kuzungumza kitu. Aliwashukuru waalikwa wote, wakiwemo aliosoma nao, anaofanya nao biashara, marafiki zake na wengine wengi.

Alizungumza mengi, lakini mwishowe alimkaribisha mpenzi wake apande jukwaani.

"Sasa namkaribisha mume wangu mtarajiwa. Huyu nimepata naye tabu sana, amenusurika kifo mara kadhaa na kudhalilishwa kwa sababu yangu, na mimi pia nimepata maswahibu mengi kwa ajili yake. Sasa yamekwisha, na kwa sababu tumevumilia vitisho na matatizo yote, tukioana hakuna cha kututengenisha." aliongea maneno hayo kwenye kipaza sauti alichopewa na DJ na kusikika vema.

Kadili alipanda juu ya jukwaa. Kwa muonekano haonekana tena kama kijana masikini kutoka Tandale kwa Mtogole. Badala yake alionekana ni kama afisa mmoja kijana hivi. Kwa muda mfupi akiwa chini ya Edina aliishi ndani ya kivuli cha utajiri wake, hivyo kufanya 'shopingi' ya vitu mbalimbali pamoja na nguo. Alibadilika kwa muda mfupi tu. Edina alimkumbatia Kadili kwa nguvu na sauti ya vigelegele vilisikika pande zote.

Ni kama kufumba na kufumbua hivi. Alichokiona Edina hakukitarajia. Kadili tayari alikuwa ameshatoa pete kwenye kwenye mkebe na iko mkononi mwake, akachukua kidole na kumvisha.

Edina alibubujikwa na machozi. "Uwe mume wangu mwema milele yote." Alimnong'oneza huku akilia.

"Nakuahidi, nitakutunza kama kuku anavyotunza vifaranga vyake." Alijibu Kadili.

"Na mimi nitakuenzi daima dumu, penzi hili ni lako peke yako milele yote." Edina alinong'ona.

Kadili alichukua kipaza sauti naye akaongea machache na kushukuru wahudhuriaji.

"Nakuhakikieni, baada ya miezi miwili kutoka leo, ndoa itafungwa na sherehe itakuwa hapa hapa." Alimaliza na kusababisha mayowe ya furaha kila kona ya ukumbi mkubwa ndani ya jumba hilo.

Wakachukua fursa hiyo kuwakaribisha jukwaani Meze na Eliza. Baada ya utambulisho mfupi kwa marafiki hao, Meze naye alitoa pete na kumvisha Eliza kwani nao, tayari mambo yao yalikuwa yameshakamilika.

Wote wanne hakuna aliyeamini kinachotokea pale. Ilikuwa kama ndoto. Edina kumpenda mtoto wa kimasikini, pamoja na vikwazo vyote leo amefanikiwa kumpata.

Kadili, licha ya woga wake wa kumwambia, alimpenda Edina, pamoja na vitisho na magumu yote aliyokumbana nao, leo yupo mikononi mwake.

Meze, rafiki wa Kadili hakutegemea lolote, zaidi ya kumpa kampani mwenzake, lakin leo amepata mchumba kirahisi tu ambaye ni dada binamu ya rafiki yake Kadili.

Eliza, aliyetolewa Mtoni Mtongani ili aolewe na Kadili kaka yake binamu, na kumuondoa kwenye mpango wake wa kutaka kumuoa mtoto wa kitajiri Edina baada ya kuona anapata madhila kila kukicha, lakini leo anakuja kuolewa na rafiki wa kaka yake binamu.

"Ndugu wapenzi, napenda kuwaambia kuwa ndoa yetu na ya hawa wenzetu itafanyika siku moja, na sherehe pia itakuwa hapa hapa siku hiyo hiyo, nina maana ndoa mbili, sherehe ni moja." Edina alisherehesha na kumkumbatia Eliza.

"Dj lete vitu." Kadili tayari alikuwa amempora kipaza sauti Edina na kuongea yeye.

Muziki uliwekwa. Kila mtu alikuwa akiserebuka na wake. Kadili alikuwa amemkubatia Edina. Aligeuza kichwa pembeni kumuangalia rafiki yake naye alikuwa amemkumbatia Eliza. Meze naye aliuguza kichwa. Macho yao yakakutana. Wakatabasamua kwa pamoja. Wakapeana ishara ya dole. Ina maana wamemaliza kazi.

**Ndugu wapenzi, napenda kuwaambia kuwa ndoa yetu na ya hawa wenzetu itafanyika siku moja, na sherehe pia itakuwa hapa hapa siku hiyo hiyo, nina maana ndoa mbili, sherehe ni moja.**

**Itaendelea Jumamosi**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NYUMBA INAUZWA MIL 70 ARUSHA NGULELO:,** SELF VYUMBA 3 KIMOJA MASTER, SITTING, JIKO NA STORE, INA UMEME âNA MAJI INAFAA KUISHI, FINISHING NA FENSI UNAIMALIZIA.MWENYE NYUMBA **0757 804 970**

**MKOPO WA HARAKA NA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL)** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumaliza tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga: **0758 112 332. Karibu EFL**

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

### KUPOTEA KWA CHETI



**TITUS VICENT MAHONGE** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba P1213-0270 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ARDHI INSTITUTE SEKONDARI mwaka 2003.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi: DAR/MAG/RB/143577/2020.**

115631202

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

LUKUBA WAKARA KIHEZEKO anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili T.248 CLA aina ya Toyo, rangi nyeusi.Chassis namba KE7KEFPK010085 Engine namba 162MJD5080788.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya polisi MBE/MBE/RB/143041/2020

15632002

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MASWA**
**MAHALI MASWA**
**MAOMBI NAMBA 83 YA MWAKA 2017**
**KATI YA**
**SIMON BUJASHI..................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MATHIAS MARCO..................MJIBU MAOMBI**
**WITO / TAARIFA**
**KWA: MATHIAS MARCO POPOTE ALIPO KATIKA JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua maombi dhidi yako katika Baraza hili la wilaya ya Maswa na kwa kuwa ulishaleta utetezi wako hivyo unafahamishwa kuwa maombi haya yamepangwa kusikilizwa siku ya tarehe18/03/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mhe. J.F. Kanyerinyeri Mwenyekiti, Baraza la Ardhi na nyumba wilaya Maswa. Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakaidi wito huu na kushindwa kufika siku iliyopangwa, Baraza litalazimika kusikiliza maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.
IMETOLEWA kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 10/02/2020.

15631902

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# VALVERDE HAITAKI EPL, AITAKA LIGI YA AUSTRALIA



**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa zamani wa Barcelona, Ernesto Valverde amesema angependa kufanya kazi nchini Australia kuliko kwenye Ligi Kuu ya England.

Valverde alifukuzwa pale Barca Januari, licha ya kuwaongoza miamba hao wa Hispania kushinda taji la LaLiga mfululizo na Copa del Rey pamoja na Supercopa de Espana.

Akizungumzia majaliwa yake wakati huu akiendelea kuwa kwenye likizo ya soka, kocha huyo mwenye umri wa miaka 56 alisema angependa kwenda kufundisha kwenye Ligi Kuu ya Australia maarufu kama A-League.

"Watu wananiuliza vipi kuhusu Ligi Kuu ya England na nawajibu 'nzuri lakini mimi ningependa kwenda Australia'," amesema Valverde.

"Maisha katika soka hayaishii sehemu moja na wakati mwingine unatakiwa kufikiria kuchukua nafasi nyingine sehemu nyingine."

Valverde alimtolea mfano nahodha wa zamani wa Barca, Andres Iniesta, ambaye aliondoka pale Camp Nou na kwenda kwenye klabu ya Ligi Kuu ya Japan, Vissel Kobe mwaka 2018.

"Nilikubaliana na Andres wakati aliponiambia anakwenda Japan," aliongeza Valverde. "Niliona ni wakati wake wa kuelewa na kujifunza utamaduni mwingine tofauti, na mimi pia nina husudu kwenda Japan."

# Sarri ajifariji kiwango cha Juvenstus

**TURIN,** Italia

MAURIZIO Sarri amesema Juventus "ni kama imesimama kukua" lakini kocha huyo aliyekalia kuti kavu hana shaka baada ya mabingwa hao wa Serie A kutoka sare ya 1-1 na AC Milan kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Coppa Italia.

Penalti ya utata ya Cristiano Ronaldo ya dakika ya 90 iliikoa Juve na kipigo na kuambualia sare hiyo ya 1-1 dhidi ya 10 iliyokuwa na wachezaji 10 dimbani.

Ikiwa imetoka kupokea kichapo cha kushitukiza kutoka kwa Hellas Verona, na kuwaruhusu Inter Milan kupaa kileleni mwa msimamo wa Serie A wiki iliyopita, Juve hawakuwa kwenye ubora dhidi ya Milan.

Bao la Ante Rebic la dakika ya 61 lilionekana kama lilitosha kuwapa ushindi Milan kwenye mchezo huo wa kwanza, hadi Davide Calabria alipounawa mpira na kutolewa penalti iliyofungwa na Ronaldo.

Juve imeshinda mechi moja tu kati ya nne zilizopita kwenye mashindano yote, lakini Sarri amebainisha hana presha kuhusu majaliwa yake.

"Sina hofu yoyote hapa, naona mambo yanakwenda sawa kabisa, ni jambo lisilofikirika timu kushinda kila mchezo."

Juve ambao ni mabingwa mara 13 wa kombe la Coppa Italia – watawakaribisha Milan kwenye mchezo wa marudiano mjini Turin Machi 4 mwaka huu.






# Man United kumuuza Henderson asiende PSG

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inapanga kumuuza moja kwa moja golikipa wake, Dean Henderson kwa Sheffield United huku kukiwa na kipengele cha kumnunua tena baada ya kuibuka kwa uvumi kwamba, kipa huyo mwenye umri wa miaka 22 amekuwa akifuatiliwa na Paris Saint-Germain na Chelsea.

Henderson amekwa na wakati mzuri kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu akiichezea kwa mkopo pale Sheffield United akizidiwa na Alisson wa Liverpool pekee kwa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao.

Na sasa Man United inapanga kumuuza Henderson moja kwa moja pale Sheffield na kuweka kipendelea chenye bei maalumu ya kumnunua tena kurudi Old Trafford.

Kwa mujibu wa ESPN, sababu ya Man United kupanga kumuuza Henderson ni kuepusha nyota huyo kusajiliwa na PSG wanaomtolea macho.

Pia ESPN imeripoti kwamba, klabu ya Chelsea nayo inamuangalia kwa karibu golikipa huyo.

Keylor Navas kwa sasa ndiye golikipa namba moja pale PSG baada ya kununuliwa kutoka Real Madrid, lakini raia huyo wa Costa Rica mwenye umri wa miaka 33 anaonekana kwamba hatakuwa na muda mrefu wa kucheza kwa mabingwa hao wa Ufaransa.

Huku pia Chelsea nao wakiona Kepa Arrizabalaga kiwango chake kimeshuka hivyo wanahitaji kipa atakayeweza kubeba mikoba yake.

Henderson alitajwa kwamba angerudi Manchester mwishoni mwa msimu, lakini angekuwa na kibarua kigumu cha kuwania namba na David de Gea na Sergio Romero.

# Messi yupo vizuri Barca

**BUENOS ARIES,** Argentina

KOCHA wa timu ya taifa ya Argentina, Lionel Scaloni anaamini nahodha wa Barcelona, Lionel Messi anajisikia vizuri zaidi kubakia kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Majaliwa na Messi katika klabu hiyo yamekuwa kwenye mjadala mkubwa tangu kutokea majibizano ya hadharani na Mkurugenzi wa soka, Eric Abidal.

Baada ya Abidal kubainisha kwamba kuliwa na wachezaji ambao walikuwa hawajitumi chini ya kocha Ernesto Valverde aliyetimuliwa Januari, Messi alijibu kupitia mtandao wa kijamii na kuibua shaka juu ya majaliwa yake pale Camp Nou.


Hata hivyo, Scaloni hana shaka ya kubakia hapo kwa nahodha huyo wa Argentina na mshindi mara sita wa Ballon d'Or – ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2020-21.

"Namuona yeye (Messi) yuko vizuri," amesema Scaloni akiwaambia waandishi wa habari. " Siku ile dhidi ya Real Betis, alikuwa mchezaji bora dimbani bila kufunga. Alitoa asisti na kuhusika katika kila nafasi.

"Yupo vizuri, ametulia, ataweza kuamua kuhusu majaliwa yake, lakini nafikiri anajisikia vizuri zaidi pale."

"Sina hofu yoyote," Scaloni aliendelea. "Anajisikia vizuri akiwa na timu ya taifa ya Hispania na Barcelona. Halafu tutaangalia nini kinaendelea."






# POGBA HANA TATIZO KURUDI JUVE – WAKALA

**MANCHESTER,** England

PAUL Pogba "hana tatizo" kurudi Juventus kwani "Italia ni kama nyumbani kwake" kwa nyota huyo wa Manchester United, kwa mujibu wa wakala wake, Mino Raiola.

Pogba – ambaye anaendelea kujiuguza majeraha ya enka – amekuwa akihusishwa na mabingwa wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juve na miamba wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Real Madrid, huku kiungo huyo wa United akiripotiwa kutokuwa na furaha pale Manchester.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 aliondoka United kwenda Juve mwaka 2012, lakini Pogba alinunuliwa tena pale Old Trafford mwaka 2016 kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia kipindi hicho ya euro milioni 105.

Raiola alizungumzia majaliwa ya Pogba kule United baada ya kushuhudia mchezo wa sare ya kufungana 1-1 kati ya Juve na AC Milan kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya kombe la Coppa Italia, Alhamisi.

"Italia ni kama nyumbani kwa Paul. Hatakuwa na tatizo kurudi Juve, lakini tutaona nini kitatokea baada ya Euro," alisema Raiola akiwaambia waandishi wa habari.

Pogba amekuwa akisumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara, ambapo ameanza katika mechi tano tu za Ligi Kuu msimu huu na kucheza jumla ya mechi nane katika mashindano yote kwa United, ambao wapo nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya mechi 25.

# *Pele: Mimi mzima wa afya njema*

**RIO DE JAINERO,** Brazil

GWIJI wa Brazil, Pele, amekanusha madai yaliyotolewa kuhusu kuzorota kwa afya yake, akisisitiza "yupo vizuri".

Mtoto wa kiume wa Pele, Edinho, mapema mwanzoni mwa wiki hii alielezea kwamba baba yake alikumbwa na "msongo wa mawazo" na kusababisha afya yake kuzorota.

Hata hivyo, mshindi huyo mara tatu wa kombe la Dunia, Pele – ambaye atatimiza umri wa miaka 80 Oktoba mwaka huu – alikanusha madai hayo juu ya afya yake, juzi Alhamisi.

"Asanteni kwa maombi yenu," alisema Pele katika taarifa yake. "Najisikia vizuri. Natimiza umri wa miaka 80 mwaka huu. Nimekuwa na siku nzuri na mbaya. Hii ni kawaida kwa watu wa umri wangu.

"Siogopi, najifahamu na najiamini kwa kile ninachokifanya. Wiki iliyopita nilipewa heshima ya kukutana na Rais wa Shirikisho la soka la Brazil, CBF, nikiwa studio kurekodi makala yangu.

"Kuna matukio kadhaa niliyopangwa kuhudhuria yanakuja. Huwa siepuki kukutana licha ya kwamba ratiba yangu inakuwa bize. Mungu awabariki wote."

Katika mahojiano yaliyochapichwa kwenye GloboEsporte.com Jumatatu, Edinho alisema: " baba yangu ana msongo wa mawazo na ni mtu anayeonekana kukata tamaa na hajahudhuria matibabu."

Edinho aliongeza: "Anajisikia aibu na kwamba ni mtu ambaye hataki kutoka nje."

Pele alitumia miaka 18 akiwa Santos, akicheza mechi 1,281 na kufunga mabao 1,091 ingawa siyo yote ambayo alifungwa kwenye mechi zinazotambulika rasmi.

Anaongoza kuwa mfungaji bora wa timu ya taifa ya Brazil akiwa na mabao 77 na anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# IVAN RAKITIC ATAKA KUCHEZA NA RONALDO

## ●●● Amtaja kuwa bora zaidi kwenye historia, ajivunia kucheza miaka sita na Messi...

**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa Barcelona, Ivan Rakitic, amesema angependa kucheza na nyota wa Juventus, Cristiano Ronaldo, huku Bado kukiwa na shaka juu ya majaliwa yake pale kwenye dimba la Camp Nou.

**Rakitic alikuwa akihusishwa na miamba wawili wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus na Inter Milan kabla ya kufungwa kwa dirisha dogo la usajili la Januari, huku miamba wa Ligi Kuu ya England, Manchester United pia walikuwa wakihusishwa nae.**

Ikaja kuripotiwa kwamba, Rakitic angepewa ofa na mabingwa wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain katika mpango wa kumrudisha Neymar pale Camp Nou mwanzoni mwa msimu.

Rakitic ameendelea kuhusishwa na mabingwa hao wa Italia, Juve na alipoulizwa kama atapenda kucheza na mshindi mara tano wa Ballon d'Or, Ronaldo, nyota huyo mwenye umri wa miaka 31 alijibu: "Bila shaka ningependa.

"Yeye ni mmoja wa wachezaji bora zaidi kwenye historia ya mchezo wa soka.

"Nafurahia kumuangalia namna anavyocheza na anafanya vizuri pale Juventus."

Rakitic kwa sasa anacheza pamoja na nahodha wa Barca na mshindi mara sita wa Ballon d'Or, Lionel Messi na alisema: "Ni jambo la kuvutia kucheza na yeye - ni mtu wa aina yake. Kumekuwa na wachezaji wakubwa katika kila zama, lakini nina uhakika yeye ni bora kwa kipindi cha miaka 15 iliyopita.

"Kwa maoni yangu, yeye ni mchezaji bora wa wakati wote. Kucheza naye kwa kipindi cha miaka sita ni jambo la kujivunia."

Rakitic awali alibainisha namba gani alivyokuwa hana wakati mzuri chini ya kocha, Ernesto Valverde na wasaidizi wake ambao walifukuzwa Januari, akibainisha kwamba alifikiria kuondoka Barcelona.

"Ni sehemu ya soka," alisema Rakitic. "Unatakiwa kuelewa hilo na kuwa tayari (kama kuna uwezekano wa kuondoka.

"Unatakiwa kuwa na furaha, unatakiwa kufikiria kuhusu familia yako na kama nikicheza Barcelona nakuwa na furaha."

## ZISIKUPITE

### PEP AHOFIA KUFUKUZWA

PEP Guardiola amedai kwamba huwenda Manchester City ikamfukuza kama timu yake itashindwa kuifunga Real Madrid kwenye hatua ya mtoano wa timu 16 katika kombe la Ligi ya mabingwa Ulaya. ***(Guardian)***

### MAN UNITED YAPEWA RUHUSA

KLABU ya Manchester United imeruhusiwa kumsajili mshambuliaji wa Lyon na timu ya taifa ya Ufaransa, Moussa Dembele, mwenye umri wa miaka 23, kwa dau la pauni milioni 60. ***(Star)***

### YAMVUTIA KASI GODFREY

TIMU ya Tottenham Hotspur inafikiria kumsajili beki wa Norwich na timu ya taifa ya England, Ben Godfrey mwenye umri wa miaka 22, ambaye thamani yake inatajwa kuwa pauni milioni 50. ***(Express)***

### PSG KUMJAZA NOTI MBAPPE

KLABU ya Paris St-Germain inajiandaa kumpatia mshambuliaji wake, Kylian Mbappe, mkataba mpya ambao utamfanya achukue pauni milioni 41 kwa mwaka, ili kumzuia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kwenda Real Madrid mwaka 2021. ***(Mirror)***

### YAJIPANGA KWA MARTINEZ

TIMU ya Real Madrid iko tayari kuilipa Inter Milan pauni milioni 120 zinazohitajika ili wamsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Argentina, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 22. ***(TyC Sports)***

### MFUNGAJI AANDALIWA SHEREHE

KLABU ya Tottenham Hotspur inapanga kumsherehekea mfungaji wa magoli mengi zaidi katika klabu hiyo, ambaye amefikisha umri wa miaka 80, Jimmy Greaves kabla ya mechi yake ya ligi ya mabingwa Ulaya dhidi ya RB Leipzig wiki ijayo. ***(Standard)***

### LIVERPOOL YAWASHA TAA

TIMU ya Liverpool inapanga kumnunua mshambuliaji wa RB Leipzig, Timo Werner mwenye umri wa miaka 23, mwisho wa msimu huu huku dau lake likitajwa kuwa ni pauni milioni 46. ***(Bild)***

### YATAFUTA MRITHI WA SANCHO

BORUSSIA Dortmund imeanza mikakati ya kumtafuta mrithi wa mshambuliaji kinda wa England, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 19, baada ya kukubali kwamba ataondoka mwishoni mwa msimu huu. ***(Telegraph)***

### LAMPARD KUSAJILI WANNE

KOCHA wa klabu ya Chelsea, Frank Lampard analenga kuwasajili wachezaji wanne mwisho wa msimu huu ambapo wote kwa ujumla wake watagharimu kiasi cha pauni milioni 150. ***(Metro)***

### ALLEGRI ATAJWA TENA MAN U

KOCHA wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri, ameripotiwa amefikia makubaliano na klabu ya moja ya Ligi Kuu England, uvumi ukisema huenda akajiunga na Manchester United. ***(Corriere dello Sport, via Mail)***

### GUENDOUZI KUPATA MKATABA

KLABU ya Arsenal inatarajiwa kuanzisha mazungumzo ya kumsainisha mkataba mpya Matteo Guendouzi, 20, ambapo malipo yake yataongezeka. ***(Football.London)***

HABARI MICHEZO

## Hererimana abaini 'gonjwa' KMC FC

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa KMC FC ya Kinondoni, Hererimana Haruna amesema kwa sasa anafanyia kazi safu yake ya ulinzi pamoja na ushambuliaji ambayo imekuwa na upungufu kila inapocheza mechi.

Akizungumza na Nipashe jijini jana, Kocha huyo alisema malengo yake ni kupata pointi, hivyo washambuliaji wake wanatakiwa kuwa makini kuhakikisha wanapata ushindi katika kila mechi.

Alisema licha ya kutafuta pointi, lakini pia wao wanahitaji kuwa makini na wapinzani wao wasifunge bao, hivyo anahakikisha mabeki wake wanakuwa salama.

"Hali ya timu haiko katika nafasi nzuri inatulazimu tutafute pointi, wakati huo huo tusifungwe, hivyo tutafute ushindi na kuwa makini kulinda kwa ajili ya kujiondoa katika nafasi ya kushuka daraja."

"Nimeshaongea na wachezaji wangu hasa katika nafasi hizo mbili, nilizoona zina shida kutokana na kukosa nafasi nyingi za kufunga katika michezo iliyopita lakini pia na mabeki kutokuwa makini na kuwapa nafasi wapinzani kutufunga kwa urahisi," alisema.

## Twiga Stars yaanza vema

**Na Somoe Ng'itu,** TUNISIA

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), imeanza vema kampeni ya kuwania ubingwa wa Kombe la UNAF kwa kupata ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya Mauritania katika mechi iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Kram hapa jijini Tunis.

Mabao yote ya Twiga Stars yalifungwa katika kipindi cha kwanza cha mchezo huo uliochezeshwa na mwamuzi, Asma Chouchane wa Tunisia.

Amina Ally alikuwa mchezaji wa kwanza kufunga katika mechi hiyo dakika ya saba na kufuatiwa na Oppa Clementi aliyepachika goli la pili dakika ya 15 na Kadosho Shekigenda akifunga la tatu dakika ya 22 ya mchezo huo ulioanza saa 5:00 asubuhi ya hapa sawa na saa 7:00 mchana ya Tunisia.

Bao la nne katika mechi hiyo lilifungwa na Enekia Kasonga huku mshambuliaji mzoefu wa timu hiyo, Mwanahamisi Omary ' Gaucho' akifunga bao la tano la sita huku akaunti ya magoli ikifungwa rasmi na Kadosho dakika ya 44.

Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime alisema baada ya kumalizika kwa mechi hiyo kuwa mchezo ulianza kwa kasi lakini baada ya kuwasoma, waliweza kumiliki mchezo na kupata mabao yaliyowapa ushindi.

Hata hivyo, Shime alisema wapinzani wao walibadilika katika kipindi cha pili na hivyo timu yake ililazimika kupambana ili kulinda ushindi wao.

"Hata hivyo, tumepoteza nafasi nyingi za mabao katika kipindi cha kwanza na cha pili, ila tulivyowafahamu tukajua wapi tunapaswa kupita na kuwazuia, ushindi huu umetusaidia kujiimarisha kuelekea mechi yetu ya pili," alisema Shime.

# KANDA AREJEA KAZINI

**Na Saada Akida**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Deo Kanda amerejea uwanjani baada ya kuanza mazoezi na timu hiyo kwa ajili ya kujiweka sawa kabla hajarudi rasmi dimbabi kucheza mechi za ushindani.

Akizungumza na Nipashe jana, Kanda alisema tayari amepona na kuanza mazoezi na wenzake kwa ajili ya kurejea katika ubora wake.

**Alisema kabla ya kurejea katika kikosi kuendelea na programu ya timu alifanya mazoezi mepesi ya viungo 'Gym' ambayo anaendelea nayo.**

"Namshukuru Mungu naendelea vizuri na tayari nimeshaanza mazoezi, na wenzangu baada ya kutoka katika majeraha, suala la kucheza lipo chini ya kocha mwenyewe," alisema.

Kanda aliumia katika mechi ya watani wa jadi, Yanga na kushindwa kuendelea na mchezo huo uliopigwa Januari 4, mwaka huu katika Uwanja wa Taifa.

Katika mchezo huo Kanda alionekana Kama mashine iliyowaunganisha Simba na alipotoka baada ya kuumia iliwapa nafasi Yanga kupata bao la kusawazisha.



Vijana (ambao majina yao hayakuweza kupatikana) wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Total yanogesha Valentine kwa zawadi*

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kusherehekea Siku ya Wapendao (Valentine Day) Kampuni ya Mafuta ya Total, imeungana na Watanzania kwa kugawa zawadi kwa Wanawake wote waliojaza mafuta kwenye vituo vyao.

Total kwa kuonyesha inajali na kutaka kuhamasisha upendo kila mteja mwanamke aliyefika kuweka mafuta katika kituo cha Total jana, alipatiwa zawadi ya ua la ishara ya upendo.

Akizungumza kuhusu kuhamasisha upendo huo, Mkurugenzi wa Sheria na Uhusiano wa Total, Marsha Msuya alisema wanawapenda Watanzania ndio maana kampuni inawaletea mafuta bora yenye kiambata cha 'Excellium' na bidhaa bora za vilainishi.

"Leo ndio tumeungana na Watanzania kuwaonyesha upendo kwa kuwapatia zawadi ya Sikukuu ya Wapendanao ya Valentine kwa wateja wetu, kwa kuonyesha ishara ya upendo na kuwawezesha kusherehekea.

"Tumeamua kuwahamasisha Watanzania kuwa na upendo kwa kupendana kama Total inavyowapenda Watanzania, na tunawakumbusha kujaza mafuta kwenye kituo vyetu.

"Haujazi mafuta tuu, bali unajaza mafuta ya Total Excellium, ni mafuta yenye viambata vya kuifanya gari yako itumie mafuta kidogo, kwa kwenda umbali mrefu, huku mafuta hayo, yakiboresha injini ya gari yako," alisema.

Jumla ya vituo 16 vya mafuta vya Total ndivyo viliteuliwa kuendesha zoezi hilo, katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Moshi, Mwanza Mbeya na Morogoro.

Total ni kampuni ya kimataifa ya nishati ya mafuta na gesi na ni moja ya kampuni ya kwanza kabisa ya kimataifa kujihusisha katika nishati ya jua duniani kote.

Ina wafanyakazi 100,000 wenye kuchangia dhima ya kampuni ya kuzalisha nishati bora safi na salama.

Aidha, inaizalisha kwa ufanisi zaidi, nguvu na ubunifu wa hali ya juu, huku ikiwa ni nishati ya gharama nafuu inayowawezesha watu wengi kuimudu.

Total ipo katika nchi zaidi ya 130 na inafanya kila linalowezekana kuboresha maisha ya watu wa nchi hizo kiuchumi na kijamii kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira husika.

Michezo
Jumamosi Februari 15, 2020
Nipashe



Rakitic ataka kucheza na Ronaldo UKURASA 30

# Simba, Lipuli hesabu kutawala Samora leo

## ●●● Nonga aionya akimfukuzia Kagere kileleni mwa wafungaji bora, Sven asema...

**Na Isaac Kijoti,** IRINGA

WAKATI Simba ikitarajia kushuka katika Uwanja wa Samora mjini Iringa leo tayari kwa mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya wenyeji wao, Lipuli FC, wameonywa kwamba haitakuwa rahisi kuvuna alama tatu.

**Simba yenye pointi 53 kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo, itashuka dimbani ikipiga hesabu kali ya kuwania alama tatu ugenini kama ilivyofanya dhidi ya Mtibwa Sugar kwa kuichapa mabao 3-0 kwenye mechi iliyopigwa katika Uwanja wa Jamhuri, Jumanne wiki hii.**

Kwa Lipuli itakuwa ikijiuliza kwa kuchanga karata zake vizuri kaada ya kushindwa kuutumia vema uwanja huo wa nyumbani katika mechi iliyopita kufuatia kulazimishwa sare ya bao 1-1 na JKT Tanzania.

Hata hivyo, Simba itakuwa ikitaka kuendeleza ubabe wao wa mzunguko wa kwanza iliposhinda 4-0 ndani ya Uwanja wa Uhuru, shukrani kwa Meddie Kagere na Francis Kahata waliofunga bao moja moja na Hassan Dilunga aliyetupia mawili katika mchezo huo.

Lakini nahodha wa Lipuli FC, Paul Nonga, amesema watapambana kupata pointi tatu mbele ya Simba kwenye mchezo huo wa raundi ya 22 msimu huu.

Nonga ambaye ni kinara wa kucheka na nyavu katika klabu hiyo akiwa na mabao nane, manne nyuma ya straika wa Simba, Kagere anayeongoza kwenye msimamo wa wafungaji bora msimu huu, amesema itakuwa mechi ngumu lakini wamepania kuvuna alama tatu.

"Tunajua ligi msimu huu ni ngumu na kila timu inapambana kutafuta matokeo, hivyo tutakachokifanya ni kupambana na kujituma ili kupata alama tatu kutoka kwa wapinzani wetu," alisema na kuongeza.

"Tunatambua Simba ni timu kubwa ila inapofika uwanjani wote ni wachezaj, tumejipanga kuona tunapata matokeo."

Huku wakikaribishwa na mvua jana katika mazoezi yao, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck (pichani) amesema anaamini wachezaji wake wapo tayari kwa mchezo huo na anatarajia kupata matokeo.

Sven amesema anatambua haitakuwa mechi rahisi kutokana na timu nyingi kucheza kwa kujuhudi hususan zinapokuwa nyumbani dhidi ya Simba.

Alisema lakini anaamini wachezaji wake wataonyesha kiwango kama ilivyokuwa katika mchezo uliopita ugenini dhidi ya Mtibwa Sugar.

"Kwa kiwango tulichokionyesha mechi iliyopita kama tutaendelea nacho ninaamini tunaweza kupata matokeo.

"Lengo letu ni kuendea kujiimarisha kileleni hadi tunatwaa ubingwa, na kila mchezaji analitambua hilo," alisema Sven ambaye amerithi mikoba ya Mbelgiji mwezake, Patrick Aussems.

Simba ipo keleleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 53, wakati Lipuli ipo nafasi ya tisa na pointi zake 29 baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 21.



# Yanga, Prisons ni ushindi na kisasi

**Na Saada Akida**

USHINDI na kisasi! Ndiyo unavyoweza kusema kutokana na kauli za kocha wa Yanga, Luc Eymael na wa Tanzania Prisons, Adolf Rishard, kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu katika Uwanja wa Taifa leo.

Hiyo ni kutokana na wakati Eymael akisema kuwa hakuna namna leo ni ushindi tu, Rishard yeye amesema wanataka kuibuka na ushindi ili kulipa kisasi cha mzunguko wa kwanza.

Katika mchezo wa raundi ya kwanza timu hizo zilipokutana msimu huu kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa, Yanga ilishinda kwa bao 1-0 lililofungwa na Patrick Sibomana wakati huo ikiwa chini ya Boniface Mkwasa, kwa sasa kocha msaidizi.

Eymael aliliambia Nipashe: "Kwetu sisi mechi zetu ni ngumu na ushindani ni mkubwa matumaini yetu ni kuona tunashinda ili kuongeza nguvu ya kufika kwenye malengo yetu tuliyojiwekea, hatuna chaguo lingine zaidi ya kutafuta ushindi."

Naye kocha wa Prison, Rishard alisema: "Tunaweshimu Yanga, tunaingia kwa umakini mkubwa kusaka pointi tatu na kulipa kisasi kutokana na mchezo wa kwanza tulipoteza."

Timu hizo zinakutana leo zote kila moja ikiwa na kumbukumbu yake, ambapo Yanga ilazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City huku Prison ikikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa wapinzani hao wa Yanga katika uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

Baada ya mchezo huo Prison ilitakiwa kucheza dhidi ya Ruvu Shooting, lakini mchezo huo ukaahirishwa kutokana na uwanja kutokuwa na gari la kubebea wagonjwa (ambulance) kama kanuni zinavyoagiza.

9 770856 541002 >